JINSI YA KUWA HURU KUTOKA KWA

# UCHUNGU

**na maelezo mengine kuhusu Ushirika wa Kikristo**



*"Mkiangalia sana mtu asiipungukie neema ya Mungu; shina la uchungu usije likachipuka na kuwasumbua, na watu wengi wakatiwa unajisi kwa hilo" (Waheb 12:15)*

## UTANGULIZI

Sehemu ya kwanza ya kitabu hiki kidogo kuhusu jinsi ya kuondoa uchungu na kusamehe wengine kimekua kiki-wasilishwa mara kwa mara tangu miaka ishirini iliyopita katika sehemu mbalimbali na mikutano ya kibibilia. Mamia ya kanda zenye jumbe hizi zimekuwa zikipeanwa, hapa na pale. Miaka michache iliyopita kijana wetu wa kwanza, Doug-las, alikuwa na mwandishi wake, Chris LaMoreaux, alitafsiri mojawapo ya kanda hizi na baada ya marudio mengi alieza kuchapisha kopi 1000 za kanda hii kama kitabu.

Hapa Wilson Torosyan ni mtoto wetu wa kike, mke wa Ararat Torosyan akiwa mama ya Yeran, Masis na Sevan. Ali-kuwa mfanyikazi wa Kikristo kule misiri kwa miezi minane na kule ureno kwa miaka mitano.

Chris Vlachos alianzisha kazi hii yetu kule Utah mahali paitwapo Provo ambapo alijifungulia na kuendesha chumba chake binafsi cha vitabu. Na huduma yake sanasana hufun-disha kule Salt Lake (ziwa la chumvi) seminari.

Tungependa kumshukuru sana Marjorie Dykema kwa kazi yake kwa kuanzisha mwongozo wa mafundisho ya mas-wala ya kila jarida.

Mtoto wetu wakiume, Evan, anendelea kututolea huduma ya vipawa vyake kama miandiko ya michora katika kila toleo mpya.

**Kama utahitaji kuagiza kopi zaidi:**
**1-99: Senti 90 kwa kila moja**
**100 au > Senti 80 kwa kila moja**
**Wasilian na:**
**Community Christian Ministries**
**Sanduku la Posta 9754**
**Moscow, ID 83843-0180**
**Simu na Kipepesi: (208) 883-0997**
**Barua pepe: ccm@moscow.com**
**Kwa mtandao: www.ccmbooks.org**

**Ikiwa unahitaji kopi moja au zaidi zenye karatasi nzuri zaidi, zapatikana kwa $ 3.50 kwa kila moja kutoka Canon Press (1-800-488-2034 au canorder@moscow.com)**

Toleo hili limechapishwa katika lugha zifuatazo: Kiafri-cana, Kimarikani, Kialbania, Kichina-chepesi, Kichina-kitamaduni, Kikorea, Kireno, Kirashia, Kiispania, Kitelegu, Kiurdu na Kiswahili Afrika mashariki.

*Yeyote apendaye kuchapisha jarida hili katika lugha nyengine tafadhali wasiliana na Community Christian Ministries.*

Maandiko yametolewa katika Bibilia takatifu, NEW INTERNATIONAL VERSION (North American Edition). Copyright © 1973, 1978, 1984 na

## YALIYOMO

**Jinsi ya kuwa huru kutoka kwa uchungu ……………………..3**
Jim Wilson

**Kusamehe wengine ……...……...13**
Jim Wilson

**Hasira ya Mtu …………………..19**
Heather Wilson Torosyan

**Makali ya Ghadhabu……………22**
Jim Wilson

**Kuuchukua uovu ………………..25**
Heather Wilson Torosyan

**Kuuzuia Ulimi …...……………...27**
Chriss Vlachos

**Kujitafakari ………….…..……..29**
Jim Wilson

**Mahusiano na Wazazi …………32**
Jim Wilson

**Upendo Kamilifu ………………..37**
Jim Wilson

**Jinsi gani mwanamke anakuwa Salama ………………...………41**
Jim Wilson

**Mwanamume mwenye jukumu...43**
Jim Wilson

**Nyaraka: Maswali na majibu jinsi ya kuwa Mkristo ...………..45**
Jim Wilson

**Injili ……………………………...52**
Jim Wilson

James I. Wilson, Jinsi ya kuwa huru ku-toka kwa Uchungu © 1995, 1999, 2003, 2004, James I.Wilson Ushirikiano na Canon gandamizi
P.O. Box 8741, Moscow, ID 83843 na Community Christian Ministries, P.O. Box 9754, Moscow ID 83843
Mwongozo wa fundisho katika jinsi ya kuwa huru kutoka kwa Unchungu. Nakalafuatizi © 2003 Marjorie Dykema

Haki zote zimehifadhiwa. Sehemu yeyote ya nakala hii isichapishwe, kuhifadhiwa katika utaratibu wa kugeuza au kusafirishwa katika njia yeyote ile au kusudio, kumememsha, kwa mashine, kwa picha, kwa kurekodi au kwa sababu nyengine, bila idhini kutoka kwa mwandishi, isipokuwa kama vile sharti la sheria za nakala za USA.
ISBN:1-885767-11-0

# JINSI YA KUWA HURU KUTOKA KWA UCHUNGU

*Jim Wilson*

*Jiondolee uchungu wote, hasira na gadhabu, ugomvi na masingizio, yakifuatiwa na kila aina nyingine ya maovu. Kuwa mpole na mwenye huruma kwa kila mmoja wenu, na kusamehana ninyi kwa ninyi, kama vile ndani ya Kristo Mungu aliwasemehe nyinyi. Kuweni waigaji wa Mungu, kwa hivyo, kama watoto wapenzi wapendwao na saishio maisha ya pendo, kama vile Kristo alivyotupenda na akajitoa maisha yake kwa ajili yetu kama sadaka yakupendeza na dhabihu kwa Mungu (Waefeso 4:31, 5:2)*

Katika andiko letu tunashauriwa kuondoa uchungu wote. Kabla hatujaanza kujadiliana ni, kwa jinsi gani na kwa nini haya ni lazima yafanyike, yatulazimu kutambua katika mtazamo huu, kila chanzo cha matendo yetu;

Ni lazima kiwe kile Yesu Kristo ametufanyia sisi pale msalabani. Inatupasa tuwe waigaji wa Mungu katika matendo yetu yote.

Kulikuwako mwanamke mmoja katika Agano la Kale, jina lake lilimaanisha kutabasamu. Jina lake aliitwa Naomi na alihama Israeli hadi nchi nyengine akiambatana na mumewe na watoto wao wa kiume. Lakini mumewe alipata kufa na pia katika miaka kumi iliofuatia watoto wake wote vijana wakafa . Na akaweza kusimulia kisa hiki kwa wakwe zake wajane.

Ruthu 1:13b “Ni uchungu sana kwangu kuliko wenu, kwa sababu mkono wa Bwana umetoka juu yangu.” Alikuwa anafananisha ili kuonesha ni nani aliye na haki ya kuona uchungu mwingi sana.

Na katika Ruthu 1:20-21 “Akawaambia, Msiniite Naomi, niiteni Mara, kwa sababu Mwenyezi Mungu amenitenda mambo machungu sana. Mimi nalitoka hali nimejaa, naye BWANA amenirudisha sina kitu, kwa nini kuniita Naomi, ikiwa BWANA ameshuhudia juu yangu, na Mwenyezi Mungu amenitesa?

Uchungu wake ulikuwa kwa Mungu. Ni Mungu aliyechukua mume wake; na ni Mungu pia ndiye aliyewachukua watoto wake, na ndivyo alimwonea Mungu uchungu mwingi sana. Katika aya hizi tatu alieleza kumchukulia Mungu lawama mara tano kwa ajili ya uchungu wake.

Siku hizi pia kuna watu wengi wa aina hii. Sio tu ni wachungu, bali wanafurahia kuwa wachungu. Kwa njia nyingine ni kama wanapendelea hivyo, na wanaitumia sana. Hawawezi kuelewa lakufanya iwapo uchungu huu watauondoa; hata huwa wanajihisi kana kwamba hawana maana yakuishi tena. Kwa sababu wanapenda kuwa wachungu.

Tunatambua watu wa aina hii duniani, na pia twajua watu wa aina hiyo kanisani. Ni rahisi sana kutambua mtu kama ni mchungu. Waweza kuona katika macho yake, na hata mistari

## BARUA KUTOKA KWA TOLEO LA KWANZA

*Kwa mpendwa mjomba, pokea salamu,*

Ninamshukuru Mango kwa kunipa ushirika pamoja nawe.

Nimejaliwa kusoma ujumbe wako “kuwa huru kutoka kwa uchungu.” Nilihitaji sana sehemu hii katika maisha yangu kwa vile sikulifahamu niliposongwa na dhambi hii. Hivi majuzi, nilikuwa nangangana na uchungu niliokuwa nao na mtu Fulani ambapo singeweza kumpenda kama jinsi impasavyo mkristo. Mume wangu aliniletea jarida hili nisome. Kwa maombi nilipata kusoma ujumbe wako na nikaona dhambi yangu. Jinsi ulivyoelezea, sikungangana na moyo wangu au kumshirikisha mtu yeyote, bali nilimwendea Mungu moja kwa moja na kukiri dhambi yangu. Mungu alinisaidia kumpenda.

Ninakushukuru sana kwa ujumbe huu waajabu, unaobadilisha maisha yetu ili tufanane na Mwokozi wetu.

Hata hivyo ningependa kujitambulisha kwako. Mimi ni Chaitanya Daudi, mke wa C. Stefano Daudi kutoka India (Chuo cha usajili wa Thenashara). Uniombee sana ili Mungu aweze kunifunulia zaidi na zaidi dhambi zangu na kuniwezesha kujikana wmenyewe na kubeba msalaba kwa kumfuata Yesu Kristo.

Kwa ujumbe wako unaotoka kwa neno la Mungu una baraka katika maisha yangu na ninaomba utaweza kubadilisha maisha ya wengine wengi.

Binti yako katika Kristo,
Chaitanya Daudi
Hyderabadi, India.

*Salamu,*
Asante kwa Neno. Ninatoa shukrani zangu tena kwa kitabu hiki kuhusu Uchungu. Hapo jana nilitembelea rafiki yangu na akanishukuru tena kwa kitabu hiki. Amekuwa katika vita vya kinyumbani na kwa miezi michache iliyopita nimeona ile hali yake mbaya aliyokuwa nayo ikibadilika pole pole……….

*Asante,*
Rich

## BARUA KUTOKA KWA TOLEO LA KWANZA

*Hababi wapendwa,*

Jina langu ni ____________. Kwa hivi sasa mimi ni mfungwa katika gereza la Multoriah County-kwa kutumika kifungo cha siku 180, kutokana na tabia yangu ya ulevi, siku baada ya siku, na upotovu wa nidhamu kwa uma.

Hivi majuzi, nilipokea jarida lako kwenye taka na baada ya kulikausha, lilikuwa lenye nguvu sana tena zawadi kwa wakati ufao kunisaidia akili yangu, mwili na roho iliyovunjika.

Halikosi kamwe kuwa kando yangu mpaka limechakaa. Watu wengi na wengi zaidi wanalihitaji, lakini ni mimi pekee huweza kuwaazima kwa mkono baadhi ya chapa zake ili kudhihirisha hitaji lao la kweli la jarida hilo.

Hakuna mtu yeyote mule afisini mwa Kasisi afahamuye penye jarida lako hili litokako, huku wakisema hawajawahi kuliona wala kuwa na moja hapo mbeleni. Ni mimi na wewe kwa hakika twajua ni kwa nani na ni wapi uitokako. Limenibadilisha mwenendo na maisha yangu………

Na Mungu awabariki sana kwa kuwa nuru na tumaini limeweza kunirudi tena maishani mwangu kupitia kwa Jina Lake.

*Mungu awabariki, na awahifadhi!*

katika kipaji chake—hata kama mtu angali mchanga. Waweza kuona kwa midomo yao, waweza pia kuona wakati wanatabasamu au kucheka. Ni wachungu sana na waweza kuona waziwazi. Waweza kuona katika maongeo ya sauti yao. Waweza kuona wanapojaribu kukanusha ya kwamba hao si wachungu. Uchungu ndio kiunganishi na hueneza kila kitu.

Katika Bibilia kuna watu wengine walio wachungu kama vile Naomi. Hata hivyo ni wachache tu. Kwa mfano Yona alikua mchungu. Mungu akamwambia Yona, “Je! Unatenda vyema kukasirika kwa ajili ya mtango?”

Naye akasema, “Ndiyo, natenda vyema kukasirika hata kufa.” (Yona 4:9)

Alidhania ana haki juu ya hasira yake. *Ninapenda kuwa mwenye hasira. Mungu, unafanya makosa kuwasamehe watu. Sitaki uwasamehe watu.*

Watu hupenda kushikia wengine mambo fulani fulani. Lakini fundisho letu latuonya kuondoa uchungu wote ndani mwetu, na kuzingatia upole wa moyo. Hapa kuna swali! Je, yawezekana kuwa na fadhili, mwenye penzi, moyo wa upole na hali kadhalika mwenye uchungu kwa wakati mmoja? Haya yote ni malengo yatokanayo ndani ya moyo. Kufafanua neno, upole wa moyo, linahusisha moyo wenye upole. Uchungu pia humo ndani ya moyo. Lakini haiwezekani uwe na hisia mbili tofauti, ambazo zinagongana kutoka ndani ya moyo.

Mtume Paulo anatuambia tuondoe uchungu wote, na tuwe wenye fadhili na kupendana sisi kwa sisi. Kwa hivyo, ni lazima uchungu usondolewe kabisa. Kabla ya uchungu huu kuondolewa, yatupasa kwanza kujua uchungu ni nini– na kwamba uchungu upo.

Na unaweza kutambulika kiurahisi tunapowaona watu wengine wakiwa wachungu. Lakini sio rahisi tujione wenyewe tunapokua nao. Kwa hivyo,ni vizuri sana tena muhimu jinsi Bibilia inavyo pambanua shida hii.

Tuchukulie kwamba mkristo ametenda dhambi. Kwa mfano amesingizia uongo. Na sasa anaposema huo uongo, je, huwa anaaibika au huwa anahisi uchungu? Jibu ni kwamba huwa anahaibika.

Tunapotenda dhambi, sisi huwa tunaaibika;na inaeleweka waziwazi. Na je, hebu tuazie kwamba mtu mwengine amemusingizia uongo huyu mkristo na kueneza habari hizi kila mahali kwa jiji. Je, ahisije sasa hivi? Mwenye hatia au uchungu?

Hatia ni ile hisia tuipatayo moyoni baada ya kutenda dhambi, na *uchungu ni ile hisia ambayo hutushika wakati wengine wanatutendea mabaya au dhambi*. Na tendo lile la uchungu linapambanuka waziwazi kupitia hisiya za wengine. Na kama tungelitenda dhambi, tungeiuzunikia na tungelijua ya kwamba yatupasa kukiri na kuziacha dhambi zetu.

Twaweza kukosa kukiri dhambi, sio kwa sababu hatujui lakufanya. Lakini tufanyeje na hatia ya wengine? Kila mara uchungu hupimwa kwa dhambi ya wengine—hata kama ni ya haki au kudhaniwa.

Hebu fikiria dhambi ya kudhania. Mara nyingi twaweza kuonea mtu uchungu kwa alilosema, na ilihali kwa hakika hakusema jambo kama lile. Tulisikia ripoti la uongo na sasa tuna uchungu. Twamungojea atuombe msamaha jambo ambalo hawezi. Je tutaendelea kuona uchungu siku zote kwa sababu hakuomba msamaha kwa jambo ambalo hakutenda?

Kwa bahati mbaya, watu wengi wachungu hawawezi kufikiria kuna uwezekano wa hao kuwa wachungu kwa dhambi ya kudhania. Na kama vile uchungu unavyoeleweka, hatia ya yule mtu mwengine kila wakati huwa ni kweli. Kwa mtu kama huyo kwa kujaribu kuwa huru kutoka kwa uchungu, inakubalika nao kufanya kweli ya yule mtu mwengine*, mradi tu wajiondolee mbali uchungu wao.*

Je, na dhambi ya kweli? Kuna watu wengi walio wachungu ambao kwa kweli walidhulumiwa na mkosaji. Kwa hivyo tutachukuliaje kosa la kweli?

Uchungu hulingana na dhambi unayohusika nayo kwa njia yeyote ile. Haijalishi dhambi hii ni kubwa kiasi gani, inategemea uhusiano wa karibu kwa dhambi ile. Kwa mfano, uovu mbaya sana na mkubwa zaidi umetokea kule Irani, Elsalvador, au Kolombia, tutafanyaje? Kweli tutasoma habari zake, lakini hatutapatwa na hatia. Tutasoma habari zake, lakini hatutahisi uchungu. Twaweza kutishwa sana au kushangazwa sana, lakini hatupatwi na hatia, na hatuhisi uchungu. Hata hivyo, ilikuwa dhambi mbaya sana, na kwa hakika mtu aliitenda hio dhambi. Kwa hivyo hautegemei ni ukubwa gani wa uovu ulivyo, bali *inategemea ule uhusiano uliopo kati yangu na yule mtu mwingine*. Uchungu uhusika kati ya watu walio na uhusiano wa karibu.

Ni nani huenda wakawa wataka? Jibu ni rahisi: ni Baba, mume, wandugu, wadada, mabwana, mabibi, watoto, mpenzi mume, mpenzi wa kike, wakaaji wa chumba kimoja, waheshimiwa wa karibu, waheshimiwa wadogo, wafanyakazi wenzio, wafanya biashara, na labda watu wengine wa jamii—wazazi wa wazazi wetu, wajomba, na wengineo. Pia kuna watu wengine waliowachungu dhidi ya Mungu.

Hatuwi wachungu kwa uovu ulioko kando na wahusika wetu wakaribu. Uchungu hutokana na dhambi ya mtu mwingine aliye karibu sana nasi, na ambaye ametutenda jambo baya. Jambo hilo laweza kuwa dogo. Sio lazima liwe kubwa, *mradi liwe karibu sana nasi.* Je huwa anachukua soksi zake? Hapana? Waweza kuwa mchungu kwa jambo kama hilo? Sawa, haiwezekani, lakini jee akifanya kitendo hiki mara 5,000?

Waweza kufikiria unahaki ya kuwa mchungu. Lakini Bibilia hairuhusu mtu yeyote kuwa na haki ya kuwa mchungu. Fundisho letu lasema hivi; *uondoe uchungu wote.*

Mwangalie sana mtu asiipungukie neema ya Mungu; shina la uchungu ilisije likachipuka na kuwasumbua na watu wengi wakatiwa unajisi kwa hilo. *(Waebrania 12:15)*

Hapa fungu hili laelezea uchungu ni kama mzizi. Mzizi ni kitu ambacho kimejificha na hakiwezi kuonekana. Lakini kun-

**BARUA KUTOKA KWA TOLEO LA KWANZA**

*Mpendwa Jim,*

Nilisoma jarida hili, "Jinsi ya Kuondoa Uchungu." hapo mwisho mwisho wa 1993. Ulikuwa kama ufunuo mwingine kutoka kwa Bwana ambapo nilijihisi nianze maisha yangu upya lakini kwanza nipate kumusamehe mme wangu ambaye tumetengana kwa miaka 10 tayari na hakuna siku nyingine wala mahali nitamlaani mara kwa mara) na pia kulikuwa na rafiki yangu, tuliyesoma naye (tumekuwa marafiki wa karibu sana kwa miaka 14 kabla hajanisaliti nilipopata bahati ya kupata nafasi ya daraja ya kuniwezesha kuingia pahali bora katika chuo cha kisayansi cha Presidium). Nilisoma tena na tena jarida hili na sikuweza kuuzuia mushtuko kwa mshangao niliokuwa nao na aina gani ya upumbavu niliokuwa nao kuhisi uchungu kwa ajili yao, mimi nilimjua Yesu vizuri sana na nikakumbuka yale yote niliojifunza kwake maishani. Nikaanza kuomba kwa Bwana aweze kuniondolea dhambi hii. Sikutokwa na machozi ya usafisho niliyokuwa nikitokwa nayo nilipotubu na kumpokea Kristo kama Mwokozi wangu badala yake nilijihisi kuwa na raha na kufurahia kwamba niliomba na kuomba na kujihisi kukuwa mtu tofauti. Ni muda mrefu nikikumbuka; kumekuwa na watu kama hawa maishani mwangu, ili hali wazo hili halimo moyoni mwangu: ni jambo nimekaukiwa nalo kiasi cha 2 x 2 = 4. Nilifurahia sana na NIMEKUWA NA FURAHA kuwa na silaha hii ya Mungu dhidi ya Uchungu.

Marafiki zangu wote wako na jaride hili kwa lughaa ya kirusi na kwa hao wote nikasikia, "Nell, ni la ajabu tena rahisi!. Ninafuraha sana kuelimishwa kuhusu kweli hii ituwekayo huru" Sijui ni nani aliyenipa kijitabu hiki kwa sababu kulikuwa na kundi kubwa sana kutoka kule Amerikani na walikuja na vitabu vingi vizuri. Lakini kuelewa kwangu ni kwamba alikuwa malaika wa Mungu aliyekiweka katikati ya vitabu vingine, la sivyo ningejithuru mwenyewe kwa uchungu niliouhisi.

Na ni vigumu kuwazia furaha niliokuwa nayo nilipopokea barua kutoka kwa JIM WILSON mwenyewe. Mapenzi ya Mungu yatimizwe.

Nellie Provolotsaya
Novosibirsk, Urusi

## BARUA KUTOKA KWA TOLEO LA KWANZA

*Mpendwa Jim*,

___________ ni rafiki yetu mzuri sana na tunashiriki pamoja kanisani. Hakosi kutuletea kitabu chako "Jinsi Ya Kuwa Huru Kutoka kwa Uchungu" bila kukoma. Wiki iliyopita niligawa rafiki aliyehitaji ushauri wa kumusaidia kaka yake na shemeji yake kuhusu sehemu hii ya uchungu. Hapo chini kuna sehemu ya arafa yake ya mtandao jinsi alivyo nijibu.

"Jaride hili la Uchungu nilitumia shemeji na ndugu yangu. Alikisoma toka mwanzo hadi mwisho na akamsihi mkewe afanye hivyo. Hakutarajia mke wake kukisoma, na kufikia kiwango cha yeye kumuongelesha walikuwa wanaelekea wiki ya pili bila kuongeleshana. Aliomba mkewe msamaha kwa mambo kadha wa kadha ya kuudhi aliyomtendea na akaondoka kuenda zake kazini.

Basi, aliporudi nyumbani kutoka kazini, alimpata mkewe akilia, akamwambia anasikitika na kwamba hatambui madhara aliyomsababishia kwa Uchungu na maovu yaliyokua moyoni mwake. Alisema kwamba hiyo ndio mara yake ya kwanza yeye kukubali makosa yake."

"Aliniita ili kunirudishia shukrani kwa kumutumia jaride hili. Yani ninamaanisha alinishukuru tena na tena na akaendelea kunisihi kwamba angelipenda tu anionyeshe shukrani zake kwangu. Akasema jaride hili limembadilisha maisha yake kabisa, hata jinsi anavyohudumia watu pale kazini (na kisia nivizuri nikisome pia)"

*Nilitaka tu nikujulishe jinsi kilivyogusa maisha yao.*

auezekano wa ushahidi wa kuonyesha wakati dalili zake zitachipuka.

Mzizi hufanya vitu vingi. Jambo la kutoiona mizizi, haimanishi haitaonekana na haionekani,ndipo baadaye hujitokeza waziwazi kama mizizi.

Tunda lililozaliwa linaonyesha uhusiano kamili kwa shina linalolizalisha. Shina la mti wa tofaa hutuzalishia matofaa. Na ikiwa pangekuwa na shina chungu, lingezalisha matunda machungu.

Na hivi ndivyo aya hii inavyo maanisha. Uwe macho isiwe shina lolote la uchungu litainuka, kusababisha shida, na kuchafua watu wengi, ikimaanisha kufanya watu wengi kuwa najisi. Je umewahi kuona uchungu ukienea kanisani? Uchungu waweza kuenea katika mikutano kama moto ulao. Unaweza kuenea hata mahali pa kazi au kwa bweni. Mtu mmoja akabashiri, kwa nini hivi? Alikuwa mchungu, wacha shina lijitokeze nje na kuzalisha tunda. Alishirikisha wengi na wakawa wachungu. Mwandishi wa kitabu cha Waebrania anatuonya sisi kuhusu jambo hili. Anatuambia tuwe macho tukalishwe neema ya Mungu. Unapoukubali uchungu huinuka na kuchafua watu wengi. Unafanya watu wengi kuwa najisi.

Hufanyika nini ikiwa mtu ataweka uchungu ndani mwake kwa miaka nyingi? Hufanyika nini kwake kimwili? Anaweza kuwa mgonjwa kimwili? Chukulia kwamba ni uchungu ambao umesababishwa na baadhi ya watu wakifamilia. Na ameuweka ndani na hajaushirikisha kwa wenziwe. Kwa hivyo hajawatia taka watu wengi—amejinyamazisha nao. Anapojinyamazisha nao kwa miaka kadhaa, mwishowe anaanza kupatwa na maradhi. Anamwendea dakitari naye anamwambia, "wewe umesema kweli, wewe ni mgonjwa. Lakini ugonjwa wako sio ambao mimi hutibu. Nitakutuma kwa daktari mwingine tofauti."

Basi anamtuma kwa mtaalam wa akili, naye mtaalam anakubali. "Sawa, ni kweli wewe ni mgonjwa. Nami ninaelewa kwa nini wewe ni mgonjwa. Wewe mgonjwa kwa sababu ya kumwonea babako uchungu kwa miaka 20. Miaka hii yote, umeuzuia moyoni mwako na imekolea ndani mwako. Sumu hii umeiweka ndani mwako na ukali wake ndio unaofanya mwili wako uwe mgonjwa: Basi kile ningependa ukifanye ni kwamba uende nyumbani na ushirikishe babako katika uchungu wako. Kwa nini ujinyamazie na uchungu huo na uwe mgonjwa? Funua uchungu wako kwa wengine. Fanya kila mtu awe mgonjwa."

Basi ulimwengu una suluhu mbili. Ufiche uchungu moyoni ujitakie ugonjwa, au ukaufunue ugonjwa huu waziwazi na uenee kila mahali.

Suluhisho la Mungu ni kuliondoa shina lote. *Lakini hapa panahitaji neema ya Mungu*. Lazima mtu aelewe kwamba Bwana Yesu Kristo ana uweza wa shida hii yote. Yeye ni chanzo cha neema.

Wakristo hawastahili watumie suluhisho la kidunia kuondoa uchungu. Wakristo wanaoiga dunia, huwa na chaguo mbili duniani. Bibilia inatuambia ya kwamba tuondoe uchungu

wote kabisa. Haistahili kujinyamazia nao wala kushirikisha wengine. Uusalimishe kwa Baba Mungu, kwa njia ya mwana.

*Lakini, mukiwa na wivu wenye uchungu huwa ugomvi mioyoni mwenu, msijisifu, wala msiseme uongo juu ya kweli. Hekima hiyo siyo ile ishukayo kutoka juu, bali ni ya dunia, ya tabia ya kibinadamu, na shetani. (Yakobo 3:14-15)*

Wakati nilikuwa mwanafunzi mchanga wa manuari kule chuo cha Naval Academy, nilidhani kwamba uchuki na uivu niliouzingatia ungeniwezesha kukomaa. Nikawazia upandapo cheo zaidi, ndivyo unavyokomaa zaidi, na sivyo ndivyo ilivyo kuwa. Lakini nilivyoendelea kuwa na umri mkubwa niligundua uivu kuzidi kuniongezekea. Uchungu ukafurika. Isipokuwepo suluhisho kwa jambo hili, watu hawawezi kupungukiwa na uchungu kwa kukomaa. Huzidi kuwa wachungu miaka yote. Uchungu huzidi kuongezeka zaidi na zaidi.

Na ikiwa utaficha, uchungu wa husuda ndani mwako, utaanza kuwa na matendo ya uovu. Tabia hii sio itokayo mbinguni. Ni dhahiri imetoka kuzimu na ni ya shetani. Kila tendo la uovu latokana na tabia hii. Kwa hakika tunashida kubwa, kulingana na jinsi mambo, yatakanavyo kuwa. Basi je tutauondoaje huu uchungu?

Kabla ya kuondoa huu uchungu,tunastahili tuelewe ya kwamba tuna uchungu.Tutajuaje tuna uchungu?.

Mfano mmoja mzuri wa sheria ya utumwa ni huu. Hali *uchungu hukumbusha kila jambo lililopita*. Umeyasikia maelfu ya mazungumzo katika maisha yako, ambayo mengi yake hauwezi kuyakumbuka. Lakini jambo hili lilifanyika miaka tano iliyopita, na bado unaweza kukumbuka kila neno lililonenwa, kimatamshi na mabadiliko ya sauti ilivyotoka. Unaelewa vizuri sana ni nini kilitokea—hivi kumaanisha wewe ni mchungu.

Mtu anaweza kukataa na kusema kwamba ni vizuri pia kuwa na kumbukumbu nzuri ya mazungumuzo ya kustaajabisha.Kuna uwezekano hivyo? Ndivyo,bali sio vile. Kwa nini iwe hivyo? Kwa sababu kukumbuka huwa kunasaidiwa na *kufikiria, fikiria, na kufikiri zaidi*. Sio kawaida ya watu kuchochea sana juu ya mambo ya ajabu. Nimewahi kutoa ushairi mchache kwa watu ambao ndoa zao ziko hatarini kuvunjika. Nimewajua na wengine wao tangu kuoana kwao, na wakati wa furaha katika maisha yao. Na wakati wa talaka hawawezi kumbuka hata wakati mmoja wa furaha waliokuwa nao hapo awali. Kile ambacho wanaweza kukumbuka ni yale mabaya wamekuwa wakipitia mara kwa mara. Kwa hivyo wana uchungu.

Hivi haimaanishi hawakuwa na wakati wa furaha. Lakini ni vile kila mmoja anaangalia vile alivyo mzuri na vile mwenzake alivyo mmbaya.

Mtu akiwa hodari wa kumbukumbu ya mambo yote, yaliyofanyika miaka iliyopita akiwa angali mtoto, au kijana ama msichana, na kukumbuka kule kuwe kwa kulaumu mtu mwengine, pale huonyesha hali ya uchungu. Na suluhisho la uchungu ni kuuondoa kabisa.

Kule Dallas na Texas, nilikuwa na maarifa ya ajabu sana.

## BARUA KUTOKA KWA TOLEO LA KWANZA

*Jim,*

Nilitaka kukushukuru kwa kitabu hiki cha usiku na mchana ulichonitumia . Nilisoma nusu yake siku ya kwanza na, nilipokuwa nikisoma kuhusu Uchungu, nilijifunza mambo Fulani kunihusu. Nilitaka tushirikiane kwa kifupi yale nimeyapata kutoka kwa kitabu hiki Uchungu. Mimi nina miaka 38 na nimekuwa mkristo maisha yangu yote, lakini sikuweza "kuushika" kabisa hadi nilipojitoa kabisa maisha yangu kwa Kristo nilipohusishwa kwa urejesho wa tarehe 4,Novemba,1995. Katika miaka ya mapema ya ujana wangu nimekuwa na shida ya kukaukiwa na ngozi ya vidole vyangu vikipasuka na kuvuja damu pia kutokwa ngozi na vikawa uchungu sana. Nimetafuta usaidizi wa kila aina ya matibabu ya ngozi iliyokaukiwa katika vituo mbali mbali vya matibabu, nikianzia na madawa kutoka kwa watu wa ukoo, na vitu nilivyopewa na marafiki na watu waukoo kufuatana na hali niliyokuamo. Pia niliweza kutibiwa na wana Anga wa U.S., wakuu wa Dermatologia, nilipokuwa Texas kwa mazoezi ya kwanza. Sijawahi kupata matibabu yenye usaidizi na mabadiliko mazuri zaidi kama haya kwa muda mrefu. Nilijaribu kutumia vifaa vya unyevu, mpira au mifuko ya pamba nilipoenda kulala na hata wakati wa siku mbovu za kazi.

Nilipopokea jarida lako la Uchungu nililipakia kwenye mfuko wangu na nikalitanua siku iliyofuatia kuelekea Uarabuni kama sehemu moja ya kikosi cha dharura cha nambari 6,cha wana Anga. Nilikisoma kitabu hiki njiani nikisafiri na nikarudia tena na tena hata nilipofika huko. Baada ya muda mfupi wa kwanzia, mwishowe niligundua labda shida yangu inatokana na uchungu niliokuwa nao kwa watu wengine; nilithibitika kukaukiwa kwangu na ngozi kulisababishwa na uchungu niliokuwa nao. Nilijitoa uchungu kabisa (na kwa kukaukiwa kwa ngozi) na tangu wakati huo nimekuwa nikingangana niwezavyo kusahau maovu yaliyopita na katika hali zote uchungu na hasira kuniondokea. Ninafuraha kushuhudia kwamba niliporejea nyumbani baada ya siku 45 ngozi yangu ilikuwa imerudi kama kawaida kwa mara ya kwanza kwa miaka 25, na ingali hivyo kwa miezi nne sasa. Huwa ninalisoma jarida hili Uchungu kila wiki kuona kwamba niko huru kutoka kwa uchungu na niendelee kuishi duniani.

*Kuwa na siku njema na tena niasante*
*Baraka za Mungu kwako na huduma yako.*
Tony

## BARUA KUTOKA KWA TOLEO LA KWANZA

*Mpendwa Jim*,

Salamu za leo na nina barua fupi tu____ kama ushuhuda mwingine kuhusu kijitabu chako kidogo juu ya uchungu na msamaha. Kijitabu hiki kilinifikia pasipokutarajia kupitia posta siku chache kabla sijaenda Quantico kwa wakati wa kazi ya juhudi. Nilikitupa kwa kijisanduku changu huku nikipanga vitu vyangu, nikifikiria nitakisoma njiani. Baadaye nilikisoma, nikatambua umuhimu wake.

Baada ya darasa la mchana kule Quanctico, afisa alinijia akitaka nimushauri. Huyu afisa mkuu alikuwa mwana sheria katika Pentagon. Alikuwa anataka ajue kama atatoa mashtaka ya halali kupambana na Amiri Mkuu aliyekuwa amemuajiri. Siku ya kufuatia alinipa hati kamili yenye kurasa 20 zilizopangiwa na kuorodheshwa maovu yote aliyomwekea mtu huyu miezi sita iliyopita. Hakuna lolote lililoonekana la maana kwangu, lakini sanasana yalilenga juu ya afya yake. Kabla hatujaongea nikamuuliza asome kile nitampatia. Kwa hivyo alipata kusoma kitabu chako juu ya jinsi ya kuwa huru kutoka kwa uchungu. Kilimwelekeza moja kwa moja kwenye lengo; ingaweje alikuwa amelelewa kwa kanisa, kilimfunulia yote kwa njia ya maono. Baadaye, kwa kushughulikia mambo ya bosi wake (na maovu mengine mabaya tokea hapo nyuma) nilipata fursa ya kumushirikisha katika injili ya kumubadili maisha yake. Katika hali hiyo ya mazungumzo nilimuuliza kama anajua kile kingetokea, ikiwa angekufa siku hiyo n.k. Hili ndilo nilifahamulo. Akasema, "Baada ya kukisoma kitabu hicho juu ya Uchungu, sijui kile kingelinifanyikia mimi." Ilikuwa dhihirisho kwangu ya kuwa ujumbe wako kwake ulikuwa mahubiri ya sheria,na ulionyesha hitaji la yeye kumuendea Kristo. Ninafurahia jinsi Mungu aliutumia ujumbe huo na uendelee kumuombea ili Mungu amusimamishe katika imani…..

Ningali ninahitaji urafiki na uongozi wako katika Kristo Yesu

*Mwaminifu,*
Steve

Jumamosi usiku nilikuwa na usemi nyumbani mwa rafiki yangu wa zamani. Kwa sababu nilikuwa ninaenda Dallas, niliwaandikia watu kadhaa nyaraka ndogo ambao niliwajua wakati mmoja kutoka sehemu mbalimbali nchini, na walijitokeza kwa wingi mle nyumbani.

Mwenyeji wangu akanisihi niongelee kuhusu uchungu, na nikafanya hivyo. Baadaye wachumba wawili wakaja kuniona. Nilikuwa nimewajua hapo awali kwa muda wa miaka minane kule Pullman, Washington. Mke wake akanijia nakuniambia, "Tumeoana kwa muda wa miaka minane. Mwaka wa kwanza wa ndoa yangu nilimwonea mama yangu uchungu mwingi sana ambao niliugeuzia mume wangu kila siku. Mwaka wetu wa kwanza ulikuwa wa kuudhi sana kwa sababu uchungu niliokuwa nao nilishinda nikiwashirikisha mama yangu na pia mume wangu."

Pale pale akaniambia ya kwamba nilikuwa nimeongelea kuhusu uchungu miaka saba iliopita na kwamba amejiondolea wake uchungu. Siku moja akamuona mama mmoja ambaye alikuwa mchungu sana kwa mamaye. "ninaweza kumsaidia mama huyo. Ninaweza kumshirikisha katika ujasiri wa kawaida. Nikamwendea nimushirikishe na sikuweza kukumbuka lolote la maarifa ningemshauri. Kumbukumbu yangu ya maarifa ilikuwa imetoweka. Kile niliweza kumshawishi ni kwamba hata mimi nilikuwa mwenye kumbukumbu mbaya na sasa siyakumbuki kamwe."Kwa kweli "Bwana" aliweza kumuondolea uchungu wake.

Wakati mmoja nilikuwa na fundisho la kosi ya wiki nne kuhusu ndoa. Nilieneza habari hii kupitia kwa vijikaratasi na sikuweza kujua ni akina nani watakao kuja. Akaja mama mmoja ambaye alikuwa ametumwa na daktari arudi darasani kwa mafundisho. Alipata kuingia ndani na kwa hakika naweza kusema kwamba sijawahi kuona mtu yeyote maishani mwangu akiwa na uchungu mwingi" kwa sura. Alikuwa na uchungu wa miaka arobaini, kila moja juu ya nyingine. Usiku huo mama huyu aliweza kujiondolea uchungu wake wote na akanialika kuniona siku ifuatayo mahali pangu pa kazi katika zana ya vitabu. Alikuja kwenye zana, na sikuweza kumtambua yeye ni nani. *Alionekana kuwa tofauti sana*. Nilikuwa nimemwona tu usiku uliopita, lakini sasa alikuwa amebadilika ndani na kuwa msafi.

Kuna shida gani? Kwa nini hatuwezi kuondoa uchungu? Ikiwa nitasema uongo, ninaweza kukiri kosa langu na nisamehewe. Ili niweze kuondoa inanibidi kuirudisha tena moyoni mwangu. Tunahitajika kurudisha ufahamu wa uchungu mioni mwetu. Badala yake, huwa tunajaribiwa kumwangalia mkosaji. *Ona ambacho yeye alifanya*. Hiyo ni asili ya uchungu. Ili kuondoa, mbali, kunanihitaji kutambua ya kwamba kosa ni langu kabla ya kulikiri na kuachana nalo.

Lakini wewe wasema, "Mimi sio mchungu, huwa nakasirika haraka." Lakini dalili za kukasirishwa zimekaribiana sana na dalili za chuki. Je unaelewa maana ya kuchukizwa kwa ghafla? Waweza kusema "Sio uchungu—ni nia tu ya

kuudhiwa" Lakini kuna uhusiano wa karibu sana kati ya kukasirishwa na kuchukia. Mtu anaweza kukasirishwa na tena achukizwe. Kuna tena uhusiano mwingine wa karibu sana kati ya chuki na uchungu. Chuki huwa inageuka kuwa uchungu mwingi sana.

Uchungu ni kama chuki iliyokunasa,imegeuka kuwa kali na baya sana. Inafichwa ndani na inazidi kuwa baya na baya zaidi. Na mambo haya huzidi kufululiza nyingine juu ya nyingine. Kuna uhusiano kati ya uchungu na chuki, na kuna dhibitisho kamili katika Bibilia kati ya chuki na uuaji. Kile ninajaribu kumaanisha hapa ni kwamba kukasirishwa kwaweza kusababisha uuwaji. Wengine waweza kataa fundisho hili wakisingizia ya kwamba ni zito sana. Lakini nguvu zake zatoka kwa Bibilia.

Ambacho tunataka kufanya ni kuweka dhahiri *jinsi dhambi ya uchungu ilivyo*. Mtu mchungu ni lazima kwanza ajitambue ya kwamba yeye ni mchungu, la pili, ni dhambi mbaya sana. Na tena, kinacho sababisha watu kutojiepusha na dhambi hii ni kwamba wanadhania dhambi hii ni ya watu wengine. Shetani husema, "Sawa, anapokwepa kudanganya, au anapokwepa kufanya hili au lile, au asemapo pole, basi utasikia vizuri."

Basi iwapo hatawezi? Iwapo hataepuka? Je utaendelea kuwa mchungu maishani mwako mwote kwa sababu mtu mwingine anakushawishi kuishi kwa dhambi? Jambo hili halileti ubusara wowote kabisa. Waweza kusema, "Nitamsamehe wakati ataniambia pole, na ahadi atakapo fanya hivyo. Niko na haki juu ya uchungu hadi atakaponiomba msamaha, hapo nitamsameha na mambo yote yatakuwa mazuri. Unazidi kuweka ukuta huu wa uchungu na wakati mmoja anakujia na kukuambia, "Nakuomba msamaha." Waweza kumsamehe sasa hivi? La hasha, kwa sababu uchungu hausamehi. Ili kumsamehe mtu huyu anapoomba msamaha unastahili uwe tayari kumsamehe hata kabla hajakuomba msamaha. Na ikiwa utakuwa tayari kumsamehe kabla hajakuomba msamaha, basi haijalishi iwapo ataomba msamaha au hapana. Kwa msemo mwingine ni kujiondolea uchungu binafsi. Haijalishi mwenzio anafanya nini.

Hapo awali kusudi lilikuwa uchungu ni kama shina litokalo kwa dhambi ya mtu mwingine-iwe ya kweli au kudhaniwa. Huonekana tu kwa njia hiyo. Kwa hakika uchungu ni dhambi isimamayo peke yake. Mtu mchungu huamua kuwa mchungu binafsi kando na mkosaji.

Lakini wewe husema, "La hasha, alinitenda dhambi, na asemapo pole, kila kitu huwa sawa." Lakini hivo si kweli.

Ninaelewa hali kama hii ambapo mkosaji aliomba msamaha na mwenziwe alikuwa angali na uchungu. Tuchukulie ya kwamba mkosaji amekufa na hawezi kuomba msamaha. Ninaelewa watu ambao wana uchungu mwingi kwa wazazi wao na ilihali walikufa miaka iliyopita. Lakini ule uchungu haujakufa. Uchungu ni dhambi ya mtu binafsi, bila kuhusisha mtu mwingine.

Wakati mmoja nilienda gereza la kifalme Walla Walla ili

## BARUA KUTOKA KWA TOLEO LA KWANZA

*Mpendwa Jim,*

Sidhani kama tumewahi kukutana uso kwa uso, lakini napenda kuzisoma arafa zako na nimesikia sifa zako kwa miaka mingi. Mimi nina cheo cha '74 USNA. Nilikisoma kitabu chako juu ya Uchungu miaka michache iliyopita na ningependa kukutolea ushuhuda mfupi. Nimekuwa katika huduma ya kikristo kwa miaka 22 kama mfanya kazi wa merikebu. Nilidanganyika ya kwamba ukiwa kiongozi au uongozini, unakuwa wa maana sana na nilipokosa "kupanda cheo" niliona uchungu sana. Uchungu huu uliniingia na ukakolea ndani na ukawa "shina" la kuzama katika maovu mengine mengi na mabaya yaliyonifanya nijihisi nina "haki" ya kuwa mchungu. Lakusikitisha ni kwamba uchungu wangu ulionekana na wote waliokuwa karibu nami ilhali sikujitambua. Kulingana na zaburi ni sawa, "Moyo wangu ulipoona uchungu, viuno vyangu viliponichoma, nalikuwa kama mjinga, sijui neno……….." Zaburi 73:21-22. Baada ya kusoma jarida lako ndipo nilipopatakuona kwa mara ya kwanza uchungu kuwa na tena wenyewe ni 'dhambi'. Niliomba Mungu anionyeshe kila shina la uchungu lililokuwa ndani mwangu. Muda sio mrefu niliweza kugundua na kuorodhesha mashina 16 tofauti za uchungu. Ulinichukua muda kutubu kila moja, moja baada ya nyingine nikimwomba Mungu msamaha. Nikamwita msimamizi wangu na kukiri kwake yote 16 na nikamuomba msamaha. Kwa nehema ya Mungu aliweza kunisamehe na kuniweka huru. Ni heri niilinde nafsi yangu, kwa maana imedhihirisha kuwa makao na shamba lenye rotuba kwa mbegu za uchungu. Ni lazima niwe mwangalifu kuyalinda mawazo yangu ili kuzuia shina lolote kati ya hizo 16 kutorudia tena kwangu.

Asante sana kwa kijitabu chako na mafundisho yako. Kinahitajika sana katika mwili wa Kristo.

*Katika Kristo,*
Bob

nikae na wafungwa huko kwa siku moja. Krismasi ilikuwa imekaribia. Nilikaa huko karibu masaa sita. Kufikia masaa ya alasiri, nilikuwa chini ya ulinzi mkali, na kuzungumzia kuhusu uinjilisti. Mmoja wao akaniuliza ni wafikie wahalifu sugu. Nilidhani alikuwa amevutiwa sana na kazi ya uinjilisti na nikazidi kuwaongelesha kuhusu jambo hili. Nikawa tena katika ulinzi kadiri kwa muda mchache, katika chumba cha ulinzi na sehemu zengine.

Ilipofika jioni niliwekwa tena katika ulinzi mkali, na nikafikiria kuzungumzia fundisho hili la uchungu. Niliweza kuona labda kuna watu fulani wachungu mahali pale.

Yule mtu aliyeniuliza kuhusu wiinjilisti alasiri iliyopita akaniuliza tena swali lingine. Alisema hivi, "Jinsi gani waweza kuondoa uchungu kwa mtu aliyempiga mwanao wa umri wa miaka mitatu bila huruma?" Kwa hivyo nilipata kumuelezea ni jinsi gain, na nikamwambia, "Unajua, unapoondoa uchungu wako unaweza kumsaidia mtu huyu asidhubutu tena kupiga watoto wengine wadogo."

Akasema, Hapana, mtu huyu hawezi kusaidika."

Nikamwambia, "Ni kweli anaweza kusaidika."

"Hapana, hapana." akakataa.

"Kwa nini hapana?" nikauliza.

"Hayuko nasi tena." akajibu.

Alikuwa ameuwawa na mfungua huyu. Alimuua kwa sababu ya kitendo cha unyama alichomtendea mwanawe wa kiume wa miaka mitatu—na hii ndiyo sababu alikuwa gerezani. Lakini hata kama alikuwa amemua, **angali alikuwa mchungu**. Kuelezea kwake,kwa maneno mengine, hakuweza kumuondolea uchungu. Ila kifo alichosababisha hakikuweza kumuondolea uchungu ule. Wakati mtu mwingine anaposema pole, huwa hauondoi uchungu wetu. Kukiri mbele za mungu ndilo jambo la pekee ambalo linaweza kuondoa uchungu ule kwa sababu ya kifo na kufufuka kwa Yesu Kristo. **Hili ndilo suluhisho la pekee**.

Unaweza kusema unayemwonea uchungu alikufa miaka mingi iliyopita. Haukumuua mtu huyu kama yule mfungwa. Haswa hamna utofauti; mtu huyo mwengine alikufa na wewe ungali mchungu.

Ikiwa aliyekufa alikuwa muumini, yuko pamoja na Bwana, amesamehewa na ni msafi kama theluji. Wewe ungali mchungu kwa mtu atakayefurahia kule mbinguni kwa sababu jina lake limeandikwa katika kitabu cha mwanakondoo cha uhai.

Ikiwa aliyekufa hakuwa muumini, basi yuko chini ya hukumu ya Mungu kama inavyonenwa katika (2 Wathosolonike 1:6-8).

> *Mungu ana haki : Aliwapa mateso kwa wale wawatesaoninyi, na kuwapumzisha ninyi mteswao na pia kwetu sisi. Haya yatafanyka wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni kwa mwali wa moto pamoja na malaika wa uwezo wake. Atawaliiza kisasi wale wasio mjua Mungu na hawatii Bwana wetu kristo.*
>
> *Rafiki zangu msilipize kisasi bali moeane nafasi kwa gadhabu ya Mungu, kwa maana imeandiwa, "Ni ju yangu mimi kuoeana kisasi, nitalipisha,"asema Bwana.(Warumi 12:19)*

Mungu ana haki na yeye ndiye alipishae.

Hata kama hawa watu wangekuwa wangali hai hawangelitunza uchungu **wako** wala wewe kuwatafuta. Licha ya hao kufa tayari wametunzwa kwa njia nyingine. Na jambo hili hukuacha ukiwa hai na mwenye uchungu, ukijiumiza mwenyewe na hata wale wanaokuzingira kwa miaka mingi. Uchungu wako ndio dhambi yako wewe bila kufikiria ni nini kilichoisababisha. Mungu atakuruhusu kuona msamaha na furaha yako wakati unapotubu na kukiri uchungu ulionao kama dhambi kubwa ishindanayo na Mungu.

Sio lazima tuweke uchungu na sio lazima tushirikishe wengine. Kuna jambo moja tu la kufanya na lenyewe ni kukiri uchungu kama dhambi kubwa na baya sana. Ni lazima tuendelee katika maungamo kama kanuni.

Wakati mmoja nilikuwa nikizungumza kule Monterey, California katika chuo cha Manawari cha U.S, Naval, Shule ya Post Graduate. Kulikuwa na mtu mmoja aliyekuwa na sifa kubwa kama mwalimu wa bibilia. Alikuwa afisa wa safu ya wanamaji, lakini alirukishwa kuwa amri mkuu katika Manowari ya kuzama. Yeye hakuwa amefuzu katika cheo hiki na alisikia uchungu sana. Nikamzungumzia kuhusu maungamo ya dhambi na uchungu, na shida yake ikapata kuondoka kabisa. Alikuja akanitembelea na akaondoa uchungu wake kabisa. Asubuhi iliyofata, Mke wake aliniambia, "Nimepata mume mwingine mpya" Amekuwa mchungu kwa wana-

maji wenzake, lakini ilikuwa dhambi yake sio wanamaji wenzake.

Army Carmichael ana kijibarua katika kijitabu chake kidogo '*ikiwa*' "Kikombe kilichofanyika maji matamu hayawezi kumwagika hata tone moja la maji machungu, ilihali kimetikiswa kwa ghafla" Na ikiwa kitatikiswa kama kimejaa maji matamu, ni nini kitakachotoka katika kikombe hicho? Ni maji matamu pekee. Na ikiwa utatikisa kwa nguvu zaidi, kutatendeka nini?. Ni maji matamu zaidi. Na ikiwa mtu fulani atajazwa kwa maji matamu na mwengine amtikise, ni nini kitakachotokea? Ni maji matamu. Mitikiso haiwezi kugeuza maji matamu kuwa machungu. Huwa yanageuzwa na kitu kingine.

Mitikiso humwaga tu kile ambacho tayari kimetiwa ndani ya mtungi. Ikiwa utajazwa utamu na nuru na upate kutikiswa, unaenda kumwagika nuru na utamu. Na ikiwa utajazwa asali utatokwa na asali. Ikiwa pombe ndio itatoka itadhibitisha nini? Tayari inaonyesha kile ambacho kiko mtungini. Kwa maneno mengine uchungu hautokani kamwe na kile mtu mwengine ametenda, ni yale matokeo ya kitendo tumekifanya na jinsi tulivyo.

Miaka mingi iliyopita nilikuwa nikifanya kazi kwa dawati langu katika chumba chetu cha kulala. Mke wangu Bessie, alikuwa akisomea kitandani. Kile nilikuwa nikifanya hakikuwa kinafanyika vyema. Bessie akaniambia jambo na nikageuka nimsikize. Halikuwa jambo la kikiristo. Aliniangalia kwa mshangao na akaamka na kutoka nje ya chumba cha malazi. Nikabaki pale nikifikiria " Angelisema jambo hilo. Tazama alivyosema, aliniambia, "Ona, Ona, Ona" Nilifanya hivyo kwa dakika kumi na labda hata zaidi. Nilimwonea Bessie uchungu sana, lakini lolote alilofanya lilikuwa kombe lililotikiswa. Kilichokuwamo ndani ya kombe hilo kilipata kutoka.

Na kama ningelijawa na furaha na nuru, haingeleta utofauti wowote. Nilikaa pale na kuwazia aliyonitendea. Nilielewa vyema kwa sababu nilikuwa tayari nimejifunza kweli kuhusu uchungu. Nilikuwa ningali nawazia "dhambi" yake kwa sababu kulikuemo na utani wa kulaumu yule mwingine. Watu wengine hufanya hivi kwa muda wa miaka mingi.

Nilikaa pale kwa muda mfupi na nikaamka nakuenda upande ule mwingine wa kitanda, nikapiga magoti yangu na kusema "Bwana ni mimi pekee niliyekuwa na makosa. Ilikuwa ni uchungu wangu, na dhambi zangu. Ninayakiri na kuyaacha na tafadhali nisamehe"

Nikasimama kwa miguu yangu na kusema, "lakini tazama alichosema" . Nikarudi tena kupiga magoti yangu.

"Mungu pole sana kwa yale nimeyatenda. Ninakubali lawama. Ilikuwa dhambi yangu na yangu pekee"

Nikainuka kwa miguu yangu na kusema "Mungu mimi na wewe ndio tunajua kweli ni nani mkosaji" Nikapiga magoti tena na kuendelea hivyo kwa muda wa dakika 45 hadi niliposimama na kutosema "tazama alichosema"

Na sasa siwezi kukumbuka yale aliyoyasema, na siwezi kukumbuka yale niliyoyafanya pale chini ya dawati. Siwezi kukumbuka hayo yote . Kile ninachokikumbuka sasa hivi ni inuka juu. Bali pia ninafahamu kama singelijihadhari na uchungu wangu **ningelikumbuka sawasawa aliyoyasema hata wa leo** hii. Na hivyo ndivyo ilivyo asili ya uchungu.

Ili niweze kuuondoa, nastahili niyaone kuwa ni maovu, na ni dhambi yangu na yangu pekee. Siwezi kuuondoa kwa yule mtu mwengine kusema pole. Siwezi kuuondoa iwapo mtu huyo mwingine atakwepa au kufa. Siwezi kuuondoa kwa njia nyingine ile isipokuwa kuuita uovu dhidi ya Mungu aliye mtakatifu, ni kukiri na kupokea msamaha.

Shida ni kwamba siwezi kuzuia macho yangu kutazama dhambi ya yule mtu mwingine. Lakini ni lile lengo la kudhania kwamba shida yake ndio ionyeshayo hasa si dhambi. Ingelikuwa shida ni yake, na ningelijaa furaha na nuru, bila uchungu, basi ningemsikitikia yule mtu mwingine.

Ningelisema hivi "Tazama mtu huyu maskini alichokitenda. Ningelitenda kitu kama hicho, ningelihisi nimetenda maovu. Anastahili ajihisi kweli ametenda maovu. Nimeghairi nitaenda nimsaidie." Basi kama hilo silo jukumu langu, basi mimi ni mchungu na ni dhambi yangu sio yake.

Ninaamini dhambi hii ni kizuizi kikubwa katika ufufuo wa kiroho nchini humu. Wakristo waanzapo kukiri dhambi zao, hawawezi kuwasamehe wengine maovu yao.

**MWONGOZO WA SOMO: Jinsi ya Kuwa Huru Kutokana kwa Uchungu.**

*Uchungu wote na ghadhabu na hasira na kelele na matukano yaondoke kwenu, pamoja na kila namna ya ubaya, tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika kristo alivyowasamehe ninyi.Mkaenenda katika upendo, kama kristo naye alivyowapenda ninyi, tena akajitoa kwa ajili yetu, sadaka na dhahabu kwa mungu, kuwa harufu ya manukato.(Waefeso 4:31-5:2)*

**Maswali ya Kujadiliana**

1. Uchungu ni nini?
2. Je, uchungu ni dhambi? Kwa nini au mbona sio?
3. Hebu taja hali moja katika maisha yako ambayo ilisababisha uhisi uchungu.
4. Ni nini chanzo cha uchungu? Je, inategemea kiwango cha kosa?

*Tabia ya uchungu ni kwamba hukumbusha yale yote yaliyopita. Kulingana na hali maelfu elfu na mazungumzo ambayo yamekuwa yakiendelea katika maisha yetu, hili lingali lipya katika maisha yetu. Tunakumbuka kila kitu kikijumulisha mambo yaliyo tumiwa, matamshi na mabadiliko ya sauti. Haya ni kwa sababu ya kuwaza, kuwazua na kuwaza zaidi.*

5. Suluhisho la dunia kuondoa uchungu ni lipi?
   a.
   b.

*Hatua ya kwanza ya kuondoa uchungu wetu ni kufahamu tuna uchungu. Kisababu am bacho hufanya watu wasishughulikie uchungu wao ni kwamba, huwa wanadhania hiyo ni dhambi ya yule mtu mwingine.*

6. Mungu anatutaka sis tufanye nini na uchungu wetu wote? (Yakobo 3:14,15)

*Ni vigumu sana kuwa mwenye huruma, mwenye pendo, na kuwa mchungu kwa wakati mmoja.*

**Hatua ya Kufuatia; Kuitikia Neno la Mungu.**

*Angazia* moja kwa moja hali ambayo unang’ang’ana nayo katika uchungu. Kama hau-jausalimisha kwa Baba, fanya hivyo kwa haraka, ukikubali kujazwa na neema ya Bwana Yesu Kristo. *Uliza* hatua za kukufaa uweze kuzifuata, ukisaidiwa na roho mtakatifu, ili kuondoa moyo mgumu. Rudisha kwa pendo kwa kufuata sheria ya Kristo ya msamaha. *Tena iweni wafadhili nyinyi kwa nyinyi, wenye huruma, mkasameheane kama Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi( Waefeso 4:32)*

## KUSAMEHE WENGINE

Jim Wilson

*Na hivi ndivyo baba yangu wa mbinguni atakavyowatenda ninyi, msiposamehe kwa mioyo yenu kila mtu ndugu yake.(Mathayo 18:35)*

Hapa Bwana yesu kristo anaongea, na kuwapa wafuasi wake mafudisho kuhusu msamaha. Wengi wetu wamepata maarifa, mtu atujiapo sisi na kuomba msamaha. Na wakati mwingine tunapoenda kuomba msamaha.

Kumekua na majibu kadhaa ya kawaida kwa maswali kama haya, walakini jibu ungelisikia kila mara ni, "Hakuna lolote la kusamehe." Na hili jibu hutamukika kuwa lenye rehema nyingi, bali si hivyo. Hiyo ni mojawapo ya njia ya kutaka kusamehe.

Mtu mliyemwomba awasamehe ninyi anajua vyema na kwa ukamilifu kwamba mnahitaji msamaha. Lakini ninyi mwazidi tu kukwepa hitaji hili kwa kusema, "Oh, hakuna lolote la kusema hapa." Waweza kudhania kwa hakika hamna shida yeyote, bali kwa kawaida lililoko hapa sio lengo hasa.

Wakati mwingine hao husema, "Haidhuru umesamehewa." Husema hivyo kwa sababu lazima waseme, lakini haimaanishi walisemalolimo moyoni mwao. Bali fundisho hili linahitaji msamaha, utokao moyoni. Kwa maneno mengine, Mungu anajua ni nani asiyetoa msamaha wa kweli. Pia tunaambiwa tusipotoa msamaha utokao moyoni kwa ndugu zetu, Mungu atatutenda kila mmoja wetu vivyo hivyo kwa njia nyingine. Mungu hatuhitaji sisi kutumia maneno kamili, hata ingawaje waweza kuaminisha mtu huyo mbele yako, hauwezi kumsadikisha yeye yule, atafutaye moyo wa mtu. Mungu anaelewa vyema unapomsamehe nduguyo toka ndani ya moyo.

Tunapotenda dhambi kwa njia hii hatuwezi kujificha mbali na Mungu. Mioyo yetu ni wazi na dhahiri kwake. Kwa hivyo anajua tunapokataa kusamehe. Anajua dhambi zetu na hakika anajua mahitaji ya neno lake kuhusu msamaha,

Je! Biblia inatuelimishaje kuhusu Baba wetu wa mbiguni atakavyotutendea?

*Kisha Petro akamwendea Yesu na kumwuliza, "Bwana, ndugu yangu anikose mara ngapi nami nimsamehe? Hata mara saba?" (mth 18:21)*

Petro alidhani anauliza swali njema.

*Yesu akamjibu, "sikuambii hatamara saba, bali hata saba mara sabini." (mth 18:22).*

Yesu aliposema haya wadhani alimaanisha kufikisha kiwango cha sabini mara saba? Je, tunaruhusiwa kuweka orodha ya hesabu ya makosa?

Wakati wowote mtu anapohesabu na kusongesha muda wa kutoa msamaha; basi hapo hakuna msamaha wa kweli. Na ikiwa ulimsamehe ndugu yako kutoka ndani ya moyo kila alipokutendea dhambi, ingeonekana kama ni mara yake ya kwanza kukosea kila alipofanya hivyo. Watu hutumia vibaya Yesu anapofundisha ya kwamba geuza shavu la pili unapopigwa lile la kwanza. Hao husema, "Ndiyo, nitamwachilia anipige upande ule mwingine wa shavu walakini ikiwa ataniongeza la tatu, nitainuka na yeye."

Lakini yesu alipofundisha kuhusu kugeuza shavu la pili, alikuwa anatuambia tutende hivyo kutoka ndani ya moyo. Kwa kufanya hivyo, Yesu huchukulia kwamba mtu yule mwingine ndiye amekutenda dhambi. Huchukulia kwamba amekutenda maovu mabaya mara saba, Sabini na saba au mara mia nne, tisini. Lakini ikiwa utahesabu misamaha ambayo umetoa, basi wewe hujasamehe bado.

*Kwa sababu hii ufalme wa mbinguni umefananishwa na mfalme mmoja aliyetaka kufanya hesabu na watumwa wake. Alipoanza kufanya aliletewa mtu mmoja mwenye talanta kumi. Naye alipokosa cha kulipa bwana wake akamuru auzwe, yeye na mkewe na watoto wake, na vitu vyote alivyo navyo vikalipie lile deni.*

*Basi yule mtumwa akaanguka, akamsujudia akisema," bwana, nivumilie, nami nitakulipa yote pia." Bwana wa mtumwa yule akamhurumia, akamfungua, akamsamehe lile deni.*

*Mtumwa yule akatoka, akamwona mmoja wa wajoli wake, aliyemwia dinari mia. Akamkamata na akaanza kumushika koo.*
*Akamdai kwa uchungu, "nilipe uwiwacho" basi mjoli wake akaanguka miguuni mwake akamsihi akisema, "nivumilie nami nitakulipa yote pia" lakini hakutaka, akamchukua akaenda akamtupa kifungoni hadi atakapoilipa lile deni. Basi wajoli wake walipoona yaliyomtendekea, walisikitika sana, wakaenda wakamweleza bwana wao yote yaliyotendeka.*

*Ndipo bwana wake akamwita akmwambia, "Ewe mtumwa mwovu, nilikusamehea wewe lile deni lote uliponisihi nifanye hivyo. Je haikukupasa nawe kumrehemu mjoli wako jinsi nilivyokurehemu wewe? Bwana wake akaghadhabika, akampeleka kwa watesaji, hata atakapolipa lile deni lote,*

*Ndivyo na baba wangu wa mbinguni ata-*

*kavyowatendea ninyi, msiposamehe kwa mioyo yenu kila mtu ndugu yake. (mth 18:23-35)*

Tulilpobadili kutoka mautini hadi uzimani, ilipasa kurehemiwa, na deni lile lililoondolewa na lililokuwa kubwa sana. Wakati tulifanyika kuwa wakristo, hapo ndipo tulipokea msamaha halisi na wa kipekee. Ulikuwa baraka kwetu na tuliupokea bila kuambatanishwa na kikwazo chochote. Na sasa kuna utofauti kati ya msamaha wa sharti na msamaha halisi.

Tulilpozaliwa mara ya pili tilipokea msamaha halisi. Ulikuwa msamaha mkuu ajabu kama ule msamaha wa deni kubwa upatikanao katika fumbo tililojifunza katika kitabu cha wakolosai 3:13, lina tuambia:

> *"Mchukuliane nyinyi kwa nyinyi na kusameheana wote ambalo litakuwa kijisababu cha kulaumiana kati ya mtu na mwenziwe. Kama vile bwana alivyowasamehe ninyi, vivyo na ninyi. "*

Je! Bwana alitusamehe kinamna gani? Tunaambiwa tusamehe pasipo la ziada *jinsi tulivyosamehewa*. Inatupasa kusamehe kikamilifu na kabisa. Lakini punde inapofika kwa wadeni wetu, tunakuwa na huu msamaha wa kikwazo. Kumbuka jinsi baba wetu wa mbinguni alivyokaribisha wale waliokuwa na tabia kama za yule mtumwa mwovu apatikanaye katika lile fumbo.

*"Utusamehe deni zetu kama sisi tuwasameheavyo wadeni wetu. (mth 6:12)*

Bwana alituamuru sisi kuomba hivyo. Lakini sisi hupingana,(Mungu! sitaki,sitaki kusamehewa kwa njia ya namna hiyo. Ikiwa nitasamehewa jinsi niwasameheavyo wengine, niko kwa taabu kubwa.)

Mkristo aombaye jinsi alivyoamuriwa, huwa anaomba kwa msamaha wa sharti. Kulingana na mstari wa kumi na nne, baada ya sala ya bwana, yesu anasema, "ikiwa utawasamehe watu wakati wakutendapo dhambi, baba yenu aliye mbinguni atawasamehe nanyi pia. Lakini msipowasahehe watu dhambi zao, baba yenu hatawasamehe ninyi dhambi zenu." Mambo haya ni kweli na ni Yesu aliyeyasema.

Mtu anaweza kukata shauri na kusema, "yawezekanaje kuwa hivi? Tumeupokea msamaha halisi, na sasa Yesu anasema hivi, ikiwa nitawasamehe watu wanaponitenda dhambi, baba yangu aliye mbinguni atanisamnehe pia nami. Lakini nisipowasamehe watu dhambi zao, baba yangu hatanisamehe dhambi zangu. Haya nayasikia kwangu kama ni msamaha wa sharti.

Na ndipo kwa sababu hapa kuna sharti. Alisema tulipotoka mautini hadi uzimani tulisamehewa deni kubwa sana. Basi tukapewa maagizo kamili kusamehe kama tulivyosamehewa. Tulisamehewa bila sharti na pia tunaambiwa tusamehe bila sharti.

Mtu asameheaye bila sharti, hana kosa lolote akiomba hivi, "Bwana nisamehe jinsi nisameheavyo" bila shaka msamaha huu ni halisi.*Hakuna kutofautiana kwa mkristo atendaye maagizo aliyopewa.*

Utofauti waweza kuonekana tu wakati msamaha hauwezi kuwasilishwa kama vile ulivyopokelewa. Shida hii ndiyo ya mtumwa asiyesamehe. Alisamehewa na badala yake akageuka na kutosamehe jinsi alivyosamehewa.

Fundisho hili ni la nguvu sana., "Hivi ndivyo baba yangu aliye mbinguni atakavyokutenda wewe usipomsamehe ndugu yako kutoka ndani ya moyo wako, jinsi nilivyokusamehe kutoka moyoni mwangu. "Kama sitasamehe, bila shaka ni kijisababu kamili katika wokovu wangu.

*Na ndugu yako akikukosea, enda ukamwonye, wewe na yeye peke yenu; akikusikia umempata nduguyo. La, kama hasikii chukua pamoja nawe tena mtu mmoja au wawili ili kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu, kila neno lithibitike. Na asipolisikiza hao, liambie kanisa; na asiposilisikiza kanisa pia, na awe kwako kama mtu wa mataifa na mtoza ushuru. Amini nawambieni, yoyote mtakayo fungua duniani, yatakuwa yamefunguliwa mbinguni. Tena nawambieni ya kwamba, wawili wenu watakapokutana duniani katika jambo lolote watakaloliomba, watafanyiwa na baba yangu aliye mbinguni. Kwa kuwa walipo wawili au watatu wamesanyika kwa jina langu nami niko papohapo katikati ya wao. (mth 18:15-20)*

Maneno haya ya kwanza ya fumbo ambalo tumelitazama yanahusu pia msamaha wa moyoni. Ikiwa ndugu yako atakutendea maovu, enendeni na ukamwonyeshe makosa yake kati yenu nyinyi wawili. Kama atakusikiza, basi umekuwa mshindi juu ya nduguyo.

Wewe wasema, "Vema, hamuna uwezekano wa hili kutendeka. Nimeshajaribu hilo. Amenitenda maovu na nikawa wazimu kabisa, nikaenda na kumwonyesha makosa yake bali sikumshinda juu ya jambo hili kabisa." Sababu yake ni kwamba haukumwendea kwa msamaha wa ndani moyoni mwako. Fundisho hili halina ubusara sana kwa watu wengi kwa sababu hawaoni ni vipi unaweza kumwendea mtu kwa njia ya namna hii.

"Wawezaje kumwambia mtu makosa yake ambayo amekutenda wewe,na utarajie kumshinda? "Atajitetea."

Kwa nini ajitetee? Ni kwa sababu fulani anamlaumu. Bali mtu akimwendea kwa msamaha wa ndani ya moyo wake- basi suluhisho la mwisho la fundisho hili lote- matokeo yake hayatakuwa lawama.

Ninadhibitika mrudi wake **hatampata** ikiwa atamwendea kwa aina fulani ya uchungu, hasira, au roho ya lawama. Lazima mkosoaji asimwendee kwa haki kama hiyo. Tunaeza kumwendea pakiwepo na msamaha wa *mapema* ndani ya mioyo yetu. Msamaha huu hautategemea kutubu kwake. Nina uhakika hawezi kutubu ikiwa hatapokelewa kwa msamaha utokao moyoni. Ni lazima twende kwa msamaha na upendo. Ikiwa utasikiza, tutampata ndugu wetu.

Lakini asiposikiza licha ya kumwendea, tuchukue watu wengine wawili au watatu. Tuandamane pamoja watu walio na msamaha wa kutoka moyoni *mwao.* Kawaida huwa haifanyiki hivi.

Mtu anamwendea kwa lawama, mtarajiwa anajitetea na anakosa kumpata kabisa. Kwa hivyo watu wengine wawili kutoka upande ule mwingine ambao wanaelewa habari za mtarajiwa kushirikishwa ili wamuunge mkono yule mrudi.Bado hao hawajafaulu pia.

Lazima kila mmoja awe na msamaha utokao moyoni mwake ili mkosaji asije akakataa kutubu, bila shaka kosa ni *lake*. Ikiwa atakataa kusikia, basi lazima kanisa lipewe habari. Ni kweli, kuna umuhimu wa kanisa kuwa na msamaha kamili.

Kuna makanisa ambayo hudhani yanapeana urudi wa kanisa wa kiungu. Kwa vile wamekosa nia kamili ya msamaha, haiwezi kuwa ni kweli. Humwendea huyu jamaa na kumshurutisha hatimaye anaukataa. Wanashirikisha wengine wawili au watatu na wanamshurutisha, tena anaukataa. Basi kanisa linamfukuzia mbali, bali hakuna msamaha kutoka ndani ya moyo. Lakini mojawapo wa umuhimu wa urudi wa kanisa ni kumrejesha mkosaji.

Iwapo pia atakataa kusikiza kanisa, yamfaa kuchukuliwa kama mataifa au mtoza ushuru. Siamini Bwana Yesu alimaanisha kama walivyotendewa wamataifa na watoza ushuru. Nikiwazia ni jinsi mataifa na watoza ushuru wastahilivyo kutendea. Mbeleni katika Mathayo 5, Yesu anatuambia sisi tuwatendee sawasawa waliohaki na wasiohaki kama vile Baba atendavyo.

Anatwambia tuwapende adui zetu. Hata kama tumewachukua kama mataifa au watoza ushuru, bado itakuwa katika upendo. Hivi ni kumaanisha ya kwamba wamewekwa nje ya ushirika, bali kwa upendo na msamaha kutoka ndani ya moyo. Ni kusudi tu hao kutotaka msamaha wa kiungu ulioenezwa kutoka ndani ya moyo. Na ni kwa ajili ya fundisho hili Petro aliuliza swali ambalo lilituelekeza katika fumbo hili,"ni mara ngapi nimsamehe ndugu yangu?" upendo……… hauhesabu mbaya."(1wakor13:4,5) Upendo hauhesabu gharama.Baadhi yenu mumwahi patwa na jambo kama hili katika ndoa. Bwana au bibi anaweza kusema hivi, "kila mara unatenda hiki, na kile hautendi." Hivi ni kumaanisha nini? Kuna mtu anayehesabu mabaya. Biblia inatwambia tusidhubutu kutenda hili. Hesabu ya mabaya huwekwa mtu anapoendelea kuongeza makosa. Bali msamaha hautendi hili.

Je! Ni nini yesu alimaanisha aliposema ,"kile mtakachofunga hapa duniani na kule mbinguni…………..?" hivi ninazungumzia makanisa ya kikristo wenye wingi wa msamaha ambao wanatenda katika jina la Bwana Yesu Kristo.Wanatenda jinsi alivyowagiza kutenda. Basi wanapofanya uamuzi unaolingana na neno Lake, Naye huliheshimu.

Haliheshimu kanisa kwa sababu limebuni mbinu fulani ya kutatua matatizo. Bali ikiwa umetekelezwa kwa tabia na upendo wa Bwana Yesu Kristo, hata kule mbinguni mungu anauheshimu msamaha wa mwili wa walio amini kufanya uamuzi kumrudi mkosaji asiye tayari kukubali toba.

Wakristo wengi hutumia fungu hili la wawili au watatu kwa kila jambo *lisilo na maana.*Fungu hili linastahili liambatane na urudi wa kanisa na msamsha kwa ndugu. Nikweli kabisa kati ya hadithiya Yesu na swali la Petro kuhusu ni mara ngapi ingempasa kusamehe.Basi wawili au watatu wanapopatana kwa jina lake, Bwana Yesu kristo huwa jkati yao. Hili linahusika na uamuzi wa kusamehe wengine ambao wamekutenda maovu.

Unaweza Kuona uhusiano uliopo kati ya fundisho hili na uchungu. Uchungu hauna msamaha. Mara kwa mara ni usemi, Fulani alinitendea mabaya na siwezi kumsamehe. Ni kweli uchungu haujioni kuwa ni dhambi kibinafsi, bali huona dhambi ya wengine pekee.

Kwa hivyo katika wazo moja, msamaha ni mtu binafsi. Kwa fikira moja, Yesu Kristo ali-

tusamehe yote hata kabla hatujatubu.Hakuuteke-leza hadi tulipoupokea.Mungu hakua hasidi kule mbinguni hadi tuifikilie toba. Yeye hyuko pale kuishi akikaa na uchungu akingoja sisi tutubu. Yeye yu na msamaha ndani ya moyo wake hata kabla hatujakubali kusamehe. Upande wa Mungu kuna msamaha wa kipekee, na pia anatutaka sisi tuwe na msamha wa kipekee kwa yeyote yule ai-shiye kututenda ma- ovu. Huwa tunawawazia maovu ya mtu mwengine ametutenda **sisi**, au ali-tuambia **sisi**, ilahali hayo yote hayana lolote ku-husu yale mtu mtu mwengine aliyasema au ku-yatenda?

Na mkristo anapokuwa na msamaha utokao moyoni, huwa anamjali yule aliyemtenda maovu. Hajijali yeye mwenyewe.Lakini sisi ni kama Petero, " Hakika Bwana, nitasamehe mara saba lakini atakapozidi ya nane atakuwa taabani"

Bali msamaha wa kweli hauhesabu ma-boya. Kama una nia ya kuhesabu makosa iwe nje au ndani ya jamii, kuna uwezekano wa wewe ku-tosamehe. Yesu alisema kwamba babaye wa mbinguni atatutenda kila mmoja wetu pasipo msamaha tusamehe toka moyoni. *Umsamehe ndugu yako kutoka moyoni mwako.*

"Sina, msamaha moyoni mwangu kabisa" Basi ni nani anayehitaji msamaha?

Mwenye kuhitaji kusamehewa sio mwen-gine bali ni yule yule aliye na haya; asiye na up-endo, ana chuki, ana nia mbaya, ana kisasi, au lolote lile.Hawezi kuupata kwa njia zote mbili. Huwezi kuwa na kutosamehe ndani ya moyo wako na afurahie katika Bwana.

Kuna uwezekano uende kanisani na kuimba ilihali hauna msamaha moyoni mwako. Hayo yote ni bure! Kuimba kwako ni unafiki. Waweza kuimbisha watu walakini wanapokuwa wasafi hamuna haja wewe kuwafanya waimbe. Bali watuhawa watjiim- bisha kwa hiari, kwa moyo uliyojaa. Kwa nini? Kwa sababu wana usafi wa mioyo.

Kuna utofauti mkubwa sana kati ya kuimba kwa sababu ya furaha katika Bwana, na kule kuimba ili ujipe furaha. Wakristo wengine huenda kanisani kila Jumapili na kuimba ili wajipe furaha. Mara tu wanapomaliza kuimba, furaha yao huisha pia, kwa sababu mioyoni mwao hamna usafi. Sisi zote tungependa kujiwazia kuwa watu wazuri na yule mwengine ndiye mkosaji, labda si hivyo. Hebu jichukuliye kuwa wewe ndiwe haswa mwenye kosa la kutokuwa na msamaha.

Ikiwa mkristo ana msamaha moyoni mwake atakuwa na furaha bila kuwazia jinsi mwenziwe alivyo mkosaji, au jinsi mtu yule alivyomtenda maovu makubwa.

Lakini wawezaje kuonyesha msamaha kwa mtu wakati ambapo unahitajika kusimama imara kwa sababu haumwamini katika hali yao ya mai-sha? Sio vigumu vile. Ukiwa na msamaha moyoni mwako watautambua bila kujali msimamo wako ulivyo. Watautambua kutokana na sauti yako. Watu waweza kutambua unawapenda. Watatam-bua msimamo wako kwa maana wewe ni mchungu,na wanaweza kuutambua unapotenda hivyo kwa upendo. Kile ambacho unasatahili uwe na uhakika nacho ni lengo ulilonalo katika mazun-gumuzo. Usiwe na shaka na jinsi watakavyoku-chukuwa. Matokeo yake ni Bwana . Huenda ha-watakukubali lakini watatambua kuna utofauti.

Kwa muda, nimekuwa imara kwa watu. Wakati mmoja imepita miaka 35, Mtu mmoja amekuwa akienenda sawa na Bwana kufikia mwezi wa tatu uliopita. Alikuwa mkristo bandia katika mwaka huo wa kwanza katika wokovu, lakini mwaka uliofuata alienenda vikamilifu katika Bwana. Aliomba kuishi nasi nyumbani kwetu wakati huo wote wa kiangazi. Tulihamisha watotot wetu katika chumba kingine na kumpa yeye nafasi kukaa humo. Lakini alitangulia kuenda kwake kasha akarudi.Alihamia kwetu mwezi wa sita na vitu vyote. Nilikuwa naye mule chumbani mke wangu alipowapeleka watoto ku-lala ndipo nilimuuliza mambo yalivyo.Akajibu, "Sio vizuri sana".

"Shida ni kama ya wakati ule?"

"Ndio" Alijibu

"Msichana huyo moja?"

Akasema ni msichana huyo mmoja. Nika-muul;iza ikiwa anakumbuka jinsi Mungu alivyomsamehe kimmajabu mwezi wa tatu?

Akasema "ulikuwa muujiza; kulikuwa na furaha kuu na amani"

Nikasema "Vilevile Anaweza kufanya hivyo tena. Hebu tuombe hivi sasa.Unaweza kukiri, kutubu na urejeshwe tena"

Akasema "Hapana"

Nikasema "Sawa ,na ni kweli"

"Ehee, nimefahamu. Nimeshaona likifany-ika. Ninajua atatenda tena, lakini siko tayari hivi sasa"

Nikasema "Sawa sidhani umefahamu lolote.Wewe hauna hiari ndani mwako, wajua zaidi na unahitaji kurejeshwa hivi sasa."

"La hasha nitafanya hivyo wakati mwen-

Zaidi na unahitaji kurejeshwa hivi sasa." Akajibu.

"vizuri,nafikiri kulifahamisha kanisa kwamba unadumu katika dhambi"

"Utafahamisha kanisa ambacho numekwambia kwa siri?"

"Sikujua ni siri kwa lile ulikua unaenda kunioambia,pia unaenda kugeuka ombi la kutubu baada ya kuniambia.Mungu ananisihi na analisihi kanisa kwamba haustahili uwe katika ushirika. Hatuta shiriki nawe chakulani. Bibilia inatuambia ni nini la kufanya kwa yule ajiitaye ndugu ilihali ni mzinzi. Kanisa halionekani kuwa la kiungu, kwa hivyo kuna uwezekano nifukuzwe kwa ajili ya udaku.Atahivyo biblia inaniambia nijulishe kanisa.Pia nitawambia wasimamizi wa shirika la muungano wa kikristo na hawatasita kukupa jicho.Watakuondoa kwa haraka sana na sio jambo la kushangaza."Alikasirika sana.

Nikamwambia kwamba kulikuiwa bado na shida nyingine. "katika 1Wakorintho:5 inasema haistahili nile nawe. Haturuhusiwi kushirikiana na watu wajiitao waumini ilhali ni washerati.Ikiwa mtu yeyote anajiita ndugu na anaishi maisha kama hayo, hatutaweza hata kula naye.Na wewe unataka nigaidi hayo kwa sababu hautaki kutubu. Kwa sababu umekuja na mizigo yako yote nitakuruhusu ulale leo pekee, kisha asubuhi uondoke bila hata ya kuongea na mke wangu wala watoto." Alikasirika sana

"Ninakupenda sana na unajua unaweza kuishi hapa wakati huu wote wa kiangazi isipokuwa hautaweza kupata kufungua kinywa kila asubuhi kama hautakua katika ushirika" Nikasema.

Alijua nampenda na sina kinyongo naye.Alielewa upendo wangu ni kweli, lakini kama ningelirudia kuzungumuzia jambo moja hili na kwa aina ya uchungu wa hasira, ingekuwa mbaya sana.Alipata kugeukia Mungu tulipokuwa tukipata kifungua kinywa na akakaa kwetu kiangazi hicho chote.

Kwa hivyo meamaha si sawa na urudi wa kiunguNa kama urudi upo, haimanishi hakuna msamaha

Uwe na wakati wa Mungu pekee na nyumba yako iliyosafi.Kama kunsa yeyote haujampa msamaha basi msamehe toka ndani ya moyo.Mungu ni mwepesi tena wa haraka kukuypokea .Yeye ni mwepesi kusamehe.

Kwa hivyo msamaha si sawa na urudi wa kiungu. Na kama urudi upo, haimanishi hakuna msamaha.

Uwe na wakati na Mungu pekee na uisafi nyumba yako.Kama kuna yeyote haujampa msamaha, basi msamehe toka ndani ya moyo.Mungu ni haraka tena mwepesi kukupokea .Yeye ni mwepesi wa kusamehe.

**MWONGOZO WA SOMO: Kusamehe Wengine**

*Kisha Petero akamwendea akanwambia, "Bwana, ndugu yako anikose mara ngapi nami nimsamehe? Hata mara saba? Yesu akamwambia "Sikuambii hata mara saba, bali hata saba mara sabini." Mathayo 18:21-22.*

**Maswali ya Kujadiliana**

1. Eleza hali ya mtu ambaye amekutenda maovu na akakataa umpe msamaha. Je, ulikuwa tayari kumsamehe mtu huyo toka moyoni?

2. Eleza hali ya mtu ambaye amekutenda maovu akirudirudi na kutaka umsamehe. Je, ulikuwa tayari kumsamehe mtu huyo toka moyoni?

   *Petro alimwuliza Yesu kama imetosha mtukusamehe mara saba, lakini akamjibu akimaanisha tusiweke kiwango cha hesabu ni mara ngapi itupasavyo tuwasamehe wengine.Kama tunge-fanya hivi na iwe mara saba kwa siku, basi tutaingiwa na jaribu la kutosamehe wengine. Kila mara inastahili tuwe tayari kusamehe wale wanaojidai wametubu, bila kujali ni mara ngapi wametuomba msamaha.Haistahili kuhukumu kama kweli kutubu kwake ni kwa hakika. "Jilindeni kama ndugu yako akikosa, mwonye, akitubu msamehe". Luka 17:3 TMK (NIV)*

3. Je, fumbo la Mtumwa asiye na msamaha linatufunza nini kati ya msamaha wa sharti na msamaha halisi.Yesu anatufundisha jinsi ya kusali katika Mathayo 6:5-15. Je ni sharti gain anatupa katika mstari wa kumi na nne na tano kuhusu msamaha?

4. Je mwongozo wa Yesu ni upi kwa kukabiliana na hao watutesao? Ni yapi makusudio ya mion-gozo hii na ni kwa akina nani? (Mathayo 18:15-20)

   *Msamaha haustahili uegemee kwa kutubu kwa mkosaji. Akipokekelewa bila msamaha toka moyoni basi hawezi kutubu.*

5. Ni lipi tunashauriwa na Yesu kuhusu wale wakataao kusikia hata kanisa? Je, jambo hili lina uhusiano gani na uchungu?

   *Mkristo anapokuwa na msamaha moyoni mwake, huwa anawazia sana mkosaji aliyemtenda maovu.Hajiwazii yake binafsi.*

**Hatua Ifatayo:Kuitikia neno la Mungu**

1 wakorintho 13:4-5 yatufafanulia vizuri ya kwamba*" Upendo------hauhesabu mabaya."* Upendo hauhesabu gharama. Kama kuna watu maishani mwako ambao umewahesabia ma baya, tafadhali salimisha jozi lako la hesabu kwa Mungu. *Omba* msamaha kwa Mungu uka pate kuelewa huruma zake. Alafu *itikia* wito wa mungu Usamehewe toka moyoni.

# HASIRA YA MTU

**Heather Wilson Torosyan.**

*BWANA anamwambia Kaini, kwa nini una ghadhabu? Na kwa nini uso wako umekunjana? Kama ukitenda vyema hupata kibali?* Sasa hivi mtu ameligonga gari lako, na umekasirika. Umri wake barubaru sitashara aliye jeuri wa hasira. Kwa watoto wote wa leo yeye ndiye amekukasirisha na pia ule utaratibu ulioko wa kuwaachilia watu kama hawa wasiojali kuwa katika barabara za mji. Na kuiondoa hasira hii, baadhi ya wakristo wanatokea na kukusihi *uondoe kabisa hamaki na hasira yako.* Ni vyema, kwa hakika njia hii pia husaidia. *Itakuwa rahisi kwake kusema," hayana maana." Zaidi, Biblia inasema unaweza kukasirika. Yesu alikasirika alipowatimua wabadili fedha kutoka hekaluni. Kwa vyovyote vile, ni vibaya kuweka hasira moyoni, ni heri uwe kweli kuliko mnafiki.*

Kila mara vijisababu na msamaha hutolewa moja kwa moja. Unajaribu kujidanganya kwamba ni sawa kukasirika. Ninashuku sisi sote tumeshasikia na labda zaidi kutumia misamaha hii. Ikiwa mtu yeyote atakuwa mpumbavu kiasi cha kuonyesha kwamba Mungu hataki sisi kukasirika, kwa kifupi tutamhesabulia ni mojawapo ya vijisababu ya yeye kukasirika.

Watu wengine hupandwa na hasira kwa mambo yasemwayo kuwa ni kipumbavu (k.m. mambo yasiyohusika na wewe) :kama kuwa hafifu ofisini, mtu kukukata mbele na haraka haraka kunyakua kiwanda cha kuweka magari, jinsi mume anvyoacha soksi ovyo ovyo sakafuni au mke ambaye siku zote ni kuchelewa .Si haya ni ya kushangaza sana, yanayofanya watu kudunda moyo kwayo?

Wengine waweza kukasirishwa na yale "yaonekanayo ya haki" kama vile njaa ulimwenguni, kuavya mimba, vita, ukosefu wa haki za wananchi, au mapendeleo. Kuna vijisababu vingine vingi vya kuondoa hasira, vijisababu vilivyojitenga kama vile alama za vidole. Walakini silaha yetu kwa vyovyote vile ni kwamba, Biblia ina baadhi ya mambo ya hakika kuhusu hasira.

Vijisababu vitumikavyo kila mara ni, *Biblia inasema uwe na hasira*. Ndiyo, tena ni sawa, kama kidhibitisho, inasema hivi, " Mwe na hasira……" (Waefeso 4:26,NIV=TMK). Hapo ndipo watu hukwamia. Huwa wanapuuza sehemu ifuatiayo inayosema hivi, "na usitende dhambi". Kila mara wakristo hufanya vyema na sehemu ya kwanza ya amri hii bali ile ya pili, kama jambo hafifu lisilo na maana. Aya hii inaongezea sharti la pili kwa amri hii, "jua lisichwe na uchungu wenu bado haujawatoka."

Kuna mafungu mengine ambayo yaweza kutafusiriwa kukubali hasira, "kila mtu na awe mwepesi wa kusikia, bali si mwepesi wa kusema; wala kukasirika…."tena inamaanisha kwamba, usipouondoa mpini hivi sasa,ni sawa.Bali tena, fungu lifuatalo linatuongezea nuru fulani katika somo hili."Kwa maana hasira ya mwanadamu haiitendi haki ya-Mungu"(Yakobo 1:19-20).

Pia labda, ni sawa kuwa na hasira ikiwa;

1.hatutendi dhambi.
2.hatuendi kulala tukiwa nayo.
3.ni hasira kutoka kwa mungu na si ya mwanadamu.
4.inapokea haki.
5.inakuja polepole.

Je? Unahisi kwamba kiasi cha hasira yako kitatoweka ghafla ikiwa utatimiza maagizo haya?

Fungu lingine la Kibiblia lililo kama makimbilio ni ambapo Yesu analisafisha hekalu (Mth 21, Yohana 2). Fungu hili ni hatari sana kulitumia kama dhibitisho, kwa sababu sio rahisi hasira yetu iwe na wama. Hata hivyo, halielezei kinaga ubaga kwamba Yesu alikuwa na hasira, lakini bado tunaona jinsi linaweza kuingiana na mambo manne kati ya haya matano kwenye orodha.

Hasira yake ilionekana kuwa ya Mungu, kwa maana chanzo cha hiyo hasira hii, haikuwa na kujitakari. Alikuwa analitakasa hekalu la Mungu.Matokeo yalikuwa ni wema. Kwa maana, haikuwa dhambi, bali ya Mungu. Ilimjia kwa upole sana ndipo atumie mjeledi. Tukipenda, twaweza kuchukulia kwamba halikuchwa kama angali na hasira.

Kama hatutafananisha hasira yetu na ya kristo, tunaweza kutumia utaratibu ya kuwa *wewe hauelewi.* Pengine mimi sielewi, lakini bila shaka kristo anaelewa. "kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi. (Weabrania 4:15) kristo anasikitikia sana udhaifu wetu lakini hawachii pale, yeye hupeana kwetu rehema, na kupata neema ya ku-

wa mahitaji. (m 16)

Kama tungekuwa werevu zaidi, tungelisema hivi, kwa ajili ya moyo ni vema tuondoe hasira yetu. Hasira ya kujinyamazia pia yaweza kutuletea vindonda vya tumbo. Kwa kweli, ikiwa tutaiondoa hasira yetu, wengine pia waweza kupatwa na vidonda vya tumbo. Ni vigumu sana kwa watu walio na wazo la tatu kupatwa navyo, k.m, kumpelekea Mungu hasira yetu. Hivi sio kumaanisha kuelekeza chuki yetu kwa Mungu (" kweli"). Inamaanisha kukubalia mungu ya kwamba wewe una hasira; ikiwa hautaipokea haki yake, itaonyesha hauitaki. Kwa kukiri huku, hasira yetu inaondolewa kabisa na maisha yetu yanaweza kuendelea kukaa katika furaha ya Bwana na hakuna yeyote atakayepatwa na vindonda vya tumbo.

Maandiko matakatifu yanaonyesha mambo haya machache, kwamba hasira inaweza kuwa salama ikiwa itakuwa katika hali ya kiasi; walakini sanasana yaonyesha ubaya wa hasira na maovu yake.

"Lakini sasa yawekeni mbali nanyi haya yote, na ghadhabu, na uovu, na matukano, na matusi vinywani mwenu." (wakolosai 3:8) makali ya ghadhabu imeorodheshwa kama majowapo ya matendo ya mwili katika wagalatia 5:20. "*mtu wa hasira huchochea ugomvi; na mtu mwenye matusi huasi sana. (metal 29:22)"………….. asiye mwepesi wa hasira ana fahamu nyingi*;" (mithali 14:29) Methali ina mengi ya kusemwa katika fundisho hili.

Huenda sasa hivi umedhibitika kwamba hasira yako haitoki kwa Mungu na ungependa kuiondoa kabisa. Basi utaanzaje? Kwanza ni vizuri uelewe hasira yako imetoka wapi;

> *Mtu mwema katika hazina njema ya moyo wake hutoa yaliyo mema, na mtu mwovu katika hazina mbovu ya moyo wake, hutoa yaliyo maovu; kwa kuwa mtu, kinywa chake hunena yale yaujazayo moyo wake. (Lk 6:45)*

Tukionacho hapa ni kwamba, tunda la uzima wetu latokana na hali ya mioyo yetu ilivyo. Ikiwa mioyo yetu itakuwa na hazina ya maovu, yatakayonenwa ni maovu. Kama hivi ndivyo ilivyo, lazima mambo mawili yatimizwe; la kwanza, limeelezwa katika zaburi 139:23-24, "Ee mungu, unichunguze, ujue moyo wangu, unijaribu, uyajue mawazo yangu; uone kama iko njia iletayo majuto ndani yangu, ukaniongoze katika njia ya milele." Ikiwa tunaenenda katika nuru, jinsi yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote. Tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na ni wa haki atatuondolea dhambi zetu na kutusafisha na udhalimu wote.(1 yohana 1:7,9) hasira itatoweka mioyoni mwetu jinsi wabadilisha fedha walivyotoweka kutoka hekaluni.

Mara tu mioyo yetu inaposafishwa, tunastahili kuijaza kwa kila aina ya mambo mazuri. Mambo yaliyo ya kweli, yenye kuheshimika, manyoofu, safi, yenye kupendeza, yenye sifa nzuri, mazuri sana, na yenye wema wa sifa; yakiwa baadhi ya mashauri. Paulo anatupa katika wafilipi 4:8. Pia yanaweza kutafusiriwa kama kufanywa upya nia zenu (Warumi 12:2)

Je! Swali hili la kuondoa kabisa hasira laonekana kwako kama ni la upuzi na lisilowezekana? Kama ingekuwa kwa nguvu zetu wenyewe ,kuweka uzuifu kamili; fikira hii haingewezekana. Bali, mshukuruni Yeye si hivyo.

> *Kwa yeye awezaye kuwalinda ninyi msijikwae, na kuwasimamisha mbele ya utukufu wake bila mawaa katika furaha kuu…………Amina (Yuda 24)*

*Ufahamu: katika kizazi ambacho hakizungumzii* ***sana*** *kuhusu kuipenda nafsi, hauwezi kupata mtu ndani yao ambaye anajipenda sana.upande mkubwa wa hasira hautokei kama kujizuia kwa wengine. Huo ni ushawishi usababishwao na kule kujipenda nafsi sana. Waweza kusema, "mimi ni mkubwa sana au mwenye heshima kubwa kutendewa hivi. Kwa hivyo hasira, ikiwa itakuwa na "makali ya ghadhabu" basi tabia hii ni ya asiye mkristo. Yesu anatuokoa kutoka kwa orodha ya kazi ya mwili ilivyo kwa wagalatia 5:19-21, na unatuokoa kuingia kwa tunda la roho (wagalatia 5:22-23).*

*Kama* ***wewe*** *ni mkristo na unafahamu una "makali ya ghadhabu" basi ni lazima ukiri na kuyawacha leo hii.*

*J.W*

***MWONGOZO WA SOMO: Hasira ya Mtu.***

*BWANA akamwambia Kaini "kwa nini una ghadhabu? Kama ukitenda vyema, hutapata kibali? (mwanzo 4:6-7a)*

**Maswali ya Kujadiliana**

1. Mtu anaweza kuelewaje umekasirika?

. 2. Eleza wakati wa mwisho kwako kukasirishwa sana.

. 3. Waefeso 4:26, inatuambiaje kuhusu hasira?
   *Kwa maana hasira ya mwanadamu haitendi haki ya mungu (yakobo 1:19-20)*

. 4. Mungu anasema nini kuhusu madhara ya hasira na maovu yake?
   Wakolosai 3:8,
   Wagalatia 5:20
   Mithali 29:22
   Mithali 14:29

. 5. Hasira yako yatoka wapi?
   *Mtu mwema katika hazina njema ya moyo wake hutoa mema, kwa kuwa kinywa chake hunena yale yaujazayo moyo wake (luka 6:45)*

6. Tunda la uzima wetu hutoka kwa hali ya mioyo yetu. Ikiwa mioyo yenu ni hazina ya maovu kitakachotoka ni maovu. Ni hatua gani mbili za lazima kuchukuliwa ikiwa unapenda hasira yako itoweke?
   Hatua ya kwanza:
   Hatua ya pili:

**Hatua ifuatayo: Kuitikia Neno la Mungu.**

Ikiwa tunataka kupeana hasira yetu kwa Mungu na kukiri maovu yetu, Mungu ametuahidi kutuumbia moyo safi. Angaza vile wewe unavyokabiliana na hasira. *Omba* Mungu akuchunguze moyo na mawazo yako, akidhihirisha kila njia ya uovu ndani mwako. *Itikia* kwa kumkubali Mungu awe kiongozi na *"……ukaniongoza katika njia ya milele" (zaburi 139:24)*

## MAKALI YA GHADHABU

Jim Wilson.

***Basi matendo ya mwilini dhahiri, ndiyo haya, Uasherati, Uchafu, Ufisadi, Ibaada ya sanamu, Ugomvi, Uchawi, Uadui, wivu, hasira, fitina faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi, na mambo yanayofanana na hayo, katika hayo nawaambia ya kwamba, watu watendayo mambo ya jinsi hiyohawatauridhi ufalme wa mungu. (Wagalatia 5:19-21)***

***Lakini tunda la roho ni upendo, furaha, amani uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi, juu ya mambo kama haya hakuna sheria. Na hao walio wa Yesu kristo wameusulubisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake. Tukiishi kwa roho na tuenende kwa roho. (Wagalatia 5:22-25)***

Nimewahi kushuhudia baadhi ya makali ya ghadhabu yaliyo na "**kovu**" sana.

Wakati mmoja nilienda kumkabili pasta ambaye hakuwa mwaminifu. Alikuwa amewatembelea vijana wake wa kike katika chumba cha mkewe cha kusukumwa. Hakunijibu kwa hasira, walakini baadaye alipandwa na "makali ya ghadhabu" kwa mkewe na bintiye mmoja. Alikuwa angali katika hali hatari alipokuwa akiondoka, na nikafunga mlango. Alirudi tena na kuurukia malango kwa nguvuna kuanza kulitingiza gari. Alikuwa ameoa mke mwingine baada ya miaka kumi akatubu.

Miaka mingi iliyopita mimi na Bessie tuliandamana pamoja tukitumayi kuwapatanisha watu waliooana. Yule "mke wa pili" alikuwa pale. Huyo "mke wa pili" alionekana kukasirika. Hakuna aliyejeruhiwa. Akaondoka akaenda zake kwa gari. Hakuwa mkristo hataa.

Wakati mmoja palitokea mtu aliyenijia mle borini mwangu ili kunipasha habari ya kwamba anaenda kumwua mkewe, alikuwa mwenye ukali na ghadhabu. Tuliweza kumficha mkewe hadi alipotuliza ukali wa ghadhabu. Hakuwa mkristo hataa.

"Ukali wa ghadhabu" ni kitendo cha mwili. Huonekana sana tena wazi wazi katika watoto wachanga. Tunauita "wivu na hamaki". Mtoto anapoendelea kuwa mkubwa tunabashiri kusema kwa dhihaki"wivu, wivu, wivu"kwa kawaida dhihaka haiwezi kukomesha mwasho. Tuna maneno mengine yaonyeshayo makali ya ghadhabu. "Kuupoteza' na "kudundwa," ni mawili baadhi ya hayo. Maneno haya ni ya sifa kuyatumia na ni mazuri kuonyesha makali ya ghadhabu, walakini hayaonyeshi ule uovu. Baadaye sisi huendelea kubuni maneno yanenayo ouvu huu na kutojali makali ya ghadhabu. Neno lingine ni "kukatanisha tafaki". Hili ni nzuri sana kwa mtu aliye mwepesi wa hasira. Sisi wote tunawaelewa watu kama hawa, wengine wao hujivuna kuwa wakataji tafaki. Jamaa na marafiki wao wamejifunza jinsi ya "kuenenda pole" nao au "kuwaepuka". Watu hawa huwaogofya sana jamaa zao au kuwafanya mateka wa hamaki yao. Kwa maana inaweza kulipuka wakati wowote.

Kinyume cha matendo ya mwili ni tunda la roho. Ni rahisi kuona ya kwamba kujizuyia ni kinyume cha makali ya ghadhabu. Unyume huu sio pekee. Mtu aliye na makali ya ghadhabu hana upendo, furaha, amani, uvumilivu, upole, wema, uaminifu, au uungwana. Ukali wa ghadhabu huondoa yote yatokanayo na tunda la roho. Ndiyo maana ya sababu hii, mtu asiyezaliwa kwa roho huenda kwa mwili.

Mtu akizaliwa kwa roho, basi makali ya ghadhabu hayatakuwa mazoea wala kukubaliaka kwake. Ni upambanuzi gani unaonyesha kwa nini wakristo huwa wanakasirishwa? Kwanza kabisa, hakuna upambanuzi wowote au uzuri wowote unaoweza kuhalalisha kuwa na hasira. Upambanuzi wa kawaida ni kwamba mtu wa ukali wa ghadhabu ni mtu hajaokoka, hajazaliwa kwa roho, yeye sio mkristo. Ingawaje, ikiwa ni mkristo amekusanya dhambi nyingi ndogo ndogo ambazo hajatubu, hajakiri na ambazio hajakubali kupokea msamaha. Na sasa yuko tayari kutunbukia kwenye jaribu dogo lenye makali ya ghadhabu. Mkusanyiko huu umewasilishwa katika njia hii:

*Umzuie mtumishi wako asifanye mambo ya kiburi;*
*yasinitawale mimi. Ndipo nitakapokuwa kamili,*
*nami nitakuwa safi, sina kosa lililo kubwa. (Zaburi 19:13)*

Ufahamu ya kwamba fungu hili ni mojawapo ya kizuizi. Mkristo ambaye amejipeana katika makali ya ghadhabu hangependa kuzuiliwa dhambi za kusudia. Amekubali zimtawale yeye. Basi huwa anamalizia kutenda kosa kubwa.

Itakuwa vigumu sana kwako kuzuia makali ya ghadhabu ya usoni kabla haujakiri na kutubia ile ya kwanza. Kukiri huku hakustahili kuwe na madoido yatakayolegeza uzito wa ile dhambi. Ni lazima uhusishe dhambi zote za kusudia ambazo zilisababisha makali ya ghadhabu;

*Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na*

*Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na kristo, yatafuteni yaliyo juu, alikoketi kristo mkono wa kiume wa Mungu. Yafikiri yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi. Kwa maana mlikufa na uhai wenu umefichwa pamoja na kristo katika Mungu. Kristo atakapo-funuliwa, aliye uhai wetu, ndipo na ninyi mtafunuliwa pamoja naye kaika utukufu. (Wakalosai 3:1-4)*

Ushauri huu wa wakolosai ni maneno ya msingi ya kujiepusha na ghadhabu, hasira na maaovu mengine mengi yanayo "karibiana sana" nayo. Ushauri huu unatenda kazi tuu ikiwa wewe ni mkristo, kwa sababu ni mkristo pekee anaye-weza kutii masharti yafuatayo;

*……inueni mioyo yenu kwa vilivyo juu………*

*Elekeza mawazo yenu kwa vilivyo juu………*

*……bali sio kwa vilivyo duniani.*

Maagizo haya yamewekwa kama msingi wa ishara wa mashauri yafuatayo. Hapa hapahitaji tendo lolote. Tayari ni kweli kama upo ndani ya kristo.

*………mkiwa mmefufuliwa ndani ya kristo……….*

*Kwa maana mlilkufa na uhai wenu umefichwa pamoja na Mungu.Kristo ataka pofunuliwa, aliye uhai wetu, ndipop na ninyi mtakapofunuliwa pamoja naye katika utukufu.*

Mara tuu mioyo na akili zetu zinapokuwa "katika hali nzuri' na kristo, basi tumepewa ushauri ufuatao;

*Lakini sasa, yawekeni mbaki nanyi haya yote, hasira na ghadhabu, na uovu na matukano, na matusio vinywani mwenu. (Wakolosai 3:8)*

Kadhalika, wasia huu haujapeanwa kwa mtu ambaye siye mwana wa Mungu. Hivi hai-maanishi mambo haya hayakubaliwi kwa wasioamini; bali wasioamini hawawezi kuyatii. Wanaweza kuonyesha hasira na ghadhabu, walakini hawawezi kuiondoa bila kutubu kwa Mungu na kwa imani ndani ya Bwana Yesu kristo. Asiyeamini anastahili atubu dhambi zake kwa Mungu, na akiri kwamba Yesu kristo ni Bwana, aazimu moyoni mwake kwamba Kristo alikufia dhambi zake na alifufuka katika wafu. Na hapo basi atamwitia yeye;

*Yesu akamwambia, "ndivyo ilivyoandikwa: Kristo huyo atateswa na kufufuka siku ya tatu, na mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi………" (Luka 24:46, 47)*

*Kwamba ikiwa umekiri kwa kinywa chako, "Yesu ni Bwana" na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka……… kila atakayeliitia jina la Bwana ataokoka." (Warumi 10:9,13)*

**Mwongozo wa somo: Makali ya Ghadhabu**.

*Basi matendo ya mwili ni dhahiri: uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi na mambo yanayofanana na hao, katika hayo nawambieni mapema, kama nilivyokwisha kuwaambia, kwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawatauridhi ufalme wa mbinguni. (Wagalatia 5:19-21)*

**Maswali ya Kujadiliana.**

1. Wagalatia 5:19-21 inatupa orodha ya maovu yanayotuzuia sisi tusiwe na uhusiano wa karibu na Bwana. Kuna msemo usemao, “wale waishiayo haya”.Hii ni taarifa ya mazoea. Ikiwa “makali ya ghadhabu” au mojawapo ya maovu hayo mengine itakuwa mazoea, hau tauridhi ufalme wa mbinguni. Je, ni maovu gani yanakuzuia wewe?.

2. Ikiwa sisi ni wa Yesu kristo, tumeufanyia nini mwili wa dhambi? (Wagalatia 5:24) “*ukali wa ghadhabu” ni kitendo cha mwilini. Tunapoendelea kuzeeka huwa tuna vita “hamaki ya wivu”, “kuupoteza”, au “kudundwa” katika watoto. Uzuri wa maneno haya ni ya sifa walakini haya badili kitendo kuonekana ni uovu. Ni kitendo cha kawaida kwa wasio wakristo. Sio halali wala kukubali kwa wakristo. Ikiwa, orodha ya kwanza ya (Wagalatia 5:19-21) inakuhusu wewe vi zuri, basi una kila sababu ya kuamini wewe haumo ndani ya kristo. Yesu kristo anafanya kazi nzuri ya kuokoa kuliko hiyo. Ikiwa utakuwa katika orodha hizi zote, basi inakulazimu utoke katika orodha ya kwanza kwa kuyakiri na kuyaacha kabisa*.

3. Ni hali gani au swali lipi ambalo linakuvuta nyuma wakati wowote litokeaopo?

4. Tufanye nini ili kuepuka “makali ya ghadhabu” kutokolea ndani mwetu? (Zaburi 19:12-13)

5. Wakolosai 3:8 inatuamuru tujiondolee mambo yapi?

6. Wakolosai 3:9 inatupa “kwa nini” na “ni aje”. Ni yapi haya?

7. Kuna tofauti kati ya habari ya kuonya na habari ya kulazimu. Kuonya ni ambacho kinastahili. Kulazimu ni amri kutenda. Kwa hivyo Wagalatia 5:24 ni habari ya kuonya au ya kulazimisha? *Mara tu tunaposulubisha tama ya maovu yetu, basi roho mtakatifu anatuum,bia tabia tofauti kama ile ipatikanayo kwa desturi ya kristo. (Wagalatia 5:22-23)*

**Hatua Ifuatayo: Kuitikia Neno la Mungu.**

*Angaza* sehemu katika maisha yako ambazo zinazuia roho mtakatifu kutotenda kazi ndani yako.*Itikia* kwa kumruhusu Mungu awe kiongozi kwako. *Kaeni ndani yangu nami ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake; lisipokaa ndani ya msabibu. Kadhalika msipokaa ndani yangu hamtazaa matunda. (Yohana 15:4)*

## KUUCHUKUA UOVU

*Heather Wilson Torosyan*

Kutokana na waraka wa Yakobo, tunajua ya kwamba ikiwa mtu atauzuia ulimi wake amefanya vema zaidi hata kuufikilia utimilifu, na uwezo wa kuzuia mwili wake wote. Ugumu ni kwamba kuna watu wengi wadhaifu ambao hawajajifunza bado jinsi ya kuzuia ulimi. Basi mda sio mda watu hujeruhiwa kulia na kushoto kwa yale watu wengi husema.

Sio ulimi pekee waweza kujeruhi, bali pia na matendo. Basi, sio tu marafiki wetu wote, na wale tuwajuao wauzuia ulimi wao bali vile vile waaambatanishe haya kwa miili yao.

Kwa vijisababu fulani, huwa tunaelekeza lawama zote kwa mkosaji kuliko mhadhiriwa. Sina lengo la kuutetea ulimi usiozuiliwa. Ni lazima ulimi utawaliwe. Kitambo ufike hapo, kuna *haki* ya mimi kujeruhiwa? Ni lazima niendelee kupatwa na hisia za majeruhi hadi watu wengine watakapoufikia utimilifu? Yanionekania kwangu maswala haya mawili hayana umuhimu wowte wowte. Kifikia utimilifu kama huu.

Tungependa tuwe na watu walio wazuri k ili tusipatwe na hali hii ya kujeruhiwa. Kwa kawaida jambo hili si la hakika, na ningependekeza ya kwamba mhadhiriwa azidi kujitahidi.

Mojawapo ya njia ningependekeza kuyazingatia haya ni kuangalia mfano wa Kristo, *alidharauliwa na kukataliwa na watu, mtu wa huzuni nyingi ujuaye sikitiko, na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao. Alidharauliwa wala hatukumhesabu kama kitu…wakamdhulumu na kumtesa, ingawaje hakufanya kinywa chake. (Isaiah 53:3,9)*

Yeyote kwa sisi, akiwa sawa katika hali hii anaweza kuona tuna haki zote za kujeruhiwa. Ikiwa ni hivyo ndivyo watakavyokuwa, niangalieni kama nitawahi; (1) Kuongea nao tena, (2) Kuwa mzuri kwao tena, (3) Kuwasamehe, au (4) Kufa kwa ajili yao. Kama Bwana wetu angelitenda hivi, hangelienda msalabani kwa ajili yetu. Ingawaje, jambo hili lilikua la kipekee. Alikua na uwezo wote wa Mungu – Yeye kuamuru. Sisi sio wakamilifu bali Yeye ni mkamilifu.

Iweni na nia hiyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristu Yesu, ingawaje yeye alikuwa ana namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu: kitu cha kushikamana nacho, bali yeye mwenyewe, alijifanya kuwa si kitu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa mwanadamu, yeye alijinyenyekesha mwenyewe kwa kutii hata mauti, naam, mauti ya msalaba.(Wafilipi 2:5-8)

Kwa kifupi, inatupasa sis kuwa na nia hiyo hiyo ya Kristu katika sura hizi nne:

1.Usikatalie utofauti au wema wako.
2. Jishushe usionekane kitu
3. Uwe kama mtumwa
4. Uwe mnyenyekevu

Tukiwa na nia kama hii, tutayaweza yote katika furaha itungojeayo upande ule mwingine kwa kustahimili kila aina ya msalaba, pasipo kuwazia lolote la aibu litakaloshikamana nalo. (Waebrania 12:2)

Kwa kawaida,wale wenye kutudhuru sana ni walio wa karibu sana nasi. Uwezekano wa mgeni ni mdogo sana kudhuru kuliko ule wa Mume, Mke, Rafiki, Ndugu au Dada. Unapojeruhiwa na mtu wa karibu, huwa tunajiambia hivi, "Ikiwa kweli angelinipenda, hangelisema hivyo".

Bali kwa kuchanganua usemi huu, haswa hutambulikana wazi ni nani tunayemwazia. Je, tunawazia kuhusu ukosefu wa upendo wa yule mtu mwingine na vile anavyohitaji msaada? La hasha, tunawazia jinsi ukosefu wa huo upendo katika mtu yule utakavyotudhuru sisi. Kwa maneno mengine, tuna kiburi-cha kujiwazia nafsi na jinsi matendo ya nafsi yanavyo husiana na watu wengine wote.

Fungu litumiwalo sana kuhusu upendo ni 1 Wakorintho 13. linaelezea upendo kuwa, "… Hautafuti mambo yake, hauoni uchungu, hauhesabu mabaya".

Tunapohisi kujeruhiwa, ni kwa sababu msamaha wa karibu haumo moyoni mwetu. Maumbile ya msamaha *hauhesabu mabaya*. Katika Waefeso 4:22, fungu lijulikanalo sana, bali ni nadra liwekwe kwa vitendo, ambapo Paulo anatwambia, "Iwe wafadhili nyinyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama vile katika Kristo Mungu aliwasamehe ninyi". *Lazima* tusamehe jinsi tumeshasamehewa. Kumbuka 70X7. Hakuna idadi na bila shaka hakuna aliye na uwezo wa Bwana wa kusamehe.Tukizingatia ya kwamba kwa kila jaribu la uovu ,Bwana anatufadhili na njia ya kuepukia, kwa nini sababu ya kufanya kila mmoja akose kujeruhiwa tena.? Linasikika kama agizo lenye shaka, na ninafahamu wengi watasema haliwezekani. Lakini ni amini

kwangu kwamba ikiwa Bwana aliahidi njia ya kuepukia ,kila wakati itakuwepo njia.

"*kuwa magumu" haimaanishi "kujenga ukuta" au njia zingine zenye ujanja ndani ili kuepuka kupatwa na jeruhi. Haitendeki hivyo; hivi ni kumaanisha ya kwamba mtu huyu awe mgumu na sugu. Umfuate Yesu kama mfano jinsi ilivyo katika 1 Petro 2:21. Yesu aliishi kujeruhiwa. Mtu huyu anaishi kiurahisi. Haonekani kuwa mgumu. Njia nzuri na safi ya "kuwa mgumu" ni kuishi mlegevu na kulichukua. Jeruhi hupungua.*

*J.W.*

**MWONGOZO WA SOMO: Kuuchukua Uovu.**

*Alidharauliwa na kukataliwa na watu, mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko. Na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao alidharauliwa, na hatukumhesabu kama kitu, alionewa na kuteswa, wala hakufunua kinywa chake; kama mwana kondoo apelekwaye machinjoni, na kama vile kondoo anyamazavyo mbele ya watoa manyoa yao; naam, hakufunua kinywa chake. (Isaiya 53:3,7)*

**Maswali ya Kujadiliana.**

1. Eleza wakati ambao alilaumiwa na kuadhibiwa kwa jambo ambalo haukulifanya.
2. Je, ulisikia uchungu au ulisikia vyema kwa sababu ulipata kuyajua haya?
3. Yawezekanaje uwe na nia moja- sawa na kristo wakati mtu amekutenda maovu? (Wafilipi 2: 5-8)
4. Orodhesha sifa za upendo. (1 Wakorintho 13:5-8).
   *Wakati tunapohisi kujeruhiwa, ni kwa sababu hapana msamaha wa karibu ndani ya mioyo yetu*.
5. Tumeagiziwaje jinsi ya kukabiliana na wale wanao tujeruhi? (Warumi 12:17-21).

**Hatua Ifuatayo: Kuitikia Neno la Mungu.**

*Angazia* maagizo ya Mungu katika 1 Wakorintho 13:4-5. upendo huvumilia, hufadhili, upendo hauhusudu, haitakabari, haijivuni, haukosi kuwa na adabu, hautafuti mambo yake, hauoni uchungu, hauhesabu mabaya. Ikiwa tunataka kuwa waigaji wa Kristo, basi ni lazima *tumuulize* Mungu atufahamishe kwa nguvu zake na wema, akituwezesha sisi kusamehe kutoka moyoni. *Itikia* wale wanakuudhi kwa moyo huo uo wa upendo na kwa msamaha unaopewa  na Mungu.

# KUUZUIA ULIMI

*Chris Vlachos*

Wakati mmoja uliopita kulitokea kimbunga cha samaku kule falme ya New York, ambacho kilisababisha kutaharuki mawasiliano ya simu na ule mtandao wa radio uliorushwa hewani kutoka kituo cha radio kilichokuwa karibu. Matokeo yake ni kwamba, mawasiliano ya watu hawa wawili yalitanda hewani kwa pamoja bila hao kujua kwamba sauti zao zimeshikamana hewani. Kilikuwa kipindi cha pita nipishe.

Sisi sote kwa wakati mmoja au mwinginetumekua na hatia ya kudakua. Kwa hakika, kuna udaku mwingine katika makanisa mengi ya kumfanya malaika wa kunakili matendo yetu kuhuzunika na kulia anaponakili habari hizi. Tabia hii ni ya uovu ambayo Mungu huichukulia kwa uzito sana na anatuhitaji tuiache mara moja.

Katika 1 Timothi 3:11 Paulo amezungumzia udaku akisema, "Vivyo hivyo lazima wawe wastahivu, si wasingiziaji, bali wenye kiasi, waaminifu katika mambo yote. "Tusije tukafikiria ya kwamba wanaume hawawezi kupatwa na ugonjwa huu. Vivyo hivyo Paulo anatuhubiria katika waraka wake wa pilik wa Timotheo, akibashiri kwamba, siku za mwisho watu watakuwa wasiopenda wa kwao, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, wakali, wasiopenda mema." (2Timotheo 3:3)

Neno ambalo Paulo ametumia katika hali hizi mbili ni neno la kigiriki, *diabolos*, ambalo ni jina tulijualo kwa tafsiri yake "ibilisi". Haituhitaji kuenda kwa kalenda ya watakatifu ili kutaka kumjua ni mtakatifu yupi aliyemwanzilishi wa udaku ambaye ni shetani. Basi mdakishaji sio mwingine ila ni "mpeleka-barua wa ibilisi" .

Wakati mwingine neno *diobolos* limetafsiriwa kama "msingiziaji". Udaku ni usingiziaji. Maneno yaliyonakiliwa hapo juu kutoka kwa, Timotheo 2, Paulo analiweka neno udaku katikati ya orodha ya matendo ya uovu. Sehemu nyeti ya tabia ya udaku imeelezwa wazi wazi.

Bahati mbaya, kila mara ni vigumu sana kuutambua udaku/ usingiziaji uliomo ndani mwetu. Tutajuaje kama sisi ni wadaku? Kuna maswali manne ya kujiuliza tunapojaribiwa kushiriki mazungumzo na wengine. Majibu kwa maswali haya sana sana yataonyesha ikiwa sisi tunadakua watu au hatuwadakui/kusingizia.

***1.Kwa nini ninasema hivi?***

Kweli, kusudi langu ni kudhihaki Nipo hapa kumsaidia mhusika ninayemzungumzia, au lengo langu ni kuwajeruhi? Kila tukuapo na lengo la kushirikiana katika maombi, hakika sisi hudakiana au kusingiziana. Mara kwa mara tunatoshanisha udaku wetu kwa lengo la kumshusha yule mwenzetu asiinuliwe ili sisi tupate kujiinua kwa mafias yake nzuri aliyonayo. Uwe mwangalifu jinsi unavyojibu swali hili la kwanza. Ikiwa utajikuta ukijaribu kuhalalisha au kutetea uovu ambao upo tayari unaelekezwa kunenwa juu ya mtu mwingine, kuna uwezekano wa wewe kuwa mtegoni kusingizia.

***2.Je, kuna uwezekano kuwe na jambo lig nin kando ya habari hizi?***

Kulingana na kamusi ya Webster inatuarifu ya kwamba udaku ni "kueneza uvumi". Uvumi ni habari isiyo ya kweli. Ikiwa habari tunayopeana sio ya haki basi tunadakua. Inasemekana ya kwamba shida zitokeazo makanisani hazisababishwi na watu wasemao habari kamili, bali ni watu wanaoongezea habari za uongo juu ya ile ya kweli.

***3.Je, nitasikia kufarijika nikiambia yesu manbo haya?***

Ni lipi Yesu angelitujibu, baada ya sisi kumshirikisha katika habari za uongo kuhusu mtu mwingine? Bila shaka angelitujibu kwa kutuuliza ikiwa habari hizo zina uhusiano wowote kwetu sisi kumfuata Yeye (Yohana 21:22). Ikiwa utajihisi kutofarijika kwa kumshirikisha Bwana katika habari hizo, basi sio vema kushirikisha mtu yeyote

***4.Ninamjenga mtu ninaye mzungumzia kwa kumshirikisha mambo haya?***

Wakati mmoja Charls Spurgeon alisema hivi, udaku "hutokeza sumu mara tatu; huumiza msimulizi, msikilizaji na mhusika." Tunastahili tuwe waangalifu na kuyatii mausia ya Paulo, "neno lolote lililo ovu lisitoke vinywani mwenu, bali lililo jema la kumfaa mwenye kuhitaji, ili liwape neema wanaosikia. (Waefeso 4:29)

Majibu kwa maswali manne yaliyopo hapo juu yatatusaidia sisi kutambua udaku/ usingiziaji. Baada ya kujiuliza maswali haya manne na ungali hauna uhakika na yale unayoenda kushirikiana ni udaku, basi usiyanene kamwe. Ni lazima unene ya kweli?

Wazo moja na la mwisho. Ni jinsi gani tunaweza kuzuia tabia hii ya uovu wa kudakua ambao sio tu kusababisha balaa kwa maisha yetu

bali pia huingia na kuharibu makanisa? Tiba ya udaku ni mara mbili. Kwanza, usivumishe habari za uongo. Udaku ni uvumi unaoingilia sikio moja na kutokea kinywani mwa mtu. Uzuie ulimi wako!. Ikiwa hauwezi kunena lolote jema kuhusu mwenzio na usidhubutu mazungumzo kabisa. La pili, usidhubutu kusikiliza habari za uongo! Hauwezi kuwa na ndimi ya udaku pasipo na masikio ya udaku. Usihimize msingiziaji kutoa habari hizi. Usiwe mwepesi wa kuyasikiliza wasemayo. Geuza mazungumzo hayo kwa kujadili mema kuhusu mhusika. Hakuna litakalombadilisha haraka mdakuzi/msingiziaji ila kufanya hivi.

Imesimuliwa ya kwamba udaku hauna miguu wala mabawa, bali ni "hadithi" za kutunga kabisa. Kwa huzuni nyingi hadithi hizi huchoma na huleta madhara ya sumu kwa kazi ya kuhuisha maisha ya kanisa. Ingawaje tumekuwa tukisumbuliwa kila mara na nyigu- udaku hekaluni; basi hebu haya maradhi ya kishetani, udaku, yapate kukomeshwa makanisani mwetu katika nchi.

*Hatimaye, ndugu zangu, mambo yoyote yaliyo na ukweli, yoyote yaliyo na staha, yoyote yaliyo ya haki, yoyote yaliyo safi, yoyote yenye kupendeza, yoyote yenye sifa njema………… ukiwemo wema wowote au sifa nzuri……… yatafakarini hayo. (Wafilipi 4:8)*

**MWONGOZO WA FUNZO**: **Kuuzuia Ulimi.**

*Jitahadharini kwa haya: ya kuwa siku za mwisho kutakuweko nyakati za hatari. Maana watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe, kupenda fedha, kujisifu, wenye kiburi, kutukana, wasiotii wazazi wao, wasio na shukrani, wasio safi, wasiopenda wa kwao, wasiotaka kufanya suluhu wasingiziaji, wasiojizuia, wakali, wasiopenda mema, wasaliti, wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu. (2 Timotheo 3:3-4)*

**Maswali ya Kujadiliana.**

1. Jee, Waefeso 4:29 una yapi ya kusimulia kuhusu udaku?
2. Paulo ameongelea kuhusu *udaku wa kijicho* katika 1 Timotheo 3:11 na 2 Timotheo 3:3. ni nini tafsiri ya kila neon, ya maneno haya mawili?
   Kijicho:
   Udaku:
3. Jee, ni nani mtakatifu mwanzilishi wa udaku?
4. Peana orodha ya maswali manne ambayo tunaweza kujiuliza sisi wenyewe tunapojaribiwa katika kutoa habari za uongo kuhusu mtu mwingine.
   *Udaku ni kusingizia. Hamna kitu kama udaku usiodhuru (mzuri). Udaku hauna miguu wala mabawa bali ni "hadithi" za kutungwa kabisa ukiwa na sumu ya kuuma.*
5. Paulo ana dawa gain ya kuponya udaku, na kila aina nyingine ya kijicho? (Waefeso 4:31-32)

**HATUA IFUATAYO: Kuitikia Neno la Mungu.**

Mungu anatuuliza tumtengee wasaa na wakati wa kukutana naye kila siku. *Muulize* Yeye ayafanye upia mawazo yako,aifanye upya roho yako na akupe nguvu mpya itakikanayo ili uwe na nia ile ile ya Kristo. K*uitikia* kwa kukubali upendo wa Mungu ukuongoze kwa kila ulinenalo na jinsi unavyowazia.

*Maneno ya kinywa changu, na mawazo ya moyo wangu Yapate kibali mbele zako, Ee Bwana, Mwamba wangu, na Mwokozi wangu. (Zaburi 19:14)*

## KUJITAFAKARIA

*Jim Williamson*

Kujitafakaria ni tabia ya kujifikiri au kujiwazia matendo au hisia zako za hapo zamani. Kuwaza huku hutuletea mambo hayo akilini mwetu, nasi kuyaangalia kwa kiundani, kujiinua katika nuru iyumbayumbayo kama ile ya msumaa akilini mwetu; kujitafakaria hushawishika kila mara, kwa mambo yetu ya wakati uliopita, aidha zamani zile au hivi sasa, ambapo wengi huona kuwa ni kisababu cha kueleza matendo na maono yetu ya leo. Hata bila kushawishiwa na wengine, mara nyingi tabia hii hutendeka kwa wakristo wengi.

Kujitafakaria sio kama unavyoenda kutembea chini ya miale ya jua wakati wa kiangazi. Badala yake, huwa kama unavyoteremka chini ya daraja lile la gerezani huku ukiwa umebeba msumaa ambao unayumbyumba mkononi mwako. Kwako kuna mwangaza mdogo sana ambao unamulika vivuli virefu na kuonyesha mifupa kwa umbali, na tando za buibui, na wadudu wabaya wenye kutambaa.

Vivuli hivi vya mifupa ni mambo ambayo tulitenda hapo zamani ama tumetenda hivi sasa na kuaibika kwa hayo. Pia yamechanganyikana na kudhania kwetu. Mtu aliye na uzoefu wa kujitafakaria huendelea kuwazua kwa undani kiwango cha kujichimbia shimo la kaburi au kurudiarudia kuchungua vivuli hivi mara kwa mara. Mwangaza wa msumaa sio mzuri sana na hauna suluhisho lolote kwa tabia hii ya kuchukiza ya kuwazua yaliyopita. Sawasawa na uchawi kisa hiki hakina chanzo chochote chenye furaha. Kila chanzo ni kisababu cha kuhuzunika. Labda ndicho kisababu kikukubwa cha kuhuzunika kwa watu walio wachungu, wenye kusingizia ukamilifu wa nafsi.

**Thibitisho la hukumu**

Kujitafakaria hukusemesha mambo yafuatayo; “Ni mabaya jinsi gani? Ni machafu jinsi gani? Bwana ataniwezesha kuyafahamu? Ningekuwa Mungu singejisamehe?”

Kujitafakaria ni kuvunjika moyo si kujipa moyo. Yeye ni mshtaki sio msadikiki.

Kwenye mahakama kuna tofauti kati ya mshtaka na msadikishi. Mshtaka ni wakili na msasdikishi ni hakimu. Wakili hutafuta kuhakikisha kosa na hakimu hutoa uamuzi baada ya kosa kuhakikishwa. Mara tu hakimu anapotoa uamuzi basi kesi hufikia kikomo. Hata hivyo, wakili ataendelesha kusisitiza kwamba mshtakiwa yu na hatia hata kama hakimu atasema mshtakiwa hana hatia.

Katika Bibilia, mshtakiwa ni shetani na msadikishi ni roho mtakatifu.

**Nuru Halisi**

Sehemu nyingine ya kujitafakaria ikiandamana na kinyume cha matokeo yake, inapatikana kwa 1Yohana 1:5-10. Nitanakili mstari wa 5 na 7, “Na hii ndio habari tulioisikia kwake, na kuihubiri kwenu :Mungu ni nuru;ndani mwake hamna giza kamwe………..Bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo nuruni twashiriki sisi kwa sisi na damu yake Yesu, Mwana wake yatusafisha dhambi yote”

Nuru hii ndio chemichemi ya nuru yote. Sio kama msumaa unaositasita kwa giza. Humo hamna vivuli kamwe na Yakobo anasema hivi kuhusu jambo hili sura ya 1:17 *“Kila kutoa kuliko kwema, na kila kitolewacho kilicho kamili, hutoka juu, ishukayo kutoka kwa baba wa mianga na mbinguni, Asiye badilika badilika kama vile vivuli hugeuka geuka*”

Kupewa nuru hii kwamba ni kamilifu hatutafichwa chochote, ikiwa turatembea kwa hiyo. Dhambi imedhirishwa katika nguvu za hukumu jinsi ishindanavyo na nguvu za mashtaka. Dhambi husamehewa papo hapo kwa maana damu ya Yesu huendelea kusafisha bila kukoma Ushirika ni kawaida kwa sababu tumo nuruni na tunasafiwa bila kukoma. Kutii ndilo tukio la tabia kamili ya hukumu na kusafiwa.

Kuna mfano wa ajabu wa aina hii ya dhibitiko –Usafisho-Ushirika-Utiifu katika Isaya 6:1-8

*Katika maka ule aliokufa mfalme Uzia, nalimwona Bwana ameketi katika kiticha enzi, kilicho juu sana na kuinuliwa sana, na pindola vazi lake likalijaza hekalu. Juu yake walisimama maserafu, kila mmoja alikuwa na mabawa sita;kwa mawili alifunika nyuso zao, kwa mawili walifunikamiguu yao na kwa mawili waliruka. Wakaitana kila mmoja na mwenzake wakisema, “Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ni bwana wa Majeshi; dunia yote imejaa utukufu wake; kwa kilio cha sauti zao misingi ya miwimo ya milango na vizingiti vyake vikatikisika nayo nyumba ikijaa*

*moshi.*

*Ndipo niliposema, "Ole wangu! Ikiwa maana nimepotea! Kwa sababu miminimtu mwenye midomo michafu, nami ninakaa kati ya watu wenye midomo michafu; mbona macho yangu yamemwona mfalme,BWANA wa majeshi? Kisha mmoja wa masefarayo wala akaruka karibu nami mkononi mwake akiwa na kaa la moto, ambalo alikuwa amelitwaa kwa makoleo toka juu ya madhabahu. Kwa hilo akaniguza kinywa changu na kuniambia, "tazama, hili lime-kuguza midomo yako, na uovu wako umeon-dolewa, na dhambi yako imefunikwa."*

*Kisha nikasikia sauti ya bwana ikisema, "nimtume nani? Na atakayekuja kwa ajili yetu?" ndipo nikasema, "mimi nipo hapa, nitume mimi."* Sio kujitafakari ndiyo kul;imfanya Isaya kujiona dhambi zake bali ni kuwa kwake pa mbele za mungu. Alikuwa katika nuru. Hangeweza ku-jinyamazia kwa dhambi hiyo; pia hangeweza ku-jificxha uso wa Mungu. Punde tu alipokiri *yangu yamemwona mfalme,BWANA wa majeshi? Kisha mmoja wa masefarayo wala akaruka karibu nami mkononi mwake akiwa na kaa la moto, ambalo alikuwa amelitwaa kwa makoleo toka juu ya madhabahu. Kwa hilo akaniguza kinywa changu na kuniambia, "tazama, hili lime-kuguza midomo yako, na uovu wako umeon-dolewa, na dhambi yako imefunikwa."*

*Kisha nikasikia sauti ya bwana ikisema, "nimtume nani? Na atakayekuja kwa ajili yetu?" ndipo nikasema, "mimi nipo hapa, nitume mimi."*

Sio kujitafakaria ndiko kulimfanya "Isaya" kujiona dhambi zake bali ni kule kuwa kwake pa mbele za mungu. Alikuwa katika nuru. Hangeweza kujinyamazia kwa dhambi hiyo; pia hangeweza kujificxha uso wa Mungu. Punde tu alipokiri dhambi zakealipata kusamehewa. Baada ya yeye ksamehawa alikuwa tayari kutii.

Waweza kusema ya kwamba haujawahi kusamehewakwa haraka jinsi hii. Labda umehisi hivyo kwa ajili ya mshtaki badala ya mhakimu-asafishaye. Mshtaki hataki mtu yeyote kusame-hewa.

**Kutembea nuruni.**

Wakati mwingine utakapojikuta unanaswa na kujitafakari, ukatae kabisa kitendo hiki. Badala yake, njoo kwa nuru. Kivipi? Kwa komba maombi yapatikanayo katika Zaburi 139:23-24. "Ee Mungu unichunguze, uje moyo wangu uni-jaribu, uyajue mawazo yangu.;Uone kama iko njia ilitayo majuto ndani yangu ukaniongoze katika njia ya milele."

"Tazama juu,sio ndani.Haustahili uitafute dhambi," Mungu " sio ndani "kujitafakaria". Utapata dhambi kukoma kwa haraka sana na kuandamana ,ni suluhisho ikiwa utamgeukia Mungu na ule ukamilifu wa kazi ya Yesu Kristo.

Dhambi iliyosamehewa sio sawa na dhambi iliyofichwa. Kujitafakaria hutafuta kui-kumbukia ile dhambi ya zamani kwa kindani zaidi na kuonekana kuhofia wakati ujao. Paulo alisema, "nikiyasahau  yaliyo nyuma, nikiyachu-chumai yaliyo mbele,nakaza mwendo nifikilie mede ya dhawabu ya mwito mkuu wa Mungu nikitazama mbinguni katika kristo yesu." Yesu alisema, "basi msisumbukie ya kesho kwa kuwa kesho itajisumbukia yenyewe. Yatosha siku kwa sumbuko lake yenyewe." Wafilipi 3:13-14, Mth 6:34. Kusahau  yaliyopita sio kule kushinda dhambi;ni ikiwa tu ya kale yatasamehewa.

Kutembea katika nuru ni *kitendo hivi-sasa.* Haidumu katika wakati uliyopita na wakati ujao. Husikia mhukumu sio mshtaki. Hupokea usafisho na kukubali kwa kutii.

**MWONGOZO WA SOMO: Kujitafakaria**

*Ee Mungu, unichunguze, uujue moyo wangu, inijaribu na uyajue mawazo yangu. Uone kama iko njia yeyote ya majuto ndani yangu, ukaniongoze katika njia ya milele. (Zaburi 139:23-24).*

**Maswali ya Kujadiliana.**

1. Kujitafakaria ni nini?
2. Orodhesha hatari za kujitafakaria.
   *Chanzo cha mvuto utokanao na tendo la tabia hii sio cha furaha. Kisababu chake ni cha huzuni.*
3. Shauri la pili kwa kujitafakaria ni lipi? (Yohana 1:5-10 na Yakobo 1:17)
   Na hii ndiyo habari tuliyoisikia kwake na kuihubiri kwenu; Munguni nuru na hamna giza lolote ndani mwake kamwe. (1 Yohana 1:5)
4. Ni kwa jinsi gani nuru itokayo kwa Mungu inatofautiana na nuru itokanayo na kujitfakaria?
5. Ni jinsi gani Daudi anajitafuta uovu maishani mwake? (Zaburi 139:23-24).

**Hatua Ifuatayo: Kuitikia Neno la Mungu.**

*Angaza* jinsi wewe umekabiliana na majanga ambayo ulitendewa au umeyatenda hapo zamani na unaaibika kwa hayo. Mpelekee BWANA dhambi hii ya vivuli vya mifupa. Omba msamaha ukijuwa kwamba ni wa hakika na kamili kwa sababu damu ya Yesu husafisha mfululizo bila kukoma.*Kuitikia* kwa kutembea katika nuru, ikikuruhusu nia yote kristo aliyonayo kwako.

*Ndugu, sijidhanii nafsi yangu kwamba nimekwisha kushika; ila natenda neno moja tu; niki yasahau yaliyo nyuma nikiyachuchumilia yaliyo mbele.(Wafilipi 3:13)*

# MAHUSIANO NA WAZAZI

*Jim Williamson*

Kwa mambo mengi ambayo mimi huzungumzia kila mara, ni mawili ambayo yamepokelewa na kupendwa kwa wito wa hali ya juu sana,na kuzalisha tunda zuri la maombi kutoka kwa vijana sawia na wazee.

La kwanza ni "Jinsi ya kuwa Huru kutoka kwa uchungu" na la pili "Mahusiano ya wazazi".Sasa hivi nimeketi chumbani mwa kusomea, sebule la barabara makaazi Illinois, kwa chuo kikuu cha Illinois. Wiki moja imepita, niliongoza karakana kule Urbana '93, kuhusu "mahusiano na wazazi."Ni wanafunzi kama 50 tu waliohudhuria, (baraza mbili). Kwa ule mshtuko na ugumu wa roho, na upingamizi na kushindwa kuweka fundsho hili kueleweka vema, ulionekana kwa kutiririkwa na machozi, kwa changizo na mazungumzo,na maswali yaliyofatia. Kwa sababu hii imenifanya kuwa hapa kuyanakili chini.

Kwanza ningependa kuvuta wazo lako kwa mambo mawili katika agano la kale. Mwanzo nitachangia kuyahusu, baadaye nitatoa shauri kuyahusisha maandiko yafuatayo katika maisha yako.

*Usijifanyie sanamu ya kuchonga, mfano wa kitu chochote kilicho mbinguni au chini duniani, kilicho majini chini ya nchi. Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi ni BWANA. Mungu wako ni Mungu mwenye wivu, na huwapatiliza wana uovu wa baba zao; hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, nami nawarehemu maelfu elfu ya wampendao, na kushika amri zangu. (Kumbukumbu la Torati 5:8-10) Lakini ninyi mwauliza "Kwa nini yule mwana asichukue uovu wa baba yake? Yule mwana atakapofanya yasiyo halali na haki; na kuzishika amri zangu na kuzitenda, hakika ataishi. Roho itendayo dhambi ndiyo itakayo kufa; mwana hatachukua uovu kwa baba yake wala baba hatachukua uovu wa mwanawe haki yake mwenye haki itakuwa juu yake, na uovu wake mwenye uovu utakuwa juu yake. (Ezekieli 18:19-20)*

Tusomapo Kumbukumbu la Torati 5:10 "Nawapatiliza wana uovu wa baba zao; hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukizao" Tunaweza kuyamalizia kwa kusema, haya sio kwa haki ya akili zetu za busara. Hata hivyo katika sura yote ya kumi na nne ya Ezekieli tunaona kwamba watoto hawawekewi shutuma ya dhambi za baba zao. Kwa hivyo amri ya pili inatuambia kwamba dhambi hutiririka mteremko wa kilima, na mvuto wa maovu ya mababu zetu hutufuata sisi kwa kuenea na kupitia kwa vizazi kadha wa kadha. Hizi ni habari za kizazi kibaya. Hata hivyo, fungu hili halikomi kwa aya ya 9; linaendelea na " bali nawarehemu maelfu elfu ya wanipendao na kuzishika amri zangu" Neno hili "maelfu elfu" kwa hakika ni "maelfu ya vizazi" Kwa uangalifu wa vizazi vitatu au vinne. Twajuaje ni "vizazi maelfu elfu"? Ni kwa sababu mbili. Kwanza ni njia ya pekee ifanyayo aya hii kuwa ya busara, pili tunapata taarifa amini kwa tendo hilo kwa sura mbili za baadaye.

*Basi jueni ya kuwa BWANA Mungu wenu ndiye Mungu; Mungu mwaminifu ashikaye agano lake na rehema zake kwa wampendao na kushika amri zake hata vizazi elfu. (Kumbukumbu la Torati 7:9)*

Kwa Mungu maovu na chuki husababisha kurudi nyuma kwa vizazi vitatu au vinne na upendo na kule kutii kwa Mungu huleta kuinuliwa zaidi kwa vizazi maelfu.

Mara nyingi nimeyasikia yafuatayo, "Nilikuwa nimekata kauli sitakuwa baba wa aina hii (au mama) mzazi aliye nizaa mimi. Nitakuwa mkristo na pia niowe mkristo na niifanye kuwa nyoofu. Niliweza kuwa mkristo na pia nikaowa mkristo na ninaifanya kuwa mbaya, kama vile wazazi wangu. Niko katika kizazi cha pili chenye uvumi mbaya; nitaendelea tu kuvingoja vizazi vingine viwili vyenye uvumi mbaya kabla hakujatokea uwezekano wa kubadili mwenendo huu?" La! hasha, haustahili kungoja, lakini pasipokubadili uhusiano wako na wazazi wako na mababu wako, itabidi uongojee vizazi vingine viwili. Kuwa mkristo na kuhubiria wazazi wako injili hakubadili uhusino wenu. Wakristo wengi hudhania pakiwa na wazazi pale nyumbani ni mjawapo ya mazingira ambayo hasira yao inakubalika na hapo ndipo uhusiano huaribika.

Karibu miaka 400 kabla kuzaliwa kwa kristo, Nabii Malaki alipeana unabii wa sharti la kukana. Linapatikana katika mafungu mawili ya mwisho katika agano la kale.

*Angalieni nitawapelekee Eliya nabii kabla haijaja siku ile ya BWANA iliyo kuu na kuogofya naye ataigeuza mioyo ya babu*

*iwaelekee baba zao, ili nisije nikaipiga duni kwa laana. (Malachi 4:5-6)*

Malaika Gabrieli amenena sehemu ya unabii huu katika Luka 1:17

*Naye atatangulia mbele zake katika roho ya Eliya na nguvu zake ili kuigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto na kuwatitia wasiwasi akili za wenye haki na kumwekea Bwana tayari watu waliotengenezwa.*

Elewa ili kuzuia laana kutokea lazima mioyo ibaliwe pande zote. Ingawaje mifano yangu mingi huzungumzia kuhusu watoto ilhali kinaga ubaga ni kwa wazazi kuhusu uhusiano wao na wazazi wao wenyewe. Kama wewe ni mzazi mkristo badili moyo wako uelekeze kwa wazazi wako na hali kadhalika uelekeze kwa watoto wako.

Sasa hivi tunatazamia mfano wa pili katika amri kumi za Mungu ambayo tunasoma kuhusu vizazi

*Waheshimu baba yako na mama yako kama BWANA Mungu wako alivyokuamuru siku zako zipate kuzidi nawe ufanikiwe katika nchi upewayo na BWANA Mungu wako(Kumb 5:16)*

Yaliyo na umuhimu hapa ni;1) Mpende Mungu (Kumb 5:9) 2)Mtii Mungu (Kumb 5:9) 3) Waheshimu Wazazi (Kum 5:16) 4)Elekeza mioyo yenu kwa baba yenu (Mal 4:5,6)

Kwa sababu hatujazitii aya hizi mbili katika amri kumi za Mungu, tunaeza kuwa katika ahadi ya kizazi cha tatu na cha nne, hatutaishi miaka mingi duniani (Waef 6:1). Nchi iko katika hatari ya kuchomwa kwa laana. Fungu la Malaki lina wito wa kutubu ili kugeuza mioyo yetu.

Hivi sasa nitawapa mashauri machache kuhusu unaweza kutubu kwa moyo ambako 1)Kuta zuia laana 2)Kuleta kuishi siku nyingi na 3) Kugeuza kizazi cha tatu na cha nne chenye kuzungukwa na habari mbaya hadi vizazi maelfu elfu yenye habari njema.

Kwanza ili kubadilika, kuna mambo machache yenye umuhimu sana, lakini hayo tu hayatoshi kwa kutubu kwa kweli. Ingawaje ni umuhimu kwa kutubu hayo pekee hayatoi jukumu la moja kwa moja kuzuia laana.

1. Uwe mkristo, “Ni vigumu sana kumpenda na kumtii kristo bila kuongoka kwa kristo.”
2. 2. Oa mkristo, “bila ya ndoa ya kikristo hauna uhakika wa wewe kuwa na watoto wa kikiristo.”
3. Dumu katika ndoa, “ Kwa wale waliokwisha kuoana na waagiza ;………Mke asiachane na mumewe” (1 Wak 7:10-11.

Bila haya mashauri matatu kuna matarajio ya wingi wa vizazi vibaya. Hata hivyo, licha ya vizazi vibaya ,vingali tu vyaweza kutokea. Kwa nini? Kwa vizazi vyenu vya kwanza, vingali vinawadhuru pamoja na watoto wenu. Kuacha baba yako na mama yako na kuambatana na mke wako haimanishi kwamba umegeuzia baba yako moyo wako. Kitambo ifanyike hivyo utakuwa unadai kizazi kingine chenye habari mbaya. Hauwezi kutarajia kuwa mume mzuri au baba mzuri ikiwa haujamgeuzia baba yako moyo.

Kwa kumgeuzia baba yako moyo yakupasa asili nne za dharura. Kumhubiria injili sio mojawapo ya hizo; na usifanye hivyo kwa sababu utagandamiza amri yake juu yako. Badala yake waweza kumwandikia waraka ambao unaweza kumzungumzia kila moja ya asili hizi. Ninakusihi kujaza asili moja katika aya moja kama ifuatavyo

1.Ikiwa umekiri kwa Mungu maasiyako uliyowafanyia baba na mama yako hapo awali; basi vilevile yakiri vivyo hivyo kwa baba yako mzazi bila vikwazo au vijisababu.

2.Katika waraka huu mweleze baba yako jinsi unavyomheshimu. Kama haumheshimu bila shaka hauwezi kumwandikia barua hii bila unafiki ndani mwake. Lakini ni lazima uiandike. Kwa jinsi gani? Kwanza ni kwa Mungu kwa kutomheshimu baba yako. “ Kwa nini nifanye hivi?” Waweza kuuliza. “ Kwa sababu hajaupokea ujira wake.” Maandiko yanasema, “Waheshimu baba na mama yako.” Hayasemi ya kwamba, “Ikiwa tu watahitaji heshima.” Baba yako anaheshimika kwa sababu yeye ni baba yako. Umepewa amri kumheshimu bila pingamizi lolote kufanya hivyo. Ikiwa hautamheshimu basi umetenda dhambi.

Na halikadhalika hauna budi kufanya hivyo kwa mama yako. Dhambi inaweza kusamehewa na kuhitajika kutubu. Baada ya kukiri dhambi ya kutoheshimu au kutokuwa na heshima kwa babako na una uhakika umesamehewa, basi chagua kumheshimu. Unaweza kuuliza “Kwa jinsi gani?, Yeye haeshimiki ? Heshima haina uhusiano wowote na kuheshimika kwa mtu umpasaye kumheshimu. Inahusu mstahi na jinsi uhusiano wake wa karibu na ule utiifu kwa Mungu. Hivi sasa ukiwa huru na mwaminifu mwandikie baba yako katika aya hii ya pili jinsi unavyopenda.

3. Katika aya ya tatu mwelezee jinsi unavyompenda na ikiwa humpendi basi urekebike kwanza. Jibu lako laweza kuwa "Hakunipenda kwa hivyo simpendi". Ikiwa hayo ndiyo mashtaka, ni kweli ya kwamba yeye kama baba mzazi angelikupenda ili mwaliko wako ungelikuwa kumpenda yeye. Lakini hatuwezi kurejelea utotoni na kuanza tena. Hata kama inawezekana haimaanishi ya kwamba baba yako atabadilika na kuyafanya tofauti mara ya pili. Tunakabiliana na shida kuanzia penye tumefikia lakini sio penye tunastahili tuwe. Sasa wewe ni mtu mzima nawe kama mkristo una haki zote bila kuzuliwa kupenda na kusamehe. Ikiwa hauna haki hii kuna uwezekano wa kweli kwamba wewe si mkristo. Kama mkristo, unaweza kukiri kwa niaba ya babako kwa Mungu, kwa kutokuwa na upendo. Je ni dhambi? Ndio ni dhambi. Ni kutotii amri ya Mungu.Tumeamriwa kuwapenda jirani wetu na adui zetu pia.Ikiwa unaona baba yako hawezi kuwa mmoja wapo wa vikundi hivi basi unastahili kuchunguza dhamana ya pendo halisi la uhusiano halisi kuwa na kutii na pendo kulingana na Bibilia.

Baada ya wewe kukiri na kusamehewa basi chagua kumpenda babako. Upendo huu unahitaji vitendo. Kwa hivyo muelezee katika aya hii ifatuayo.

4. Aya hii ndiyo nafasi yako ya kumtolea shukrni za kumsifu. Ikiwa hauna shukrani kama vile heshima na pendo basi wewe ndiye utakuwa mwenye kosa, sio yeye. Njia ni ile ile tu. Ukiri kwa Mungu kutoshukuru kwako, ukishasamehewa basi mwonyeeshe babako shukrani zako kwake.

Jinsia hizi nne ni za umuhimu sana na zinahitajika.

Yafuatayo ni mashauri mawili yaelezeayo zaidi kuhusu heshima.

1. Muulize babako akuandikie au akusimulie hadithi fupi kuhusu maisha yake. Kuna uwezekano asifanye hivyo, lakini atafurahia kuna una haja ya kutaka kujua jambo kumhusu.
**2.** Kwa jumla, mwulize akupe ushauri na mwongozo kuhusu mambo Fulani yanayokusumbua maishani.. hii ni sehemu moja ya heshima.

Pia mwandikie mama yako barua kama hii lakini yenye badiliko moja. Aya ya kwanza itaonyesha pendo lako kwake na ya pili itamzungumzia kuhusu heshima uliyo nayo kwake. Katika maumbile yote ya jamaa ya mwanadamu, pendo na heshima inahitajika kutoka pande zote. Kati ya hayo mawili mwanamke anahitaji pendo zaidi kuliko heshima, na mwanamume anahitaji heshima zaidi kuliko pendo. Hata hivyo, kila upande unahitaji yote mawili na hakuhitaji kuyapata ndiposa uyapokee.

Waraka huu unastahili ufuatiwe na maelezo ya aina nyingine kama, kukumbatia na vitendo vingine vya asili. (k m, kusalimia; mikono iwe moto, imara na kwa nguvu.)

Barua hii, yaweza kufuatiwa na uelezi mradi usiwe wa kushirikisha vijisababu na lawama. Hapa kuna changizo; "Baba, ninajua unanipenda sana. Haujakuwa ukinionyesha upendo wako kamili, na kwa hivyo tangu utoto nimekuwa nikiwaza hauna pendo kwangu. Hata sasa imenibidi kulichukua kwa imani. Na ikwa ulishangazwa ni kwa nini nilikuwa mvulana mtukutu tangu niwe katika shule dogo bora ya msingi hadi chuo kikuu, nadhani nilikuwa natafuta pendo la kiume. Bila shaka sikulipata. Nilikuwa ninanyimwa. Na hivi sasa unashangaa kwa barua yangu niliyokuandikia na makumbatio yote unayoyapata kutoka kwangu, ninapokuja hapo kukutembelea. Ingawaje hivi sasa nina mume na watoto. Baba yangu ningali ninakuhitaji na wewe pia unanihitaji. Na ndiposa niko hapa kukukumbatia wewe. Niliwazia niwe wa kwanza kukupa upendo. Ninakupa ili niweze kulipokea. Tumia mfano huu ili ukufae wewe."

Wakati wazazi wako watapokea barua hizi mbili, kuna uwezekano mambo kadhaa kutendeka;

1. barua hii itasomwa zaidi ya mara moja.
2. haitatupiliwa mbali.
3. utapokea aina fulani ya jibu unalolipenda sana kulisikia.

Kama hautapokea jibu, usione kuwa umefanya jambo baya. Uwe mvumilivu na uzidi kumpa huo upendo. Tamaduni zingine hazina mvuto wa aina hii kuonyesha tabia yao, haswa wenye hasira. (km, wakaazi wa ulaya kaskazini). Wonyesha wa aina hii, kutoka kwako, waweza kuwatia wazazi wako wasi wasi. Lakini wangali wanahitaji kupokea uonyesho huu wa upendo hata kama hawajui jinsi ya kuurudisha.

Mtu mmoja, katika miaka yake ya hamsini mwisho mwisho, aliandikia babake barua ya aina hii. Mamake akajibu, "nimeoleka kwa baba yako miaka sitini sasa. Hii ndiyo mara yangu ya

kwanza katika ndoa yetu kuona machozi machoni mwake, mara tu aliposoma barua yako."

Mapema miaka ya 1980, tuliweka shule ya kiangazi ya utendaji wa kikristo kwa **J**umba la **D**elta **K**ule **C**huo **K**ikuu cha Idaho. Wanafunzi kama 40 waliudhuria. Mojawapo ya somo lililofundiswa ni heshima kwa wazazi. Lifuatalo ni funzo lingine kama hilo liloingia katika darasa la kibiblia la adhuhuri kule chuo kikuu cha Washington state,ambapo nilirudia kufundisha somo hili tena. Mwanafunzi mmoja akazungumza kwa sauti, alituhadithia Haiti ifuatayo;

" Nilijifunza somo hili kiangazi kilichopita katika lile jumba la Delta. Nilipokuwa na umri wa miaka kumi na sita, babangu alinitimua nyumbani na kuniambia niende kabisa, hataki kuniona tena. Nilipata kumwondokea pale nyumbani. Baadaye nikawa mkristo na nikaoleka kwa mkristo. Na sasa mimi ni mwanafunzi mhitimu katika chuo kikuu cha WSU. Kwa muda mrefu sijaonana na babangu. Wazazi wangu walikuwa wamefikia ukingoni na kutalakiana, waliishi katika vyumba tofauti vya kulala pale nyumbani, (katika makao moja kule muungano wa nchi tambarare kuu). Nilipopata habari hizi, niliwaandikia barua mbili: moja kwa babangu na nyingine kwa mamangu. Ilinichukua siku kadhaa kuandika kila moja ya barua hizi, na wazazi wangu walikuwa nyumbani wote. Kuona kwamba barua zote zilikuwa zimeanwanishwa tofauti tofauti, mamangu alichukua barua yake na kuingia chumbani mwake, vile vile na babangu. Baada ya kila mmoja kumaliza kusoma barua yake, walibadilishana barua zao na kila mtu akarudi katika chumba chake na kusoma. Walipotoka vyumbani mwao, babangu alikuwa na machozi machoni mwake na akasema, "Ninapaa kwenda Pullman kumwona kijanangu. Nimekuwa nikionana babangu tangu kiangazi kilichopita na ndoa ya wazazi wangu imeokoka."

Kuna shida mbili, shida ya moyo na shida ya utendaji. La kwanza kabisa ni shida ya moyo. Kutokuwa kwako na upendo, kutoheshimu kwako,kutoshukuru kwako, kunastahili kuwe na uangalifu wa kutubu kwa Mungu. Kuandika tu barua bila msamaha wa Mungu inamaanisha barua yako sio aminifu ni ya unafiki.

Waweza kujikuta kukawia sana ikiwa utamngoja babako akugeukie kwanza. Hautaweza kuvumilia kungoja.

Baada ya wewe kutakaswa, basi andika barua zile. Halafu endelea kuandika barua, kupiga simu, na kuwatembelea, ukionyesha heshima, upendo na shukrani.

Ukiyafanya mambo haya bila shaka utabadilika. Utakuwa mume mzuri, kijana na baba na pia mke mwema, msichana na pia mama mzuri. Upendo wako na kutii kutakuongoza kuwa na upendo kwa vizazi elfu.

**MWONGOZO WA SOMO: Mahusiano na Wazazi.**

*Usifanye sanamu ya kuchonga, mfano wa kitu cho chote kilicho juu mbinguni au kilicho chini duniani, au kilicho majini chini ya nchi. Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi ni BWANA Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu, nawapatiliza wana uovu wa baba zao; hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao, na kuzishika amri zangu.(kumbukumbu la torati 5:8-10)*

**Maswali ya Kujadiliana**

1. Kumbukumbu ya torati 5:8-10 yatuambiaje kuhusu baba zetu?
2. Ni ahadi gani Mungu anawapa wale wampendao na kutii amri zake? (kumbukumbu ya torati 5:10)
3. Ni nini kinatupasa kufanya ili kuzuia *uovu wa baba yetu* kwa kutoambukizwa kizazi kimoja hadi kingine.(mal 4:5-6, luka 1:17)

   *Waheshimu baba na mama yako; kama BWANA Mungu wako, alivyokuamuru, siku zako zipate kuzidi, nawe upate kufanikiwa katika nchi upewayo na BWANA, Mungu wako. (kumbukumbu ya torati 5:16)*
4. Ni nini kinachotuwezesha sisi kubadili mioyo yetu na kugeukia baba zetu na mama? (kumbukumbu ya torati 5:9, 5:16, na malachi 4:5-6)
5. Ni hatua gani twaweza kuzifuata ili kujiumbia moyo wa toba na kugeuza mwenendo mbaya wa kizazi cha tatu na cha nne kuwa chenye mwenendo mwema kwa vizazi elfu?

**Hatua ifuatayo: Kuitikia Neon la Mungu.**

*Angaza* uchungu na hasira ambayo umeshindwa kujiondolea wewe mwenyewe. *Omba* Mungu akuwezeshe kuachana na uchungu, kuacha hasira na hisia za kutokuwa haki kwake. *Itikia* kwa kukiri, uruhusu moyo wako kusafishwa na kuwa upya. Halafu chukua hatua ya kuandika barua ukizifuata mbinu nne zenye zimeorodheswa hapo.

*Basi jueni ya kuwa BWANA, Mungu wenu, ndiye Mungu; Mungu mwaminifu, ashikaye agano lake na rehema zake kwao wampendao, na kushika amri zake hata vizazi elfu.*

# UPENDO KAMILIFU

Jim Wilson.

Kuna maagizo kuhusu upendo utokao kwa Mungu. Maagizo haya yawapasa kutimiziwa wake, wandugu, majirani, wageni na pia maadui. Upendo huu ni **ule** ambao Mungu alikuwa nao kwetu sisi alipomtoa Yesu kristo afe kwa ajili yetu. Ni dhabihu itokayo kwa tendo lile la kwanza, **Upaji**. Imebuniwa iwe na nguvu. Ilitenda kazi kwa wokovu wetu. Upendo unahitaji chombo na utendaji. " Kwa maana jinsi hii Mungu alipenda **Ulimwengu,** hata **akamtoa………."** (Yohana 3:16). **Ulimwengu** ulikuwa chombo cha upendo na **upaji** ulikuwa uonyesho wa upendo. Upendo huu haukua zembe au tosha au " nusura kutosha". Ulikuwa mkamilifu na zaidi kuliko utoshelevu wa maovu yote na watenda dhambi katika dunia hii. "Lakini dhambi ilipozidi, neema **ilikuwa nyingi zaidi ………"** (warumi 5:20).

Kwa kutii maagizo haya ya upendo, inatupasa kupenda jinsi Mungu alivyopenda. Huo hauna masharti - bila usaza au uzembe. Inatupasa **tuwe** na **kumjalia** muhitaji pendo; upendo mwingi sana ili hitaji lake la upendo litoshelezwe. Waweza kuwazia kwamba <u>hilo</u> haliwezekani. Unamshindisha mtu huyu kumpa pendo mpaka kumpenda yeye ni kama kudondosha maji kwenye tundu la panya. Na wakati huo unazidi kusongwa kwako ili apate pendo zaidi. Umeamini kwamba utaishiwa na pendo kabla aliyesongwa na pendo kumridhisha kwalo. Hili litadhihirika waziwazi ikiwa wewe utamhesabia yeye akurudishe pendo ili kuafikia mahitaji **yako.** Bali kama utajazwa upya kwa Roho Mtakatifu, hautakaukiwa upendo kamwe. Hebu na sisi tutumie msingi huu kuwalea watoto wetu.

Kuna shida ya utofauti mwingi katika kuwalea watoto ambapo kuna hitaji la kufahamu na kuzingatia misingi ya kibibilia. Hapa kwanza kuna baadhi ya shida hizi:

1. Kutokuwa na kutii.
2. Adabu inayofaa kwa kutotii.
3. Mafundisho na mwongozo unaofaa.
4. Ushindani wa kijicho na wivu.
5. Usikizi-kupata hila kama vile manung'uniko, kulialia na hamaki.
6. Dalili za kutokuwa salama kama vile kupiga yowe, chunjue, kuzidi uzani kukwaruza, kugonga, kuuma, kubagua mwili na kupapasa.

Kila somo linahitaji kitabu, hatahivyo, vitabu hivyo vimeandikwa kwa kila kimoja masomo haya. Kuna uwezekano mmeshasoma vitabu kama hivi na kufanyisha kazi yale mliyoyasoma katika vitabu hivi, na kwa wengine wenu matokeo hayakuwa mazuri. Ni rahisi wewe kuweka uamuzi wa haraka kwamba kitabu hiki ni kibaya. Kitabu kinaweza kuwa sawa lakini jinsi ulivyoyaweka kwa vitendo ni kinyume. Je, kulitokea jambo gain?.

Hapa kuna mwongozo uliotajwa hapo awali. Nitauita **upendo kamilifu**. Upendo kamilifu ni tofauti na upendo toshelezi, wakati wa sifa au wakati wa cheo. Unajumlisha mambo haya mawili ya mwisho na kwa **uangalifu wote.** Kamilifu ni kumaanisha kufikia upeo. Myeyusho kamili ni kumaanisha kiyeyusho hakiwezi kuzidisha kuyeyusha. Kwa mfano ukiendelea kuongeza sukari na kugoroga kwenye glasi ya maji, muda si muda maji yatajaa myeyusho wa sukari, ikimaanisha kwamba sukari haiwezi kuyeyuka tena katika huo myeyusho. Baada ya ncha ya myeyusho, sukari yeyote itakayo ongezwa itazama chini ya glasi.

Yale maji **hayawezi** kuyeyusha tena. Na hivyo ndivyo ilivyo sawa na upendo. **Inawezekana** kujaza mtu upendo ili upendo mwingine ukose kupokelewa. Sio ati umekataliwa bali, hauhitajiki kwa wakati huu.

Kwa miaka nimekuwa nikiwauliza wasikilizaji wangu kuonyesha kwa ishara ya mkono, wanaodhania wazazi wao wanawapenda. Zaidi ya asilia 95% ilikuwa juu. Haikuwa asili mia 100% lakini kila mara ilikuwa juu sana. Badaye nikauliza swali kwa wale waliokuwa wamebeba mikono yao juu……… "Je, mnadhani kwamba wazazi wenu waliwaonyesha upendo huu kwa utoshelevu? Ni nusu ya mikono iliyobaki juu. Na swali la tatu lilikuwa; "kwa ninyi mnaodhania wazazi wenu waliwaonyesha upendo toshelevu, je, mngetumia uonyesho bora zaidi wa upendo?". Mikono yote ilibaki juu.

1. Hakuna upendo
2. Baadhi ya Upendo
3. Upendo tosha
4. Pia **upendo zaidi** unahitajika.

Hakuna yeyote aliyedhania alipokea upendo kadiri kutoka kwa wazazi wake. Na watoto wao vile vile wangeliulizwa, wangelisema jambo hili hili kuhusu wao.

Ni nini matokeo ya kutokuwa na upendo kadiri? Kutotii ndio ulinganifu wa wazi kwa kukosa up-

endo. Hata kama nidhamu itakua kikamilifu kwa kutotii, haifaidi mtu kitu iwapo hatapewa upendo kadiri. Hudhania hivi, "wakati wa mwisho mimi kupata kuhudumiwa mahali hapa, ni ule nilizabwa kofi na ikawa mwisho. "Ukaidi wake unakuwa njia ya pekee ili apokelewe. Kwa hivyo malezi na mafundisho yako hayakuwa na manufaa ikiwa humpi mtotoako upendo kadiri.

Ushindani wa kijicho, ubishi, ubinafsi na wivu ni maneno yaliyo kinyume na upendo kwa watoto wako. Kwa hivyo wakati watoto wote wanakamilishiwa upendo, kutakuwa na kiasi au kutokuwa na ushinani kabisa, mizozano na vita. Kuongezeka kwa upendo hupungua, malalamiko, ukaidi, uivu hamaki na vilio kupungua. Pia pakiwa upendo mwingi, ndivyo mtoto atazidi kuwa Mkristo.

"Au waudharau wingi wa upole wake na ustahimilifu wake, uvumilivu wake, usijue ya kuwa upole wa Mungu wakuvuta kutubu?. (Warumi 2:4).

Lengo la Mungu kutuelekeza sisi tobani ilikuwa kutumwagia ule upole na kutuonyesha ustahimilifu na subira hata wakati tulikuwa watenda dhambi. Ni mangapi zaidi ya hayo tunastahili kuwafanyia watoto wetu.

Shida zetu ni nini?. Sisi **hatutaki kutoa** ukumbatio na mapokoleo kwa mnung'unikaji. Hatutaki kuonyesha tabia mbaya. Hivi ni kweli, walakin kufanya hivi haimashi tabia mbaya. Bali ni kuponya jiraha. Kufanya hivi haimaanishi tunalazimishwa na mtoto bali ni haki yao kupokelewa. Kuhisi kwake ni kwa kweli zaidi kuliko kwako. "Mnung'unikaji" anahitaji kupokelewa pokeleo la pendo. Tutampa mtoto mchanga mapokeleo anapolia. Kunaweza kuwa hakuna jambo lolote libaya; yeye hana njaa, hajajikojolea, mchafu wala mgonjwa; nikuhitaji tu pendo. Na wakati mtoto anafikia umri wa miaka mbili, tatu, nne au kumi na aitishe mapokelewa hatuko tayari kuyapeana. Hatufikirii mtoto huyu anauhitaji. Unisadiki, ataliuliza,na analihitaji. **Atakapokamilishiwa** hataliuliza tena.

[Kwa upande mwingine kuna watoto ambao huhitaji kupokelewa lakini **hawawezi kuliuliza**. Wanalihitaji na hata kulipokea kwa kiwango kidogo sana kuliko *mhitaji.* Kwa sababu hawakuliuliza untadhani wametosheka.]

Shida yetu ni kwamba huwa tunakata tamaa ya "Kupeana" kabla mtoto hajakata tamaa ya kuhitaji. Huwa tunawazia **hataacha** kuhitaji mapokeleo yetu, kwa hivyo sisi hujiepusha na hitaji lao kabla wakati wake kufika. Na tungeendelea kupeana mapokeleo haya tungeligundua mtoto wetu kutosheleshwa. Mtoto atapata kujazika na baadaye kuwa salama na hitaji lake litakuwa dogo sana siku za usoni. Usalama huu una umuhimu sana katika nidhamu ya mtoto wako.

Miaka mingi iliyopita kulikuwa na kijana mdogo aliyekuwa na chunjua wa mkono kwa kitanga chake cha kushoto.

Nikikumbuka walikuwa kumi na nne kwa jumla. Alikuwa nazo kwa miezi nyingi. Siku moja baba yake akamuuliza. "Jonny, ungependa nikuombee kwa Mungu akuondolee hawa chunjua wako?" Jonny akajibu, "hapana! hawa ni rafiki zangu, mimi hucheza nao". Baba yake alijua chunjua hawa ni dhibitisho la kijanake kutokuwa salama, na chanzo cha yeye kutokuwa salama chatoka kwa yeye mwenyewe kwa kutompa mtotoake mapokeo ya pendo la kutosha. Babake aliweza kufanya uamuzi na kumfatilia kwa kumpa mapokeo ya upendo mwingi. Chunjua hawa waliweza kupotea kwa muda mfupi sana.

Miaka nyingi iliyopita nilikuwa na uhusiano wa karibu na familia moja changa sana, yenye watoto wa nne wavulana kwenye shule ya Msingi, wenye umri wa mika moja, mbili, mitatu na nne. Siku moja wazazi hawa walinitembelea kuhusu kijana wao mkubwa. Alikuwa na shida mbili kubwa zilizoonekana kushindikana kurekebisha.

1. Kila mara alikuwa akishinda mchana akipiga nduguze wadogo .Kila siku alirekebishwa kwa kukaripiwa, kuzabwa kofi au yote mawili.
2. Alimchipua ngozi ya sehemu mbalimbali ya uso wake ambako kulimtia alama nyingi nyekundu ndogo kwa uso wake wote. Alionekana kama ambaye aliye na surua.

Kuzabwa makofi hakukubadili chochote. Swali lao lilikuwa, "Tufanye nini?". Ingawaje nilikawia muda mrefu kuyasema jinsi vile imekuchukua wewe muda kuyasoma haya, majibu yalikua kama ifutavyo;

"Wakati mwingine huyu mkubwa akimpiga yule mdogo, mchukue huyu mkubwa na kumkumbatia".

Jibu lake "Sitaki kulazimisha tabia kama hiyo"
"Usitie shaka ,tayari yeye amepokea ujumbe huu. Sio tu umkumbatie wakati atakapiga nduguye tena, nataka wakati mwengine umkumbatie

mchana mzima. Hajawahi pewa pendo la kutosha tangu kuzaliwa mtoto wa pili na hivi sasa kuna watatu na wanne. Huwa anapokelewa tu anapokuwa mbaya. Kwa hivyo huwa anampiga nduguye mdogo ili apate kupokelewa. Humgwaruwa uso wake kwa sababu hana usalama. Ningekusihi ikiwa utamwagia mapokeleo ya upendo ya kuua, uso wake utakuwa sawa na ataacha kupiga ndugu zake wadogo kwa majuma mawili tu"akasema "Sidhani nitaweza kutenda hilo" "mbona lisiwezekane?" "hata simpendi tena".

Wazazi hawa walikiri dhambi zao kwa kuyatekeleza maagizo haya mara moja. matokeo yaliyokusuwa yalibainika ya kuwa ya kweli. baba na kijanake machachari wa miaka kumi na mbili waliambatana kuja kupata msaada. Kijana huyu amekuwa akkiadhibiwa vikali kwa upotovu wa nidhamu kwa mambo madogomadogo na hakuonyesha kujifunza lolote kwa nidhamu hiyo. Pia kijana alikuwa na wakati mgumu kustahimili uchungu alionao.

Wazazi walimpa kiasi kizuri cha upendo, kumsikiza na muda wa kutosha nab ado kijana hakuweza kubadili wala kutubu licha ya kupigwa kila mara. nikamwambia mzee kwamba hakummimimnia upendo mwingi. Baba kwa ukosefu wa tumaini la mabadiliko, aliumimina kwa vitendo na kupunguza adhabu ya kumrushia maneno makali kwa mambo madogomadogo. Mzee akampeleka kijana kwa matembezi ya kiume kwa bustani la starehe na akamkumbatia mkononi mwake kwa masaa mawili kwenye gari lao na kumgusagusa kila alipomzungumzia. Waliporudi nyumbani mama akagundua mabadiliko katika tabia yake na hitaji la kurekebishwa bila kulazimishwa, hali kadhalika hakutaka kukaa na amani na watoto wengine.

Kwa kuuliza maaswali na majibu kwa miaka mingi, kuna jibu moja tu lililo na msimamo. "Sikusikia babangu akikubali ya kwamba amekosea kwa jambo lolote. Wakati huo mama alijua baba ana kosa;sisi watoto tukajua ana kosa; Mungu pa alijua ana makosa na pia mwenyewe alijijua, lakini hangeweza kukubali kosa". Usemi huu unaweza kuwa wa kweli na wazee wengine wenu, ambao watoto wao sasa hivi ni wazima na wanajitegemea. Unaweza kuwa umesoma jarida hili na kutambua kwamba haujakuwa ukiwapa upendo **kamilifu** kwa vitendo walipokuwa wakikuwa. Wakati huohuo walipitia shida nyingi sana. Wengine wenu mna waototo barubaru wako pale nyumbani nawe na sio wadogo "wakupendeka".

Utafanyaje sasa juu ya jambo hili?. Jambo la kwanza utakiri kwa Mungu matendo yako **yote** maovu kama vile kuadhibu bila kiasi, kumkaripia, kudhihaki, upuuzaji, kupiga yowe, hasira, mapendeleo, ukosefu wa upendo nakadhalika. Ukisha maliza umwandikie barua kila mtoto kumwonyesha jinsi umekiri kwa Mungu. Unaweza kumwambia kuwa umekiri tabia na kumbe matendo yako mabaya kwa Mungu. Unaweza kuyakumbuka baadhi ya makosa yale unaweza kukumbuka. Unaweza kuwaomba wakusamehe mambo yale **yangali** yanawatia uchungu vilevile **wewe** unaweza kuwa ungali unatiwa machungu kwa yale uliyotendewa na babako. Watakapokuambia, **usiwe** na upingamizi bali unyenyekee na kuomba msamaha kwa sikitiko la kiungu. "Huzuni kwa Mungu husababaisha badiliko la moyo lenye kuleta wokovu na hakuna sababu ya kujuta, bali huzuni ya kidunia huleta kifo". (2 wakorintho 7:10). Basi uwaonyeshe upendo kwa mifano **mbalimbali.**

Ikwa watoto wako wangali nawe basi uwatendee vivyohivyo isipokuwa uwaambatanishe wewe mwenyewe binafsi kwa kuongea kwa barua hizi. Barua hizi ni za muhimu kwa sababu
1. Unaweza kuyasikia yote bila ya kusumbuliwa,
2. Barua hii itasomwa mara kwa mara na
3. Barua hii itahifadhiwa kuelezea yote bila matatizo, .

Kumbuka ya kwamba maumbo kutoka pande zote za watoto wanahitaji upendo wa kutosha kutoka pande zote za maumbo ya wazazi. Ikiwa mtatengana basi itakuwa vigumu sana kuwa na upendo mkamilifu. Ingawaje bado ni wa umuhimu sana. Itakuwa kutozaa, ikiwa unashindania huo upendo na utiifu wa watoto wako kwa kushusha chini mpenzi wake ule wa zamani au kupunguza pendo la watoto.

Njia moja iliyo nzuri kati ya njia zote ionyeshayo upendo kwa watoto wake **sio** kwa kupigana na mchumba wako. Hiki ni kisababu kikubwa kiletacho ukosefu wa usalama. Ikiwa wazazi hampatani basi watoto ***wasisikie*** ubishi wenu. Chukua kwamba tayari unatabia hii ya kupigana au kubishanabishana kati yenu mbele ya watoto wenu, basi kiri tabia hii kwa Mungu, alafu kwa mchumba wako, watoto wako kisha mkome vita kati yenu kabisa.

**Tunajua ya kwamba mtoto anazaliwa na hatimaye anaiga mwenendo wa dhambi ya asili.*

*Dhambi hii ya asili ndiyo fikira ya **kwanza** ya kusababisha kutotii kwake. Mabadiliko haya hupatkana kwa kutokiri. Kwa yote baada na kabla ya kuongoka kwake, kutokuwa kwake na upendo* kwake kumesababishwa na kutotii.

**MWONGOZO WA SOMO: Upendo Kamilifu**

*Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.(Yohana 3:16)*

**Maswali ya Kujadiliana;**

1. Orodhesha sababu ambazo zinaweza kumfanya mtu ahisi kwamba amenyimwa upendo.
   *Upendo kamilifu ni tofauti na upendo tosha, yani wakati wa sifa au wakati wa cheo. Ukamilifu inamanisha ya kwamba kilele chake kimefikiwa. Upendo kamilifu ni hitaji la mtu la kuridhishwa pendo kabisa.*
2. Zungumzia hali ambayo wewe uliweza kupata "Upendo kamilifu" au kuonyesha"Upendo kamilifu" kwa mtu mwingine.
3. Ni dalili zipi zioneshazo kutopata upendo wa tosha?.
   *Mungu hutuongoza sisi kutubu, kwa kutumwagia upole, Kutuonyesha sisi unyenyekevu na uvumilivu hata tumtendapo maovu. Na hii ndio tabia ambayo Mungu ametuekea mbele yetu kama wazazi.*
4. Jinsi gani tabia ya Mungu inaweza kuigwa tunapo walea watoto wetu?.
5. Ni hatua zipi tunaweza kufuata kwa kunakili makosa ambayo tumeyatenda?
   *Maana huzuni iliyo kwa jinsi ya Munguhufanya toba liletali wokovu lisilo na majuto; bali huzuni ya dunia hufanya mauti. (2Wakorintho 7:10).*

**Hatua Ifuatayo: Kuitikia Neno la Mungu**

Maovu yasiyokiriwa hurudisha nyuma uhusiano wa karibu na Mungu na wengine maishani mwetu. Lazima tukiri maovu yetu kwa Mungu na kumsihi atusaidie kureke bisha.Mungu anatusihi sisi kuitikia kwa kukiri makosa yetu kwa washikaji wetu.na waoto wetu kwa upole, huruma na moyo mkunjufu. *Iweni wafadhili na wenye huruma ninyi kwa ninyi, mkasameheane kama jinsi katika kristo Mungu aliwasamehe na ninyi.(Waefeso 4:32)*

# NI JINSI GANI MWANAMKE ANAKUWA SALAMA?

**Jim Wilson.**

Mungu alimuumba mwanamke apewe upendo, alindwe, ajukumkiwe na kuwekwa salama. Hata hivyo kwa ajili ya vijisababu vingine, mwanamke huenda haridhiki na kule kupendwa, kulindwa na usalama alio nao.Kila mara ulinzi ni manufaa ya kweli ionekanayo na hisia ya nafsini. Ninachojaribu kuelezea hapa ni kwamba wanawake wengine wamepoteza wazazi wao, waume wao, watoto wao, chakula na mavazi yao. Wako na sababu ya kutokuwa salama kwa ushuhuda wa macho na mtu anaweza kuhisi hana amani. Na wakati mwingine kuna uwezekano ahisi kutokuwa na amani na kuwazia ni jambo gani lipasalo kufanya la lazima ili upate hitaji lako. Hapa kuna mfano;

Chukulia ya kwamba mwanamke anahisi kutokuwa salama, hisia hii inazidi kuwa nzito kiasi cha yeye kudhibitika ya kwamba pia ni la kweli. Hitaji kubwa la mwanamke ni kutaka kuondoa ule upweke.Hudhania ya kwamba mwanamume ndiye atamwondolea.Kwa upande mwingine wazo hili ni kweli.Ingawaje hitaji lake linazidi kuwa kubwa zaidi hata anapata mume ambaye hawezi kumwondolea upweke huo. Hawezi kwa sababu yeye pia yuna upweke na anatafuta mwanamke wa kumwondolea. Jambo hili haliwezekani kati ya watu wawili walio na upweke ambao hauna amani ili kupata hitaji lao wakioana. Hapo ndipo mwanamke anakosa amani kuliko vile alikuwa.Hudhania akipata mtoto,basi atamwondolea upweke aliyonao. Pia kwa upande mwingine wazo hili ni kweli. Wanawake waliumbwa kuwa na watoto. Hata hivyo watoto ni viumbe vyenye mahitaji na kujumuikia. Hapo mwanamke asiye na amani anakuwa sasa na majukumu makubwa kwa mtoto wake kuliko kadri awezavyo kukutana nayo, sana sana panakuwa na ongezeko la watoto. Na hapo wasi wasi umzidi na kukosa amani. Anawazia kuwa na boma zuri lenye zana za kupendeza. Vyombo hivi ni vinahitaji fedha nyingi. Inambidi kufanya kazi kama vile mumewe. Hivi sasa anachoka,hana amani na ni mwenye hofu.Mara anataka mavazi, mziki, marafiki, na labda mume mwingine tofauti.Mumewe naye hana uhuba naye. Alikata tamaa hapo mbele ya mwanzo wa ndoa yao; kwa sababu malengo yake hayakutekelezwa.

Habari hizi nimezipata kutoka kwa wanawake wachache ambao ninawafahamu. Hivi sasa wengine wao wameolewa mara kadhaa, kuongezea na wanaume wengine. Ingawaje wamechelewa, wanangamua ya kuwa mume, watoto, nyumba, mali, na marafiki hawawezi kuwaondolea upweke wao na kuwapa ulinzi kamili wautafutao.

Shida hii inapasa kutatuliwa lakini kwa sababu ya ubinafsi ambao unazuilia kuitatua hivi sasa unaonyeaha kwamba haitatatuliwa kamwe licha ya yeye kumpata mume, watoto, nyumba na mali. Kwanza ni kuondoa ubinafsi. Ubinafsi unageuka kuwa vita vidogo na vigumu nafsini mwake. Vita hivi vidogo na sugu vya ubinafsi, hufanya mtu kuharibika na mwenye kuudhi.

Anastahili kuuponya ubinafsi, kuukiri, kuachana nao na kuutupilia mbali mbele za Mungu. Na hapo atakuwa na furaha ya ajabu, amani na Mungu atamweka huru, pasipo huo atakuwa salama kabisa ndani ya Kristo.

Kama kadri iwezekanavyo kutoa usalama katika dunia hii, hutoka kwa uhusiano wake na baba, mama, kaka, dada na jamii. Kufatia unatokea kwa wandugu na wadada katika Kristo ambao ni wapendwa na wenye kutoa. Utatokea kwa yeye mwenyewe akiwa na upendo na utoaji kwa kila aina ya watu, hata kama huwa hawarudishi huo upendo. Unaweza kutoka kwa mumeo, lakini sio kwa mume mtarajiwa. Ninasema hivi kwa sababu asije akatarajia akiolewa ndipo atapata usalama. Inampasa awe salama hata kabla hajaolewa. Basi hataona kama ni ndoto na uchungu ndani mwake.

Ni jinsi gani mwanamke anakuwa salama?

Ni lazima pia akiri nia aliyo nayo, sio matendo pekee.

Ni lazima kwa neema ya Mungu ampende baba, mama, ndugu na dada zake.

Upendo wake usiwe na mpaka. Imstahili aseme, " nitampenda ikiwa………" pasiwe na "ikiwa".

Upendo huu uambatane na matamushi ya upole, makumbatio, matendo ya kutoa na kusaidia.

Inamstahili aonyeshe upendo huu kwa watu wengi zaidi na zaidi.

Kwa maana upendo wa kristo unatutia nguvu sisi, kwa sababu tunaamini ya kuwa kuna mmoja aliyekufia wote, na kwa hivyo wote wali-

kufa. Na aliwafilia wote, ili walio hai wasiishi tena kwa ajili yake yeye aliyekufa akafufuka kwa ajili yao. (2 Wakorintho 5:14,15)
Muda mwingi wa mwanamke anastahili awe na tabia nzuri ya utakatifu, upendo, upole na kadhalika. Anastahili pia atamani kuwa na familia yenye upendo, watoto wenye upendo, na wajukuu wenye upendo. Anastahili atamani kuwa na "sifa njema, mtumishi mzuri na mwaminifu, na kuwea ndani ya Bwana" mwanamke anastahili awe na mazoea ya kumfikia babake kwa kutoa na kupokea.

Suluhisho linalopeanwa hapa lina dhana ya kwamba mwanamke huyu anayeongolewa tayari ni mkristo, yaani amekwishakumpokea Yesu Kristo, mwana wa Mungu kwa imani kama Bwana na mwokozi. Ametoka katika mauti hadi uzimani. Hili ndilo chanzo cha usalama kwa kila mtu yeyote, waume kwa wake.

**MWONGOZO WA SOMO: Jinsi gani Mwanamke anakuwa Salama:**

*Na Mungu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya kristo yesu. (Wafilipi 4:9).*

**Maswali ya Kujadiliana.**

1. Je, bibilia anasemaje kuhusu kujihisi kuwa salama na amani kilingana na mafungu yafuatayo; kumbukumbu ya torati 33:12,
   zaburi 4:8,
   Methali 29:25,
   1 Yohana 5:18.
2. Je, bibilia ina nini cha kutuambia kuhusu kutosheka?
   Methali 30:15-16,
   Muhubiri 5:10,
   Zaburi 63:5,
   Zaburi 103:5,
   Isaiah 53:11.

*Msitende neno lolote kwa kubishana au kwa majivuno; bali kwa unyenyekevu, kila mtu amhesabu mwenziwe kwa ubora kuliko nafsi yake. (Wafilipi 2:3)*

3. Je, tunawezaje kuondoa ubinafsi ndani mwetu?
4. Ni usalama gani unatupasa kuchukua ili kuhisi salama? (Yakobo 3:13-18)

**Hatua Ifuatayo: Kuitikia Neno la Mungu.**

*Angaza* sehemu katika maisha yako ambapo umekumbwa na hasira ya uchungu na kuwa na tamaa ya ubinafsi ambayo imezuia juhudi yako ya kuwa mwigaji wa kristo.*Omba* hekima ya Uungu na maono ya kukuongoza.*Itikia* kila siku kwa kumtafuta njia zake.

# MUME MWENYE JUKUMU

**Jim Wilson.**

Kama kuna ukosefu mkubwa katika wanaumewaliokomaa, awe mkristo kwa asiye mkristo, ni kule kujiamini. Neno hili ndilo linashikamanisha uaminifu, maadili mema, utakatifu, unyofu na lile hitaji lakuchukua *jukumu.* Tabia hii ya kujiamini ndiyo imezungumziwa hapa. Baada ya mtu kumpokea Kristo, matarajio ni kuwa na dalili za kujumukika. Jukumu ni mojawapo ya sifa ya mtu isiyo na ubinafsi. Kutojali ni mojawapo ya sifa ya mtu aliye na ubinafsi.

Mungu amepea wafalme, waliwali, viongozi, waume na baba majukumu. Mungu ametupa viongozi liwe liwalo au lisiwe tunajumukika kuongoza. Ikiwa hatuingiani na sehemu yeyote katika orodha hii iliyo hapo juu, inatupasa kuwa na jukumu. Ni sehemu ya kuwa mwanaume.

Adamu alikuwa na uzembe alipomwambia Mungu katika Mwanzo3:12, "*huyu mwanamke uliyenipa awe nami ndiye aliyenipa matunda ya mti huo nikala.(NIV=TMK).*

Adamu akaelekeza lawama kwa mwanamke na Mungu. Mungu akajibu katika mwanzo 3:17; *kwa Adamu akamwambi, "kwa kuwa umesikiliza sauti ya mkeo, na ukala kutoka kwa mti ambao nilikuagiza wewe, yakulazimu usile kwa kwa huo, ardhi imelaaniwa kwa ajili yako; kwa uchungu utakula mazao yako siku zote za maisha yako" (NIV ="TMK")*

Kwa jadi, wanaume wamekuwa wakiwalaumu wake zao, watoto, mabwana wao na kila mtu ili hali makosa ni yao wenyewe.

Abrahamu pia alikuwa na uzembe: *Alipokuwa karibu kuingia Misri, akamwambia Sarah mkewe, "najua ya kwamba u mwanamke mzuri wa uso. Wamisri watakapokwona watasema, "huyu ni mkewe" kisha wataniua mimi na wewe watakuacha hai. Tafadhali useme wewe ni ndugu yangu, iwe heri kwangu kwa ajili yako, na nafsi yangu iishi kwa ajili yako" (Mwanzo 12:11-13 NIV="TMK")*

Abrahamu alihofia yeye kuuawa na wamisri ili wampokonye mke wake. Alimsikia mke wake akisema uongo kuwa yeye sio mke wake, bali yeye ni ndugu yake. Farao alimpokea na kumkaribisha vizuri sana na kumfanya kuwa tajiri. Farao na nyumba yake walipatwa na pigo kubwa la ugonjwa kwa sababu alimchukua mke wa Abram na kumfanya mkewe; wakati Farao aligundua, alimrudishia Abram- Sarai na kumfukuza atoke katika nchi yake. Baada ya miaka kama 20-25 hivi, Abram ambaye sasa ni Abrahamu, alirudia kosa lile lile kwa mfalme wa taifa lingine, safari hii yeye mwenyewe alimdanganya badala ya Sarai kumdanganya. Na Abimeleki, mfalme wa Gerari, akamchukua. Mungu akamwambia Abimeleki ya kuwa yeye ni sawa na mfu kwa kumtwaa mke aliye na mume. Basi Mungu akamlinda Sara. Abimeleki hakuwaangamiza. Soma hadithi hii pale mwanzo 20. Uzembe huu uliambukizwa Isaka, mwanawe Abrahamu. Naye pia vile vile alimdanganya mfalme huyu Abimeleki kuhusu Rabeka, mkewe. Makafiri hawa walipatwa na hofu kuu juu ya jambo hili hata kuliko Abrahamu na Isaka. *Wakawa na madhihaka kwa ajili ya ezembe wa waumini (Mwanzo 26). Sara na Rabeka walikuwa na udhaifu na bila hatia*

*Uzembe wa aina hii ni wa kipekee. Ni dhambi ya kubebesha wemngine majukumu haswa kwa wale wadhaifu na labda hawana hatia. Uzembe ni sawa na udanganyifu. Ni kizuizi na njia moja ya kujikinga. Ni uzembe wa kupindukia. Unaonyesha kule kukataa kuwa baba mzazi, kutojali watoto, kulaumu wengine, kupigapiga wake, kutoa maneno ya matusi, kutosaidia, na kutopeana upendo na ulinzi kamili.*

*Wafuatao ni baadhi ya wanaume wenye jukumu katika Bibilia;*

- *Kama afisa wa serikali Yohana 4:46-53*
- *Kornelio katika matendo ya mitume.*
- *Mlinzi wa gereza kule Filipi katika matendo ya mitume 15.*
- *Mtume Paulo katika 1 Wakorintho 9, na 2 Wakorintho 8.*

Kwa mafundisho ya ziada unaweza kuyapata katika Hesabu 30:6-8. Yanahuiana na wamama walio manyumbani mwenu,mkeo na binti zako.

Kuna vitu viwili viasivyoweza kutenganishwa pasipo kudhuru pakubwa,walio karibu nawe.Vitu hivi ni mamlaka na jukumu.

Tunaweza kuyaona katika watoto wadogo. Mmoja wao anataka awe na mamlaka. Anataka awe msimamizi. Na wakati shida anapotokea kutokana na uongozi wake; anaelekeza lawama kwa watoto wengine. Hataki jukumu la kutumika. Kihistoria tumeona jambo hili likitokea kwa wafalme. Katika historia ya hivi majuzi, hitilafu iliopo katika maraisi wawili wa nchi ya Marekani. Walipokuwa uongozini walikuwa na mamlaka nyingi kuliko mtu yeyote duniani. Rais Truman

alikuwa na nguvu sana na alizitumia. Pia alikubali jukumu lake kwa vitendo. Kwa meza yake alikuwa na ishara isemayo, “mateke yakomee hapa”. Hangeweza kuhepa yale mateke. Pia rais Clinton alitumia mamlaka yake, *lakini hakusita kuhepa, kudanganya na kulaumu wengine. Upande wa kujiamini hakuwa mume, baba, kiongozi au rais mwenye jukumu.*

*Mkristo aliye kama mume, baba, pastor, au kiongozi wa kidunia, hana ruhusa ya kuwa msimamizi, sawasawa na daraja la uongozi, anastahili kuamrishwa;*

**Kama mume:**

*Waume, wapendeni wake zenu, kama vile kristo alivyopenda kanisa, na akajitoa kwa ajili yake, ili alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno, na apate kujiletea kaqnisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi, wala lolota kama hayo, bali liwe takatifu lisilo na mawaa. Vivyo hivyo inawapasa waume nao kuwapenda wake zao kama miili yao wenyewe. Ampendaye mkewew hujipenda mwenyewe. Maana hakuna anayeuchukia mwili wake popote; bali huulisha na kuutunza, kama kristo aivyolitendea kanisa- kwa kuwa tuu viungo vya mwili wake (Waefeso 5:25-30”NIV=TMK”)*

**Kama baba**;
*Akina baba msiwachokoze watoto wenu bali mwalee katika adabu na maono ya Bwana. Waefeso (NIV=TMK)*

**Kama Bwana mkubwa;**
*Nanyi akina bwana watendeeni hoa yayo hayo, mkiacha kuwaogofya, huku mkijua yakuwa yeye aliye Bwana wao na wenu yuko mbinguni, wala kwake hakuna upendeleo. Waef 6:9 (NIV=TMK*)

**Kama wazee**
Kwa wazee walio kati yenu mimi nawasihi kama mzee mwenzi wenu, na shahidi a mateso ya kristo na mshiriki wa utukufu utakao funuliwa badaye; lichungeni kundi la mungu lililo kwenu na kulisimamia, si kwa lazima bali kwa hiari kama Mungu atakavyo si kutaka fedha fedha ya aibu bali kwa moyo. Wala si kama wajifanyao Mabwana juu ya mitaa yao, bali kwa kujifanya vielelezo kwa lile kikundi. Na mchungaji muu atakapodhihirishwa mtapokea taji ya utukufu, ile isiyokauka. 1 petro 5:1-4 (NIV=TMK)

Ufahamu, kwa kutokuwepo ushauri utakaoshurutisha utiifu wako. Ufahamu ule uhakika wa nia na vitendo vimpasavyo mume, baba, Bwana kubwa na mzee kiongozi. Sehemu ya jukumu letu ni kuelemisha vijana wetu kuwa na jukumu.

Mtu awezaje kuwa mme mwenye jukumu?

Uyatambue yale maono yampasayo mtu mkristo.

Ukiri dhambi ya ile nia yako na vitendo vibaya.

Chagua kuwa mtiifu wa amri za Mungu katika Bibilia.

Wewe mwenyewe uchague kuelimishwa na watu waliojumuika, kupitia kwa vitabu, kanda za kaseti na video.

Je, wewe una dhambi zozote kwa hizo zilizo hapo juu au sawa na hizo? Ikiwa ni hivyo, mtafute Kristo na umwambie unataka kuwa mkristo. Soma *injili* iliyo kwa ukurasa wa 40. Chukua Bibilia na usome ; Mathayo,Marko,Luka,Yohana,Matendo ya Mitume na Warumi. Nipigie simu, niandikie au nitumie barua pepe.

Ikiwa wewe ni mkristo unastahili;

1. Ukiri dhambi zako kwa Mungu na kila dhambi kwa namna yake. Na tuifanye kuwa imara, ukiri nakuachana nazo. Zikatae, jitenge nazo! Zitubu kwa Mungu na upokee usafisho na ile kazi ya utakaso ya damu ya Kristo. 1 Yohana 1:5-10
2. Uwe mwenye kutii, susia kabisa katika neema ya Mungu, kulaumu wengine kwa jambo lenye haliend vyema wakati ulikuwa msimamizi.
3. Chagua kutoa huduma ya kiroho, chakula, nyumba, upendo, usalama, ulinzi na faraja kwa wako na watoto. Na hiyo iwe kazi yako ya kwanza.
4. Ukitaka kubadilika baada ya wewe kukiri, uenende sawa na mtu yule anayekuhitaji kukufunza kwa mfano na kukuelekeza, jinsi ya kujumukika
5. Uwe kitabuni, ukisoma na kujifunza kwa lengo la kumtii Mungu.
6. Omba msaada kwa Mungu.

# N Y A R A K A

**MASWALI NA MAJIBU JUU YA KUWA MKRISTO**

Wakati mmoja hapo 1997, mwanamke mmoja alijipatia nakala ya *jinsi ya kuwa huru kutoka kwa uchungu*. Alitetemeshwa alipoisoma na akanitumia posti kadi. Nilitambua ya kwamba alikuwa anaumia vibaya sana kwa hivyo nikampigia nione kama naeza kumsaidia.Akaniandikia tena. Nilihifadhi barua zake pamoja na nakala zangu za majibu. Yafuatayo ni maafikiano yetu ya miezi mitatu. Kwa ruhusa yake tulitoa nakala arobaini ili kusaidia watu wenye maswali sawa na hayo. Tulifanya hivyo kwa mara nyingi kwa zaidi ya nakala elfu. Tangu wakati ule tumechapisha nakala zingine elfu kumi.

Tumehusisha maafikio yaliyomo katika toleo hili la *Jinsi ya kuwa huru kutoka kwa uchungu*. Tunatumai kuwa hili litakuwa la msaada kwa wengine wenu walio na maisha kama hayo.

## S E P T E M B A 1

Muhebi Jim,

Nilitaka kukuandikia ili kukuambia kuwa ningali nachunguza. Haijakuwa rahisi kwangu kama ilivyo na wengine, lakini ningali na jaribu.

Ninasoma Bibilia kila siku na kuomba, ingawaje sijaelewa ni kwa nini. Nimesoma kitabu kimoja kati ya vile ulinitumia kuhusu umishonari (Uchina) na nimeanzisha ukristo changa. Shida ni wakati.

Nimefurahia vitabu ulivyonitumia na wakati uliotumia kuongea nami kwa simu. Lakini samahani kwa vile nina kiasi kidogo sana kuhusu wakristo na yote wanayoamini.

Nisomao zaidi na kuongea na wengine, ndipo nitambuapo zaidi kizuizi changu kikubwa ni tumaini na imani. Ni vigumu zaidi kwangu kutegemea mtu yeyote au kitu chochote. Ninataka kubadilika. Nilishangazwa sana uliponiambia unataka nimpokee Kristo alafu kanisa. Kila siku mimi hukumbuka maneno haya na kujiweka kwa maombi. Kwangu ni upuzi na utoto lakini nimepiga hatua.

Nilitaka kukutumia pesa za vitabu, lakini sikuweza. Kupokeas mazawadi ni ombi ligumu sana kwangu. Nanatumainia kukulipa wakati mwingine nitakapokusudia kumsaidia mtu mwengine jinsi umenisaidia mimi.

Nitaendelea kujaribu na hivi karibuni nitakapo faulu, nitakuandikia na kusema “ Ninajua ni kweli. Ninatambua yeye ni nani”

Asante sana.
Hadi wakati huo,
Vickie.

## S E P T E M B A 1 8

Muhebi Vickie,

Asante sana kwa kujieleza kwa barua yako nzuri. Ndani mwake uliyaeleza mambo kadha wa kadha.;

1. “ Ningali ninajaribu”
2. “Kizuizi kikubwa ni tumaini na imani”
3. “Kwangu ni upuzi na ni utoto”
4. “Kupokea mazawadi ni jambo ligumu sana kwangu”
5. “Nitaendelea Kujaribu”

Majibu kwa nambari 1 hadi 5:

Namba 1:Epuka kujaribu. Hauwezi “Kutumaini” na “Kujaribu”yote mawili kwa pamoja. Shida yako kubwa ni “Kujaribu”. “Kujaribu” ni sawa na kusema “itegemeavyo wewe”. “Kutumaini “ ni sawa na kusema “tegemea mtu mwengine”. Huo hautakuwa busara isipokuwa hao watu wengine wawe waminifu. Epuka kutazama na kuibagua imani yako. Badala yake utazame ule uaminifu wa Mungu.

Namba 2: Kukuwa mkristo haikugarimu imani nyingi, au imani ya nguvu. Inagarimu imani kidogo sana kwa huyu Mungu mwaminifu.Kwa maneno mengine Mungu hufanya uokozi sio imani yangu.Tumaini na imani hutoka kwa Neno la Mungu. Huletwa kwa kuhubiri Kristo. Warumi 10:17. Huzuiliwa kwa “kujaribu” na kwa kuitazama imani yako.

Nambari 3:Kwangu ni upuzi na ni utoto;*Yesu anasema, “Amini nawaambia, msipoongoka na kuwa kama vitoto, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni. Basi yeyote ajinyenyekeshe kama motto huyu, huyo ndiye aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni. mathayo 18:3-4.Yesu akasema wacheni watoto wadogo waje kwangu, wala msiwazuie kwa kuwa watoto*

*kama hao ufalme waq Mungu ni wao. Amin nawambia mtu yeyote aiye upokea ufalme wa mungu kama mtoto mdogo hauingii kamwe. Lk 18:16-17.*

Nambari 4: Madhumuni ya zawadi kuwa njia ya kipekee, ni kwa sababu - Mbingu ina karama kubwa mno kununulika. Njia ya kipekee kuipata ni kwa mmoja yule akupendae na anauweza wa kuipeana kwako.

*Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya mungu ni uzima wa milele katika Yesu Kriso bwana wetu. (Warumi 6:23*)

*Pia nasi wakati moja tulikuwa hatuna akili, waasi, tumedanganywa na kufanywa kuwa watumwa kwa kila namna na tamaa na anasa nyingi. Tuliishi katika uovu na uhusuda tukichukiza na kuchukiana. Lakini wakati wema na upendo wa Mugu wetu ulipofunuliwa, alituokoa, si kwa sababu ya matendo na haki tuiliyotenda sisi; bali kwa rehema yake. Alituokoa sisi kwa kupitia kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa mara ya pili na kufanywa upya na roho mtakatifu, alitumwagia kwa wingi, kwa njia ya Yesu kristo mwokozi wetu ili kwamba kwa kuhesabiwa haki kwa neema yake, tupate kufanywa waridhi wa milele, kama lilivyo tumaini letu.* (Tito 3:3-7)

Tafadhali usome Yohana 1:1-4, Waebrania 1:1-4, Wakolosai 1:13-20. Mafungu haya yatueleza mambo mawili yenye msingi wa kweli;

1) Mwana wa Mungu,akiwa na Baba,ndiye mwuumbaji wa kila kitu na kila mtu.
Sisi sote ni wake. Alituumba sisi.

2) Alitukomboa nasi. Yani, aliturudisha kwa kutununua kwa kifo chake pale msalabani. Sisi ni wake. Alitununua na kutuumba sisi!

Tafadhali pia soma Warumi 5:6-8, 4:24-25. Sina uhakika ikiwa umewahi kusoma injili zote nne; Mathayo, Luka, Marko na Yohana. Hizi ndizo msingi

Nambari 5:Kumbuka, jiepushe na kujaribu. Itikia ile kweli unapoisoma. Usipingane na maandiko matakatifu.

Katika Bwana wetu Kristo
Jim.

## S E P T E M B A 2 9

Muhebi Jim,

Nilipoanza kusoma barua yako nilifarijika. Ilikuwa yenye maono sana. Nimekuwa nikijaribu kwa bidii sana…..na sijafika popote; hata hivyo mambo mengine yameniendea vibaya sana.

Nimekuwa nikingojea muujiza fulani – komeo la umeme— lolote lile, lakini hakuna ambalo limetendeka. Bibilia inasema kwamba; ikiwa nitaamini na kuomba, hilo ndilo la pekee ninaweza kulifanya. Nimesoma, nimeomba na kuuliza. Na sasa nitamgeuzia Mungu yale mengine yote. Ikiwa yatakuwa vile, nitayaacha yote yawe juu yake. Kuna uwezekano hili liwe tamushi langu kubwa la imani maishani mwangu mwote.

Ninakubaliana sana na barua zako pia na simu yako. Nina furaha sana kukuandikia.Ni watu kama wewe ndio hufanya watu kama mimi kuhitaji ulichonacho. Sijawahi kukutatana nawe, bali najua unampenda Bwana kwa moyo wako wote. Unaonyesha kwa yale yote umenitendea.

Nitazidi kusoma na kuomba. Pia nitakuombea nawe! (Lingali linaonekana ni utoto kwangu! Ninabashiri hilo pia kuwa sawa!) Kuanzia Jumanne nitakuwa nikishiriki somo la Bibilia katika kitabu cha Yohana. Nimevutiwa sana!

Wewe ni mtu wa ajabu sana-Ahsante.

Pendo daima
Vickie.

## O K T O B A 9

Muhebi Vickie,

Asante kwa barua yako nzuri. Wacha nikudondoe tena kwa kukuandikia.

"Nimekuwa nikingojea muujiza fulani – komeo la umeme— chochote kile,lakini hakuna ambalo limetendeka. Bibilia inasema kwamba; ikiwa nitaamini na kuomba, hilo ndilo la pekee ninaweza kulifanya. Nimesoma, nimeomba na kuuliza. . Na sasa namgeuzia Mungu mengine yote. Ikiwa yatakuwa vile, nitayaacha yote yawe juu yake. Kuna uwezekano hili liwe tamushi langu kubwa la imani maishani mwangu mwote"

Jinsi nilivyodokeza katika barua yangu ya hapo awali, unaweza kuwa umejitahidi sana. Labda hili lingali ndilo shida . Ningeuliza swali, lakini sasa imenibidi ningoje jibu; kwa hivyo badala yake, nitatazama tu na kutoa ushauri;

Unliposoma, ulisoma kwa bidii.
Ulipoomba, uliomba kwa ushupavu.
Ulipouliza, uliuliza kwa juhudi.

Ulitumainia bidii yako, juhudi na ushupavu wako ukushushiye komeo la umeme au lolote lile. Hata ulipomgeuzia Mungu, ulimsukumia na kumwachia yote juu yake. Hata ulipotoa tamko kubwa la imani, hakika ulinena kwa (muda mrefu na ukazidi kiasi).

Je, unaona kusoma, kuomba, kuuliza, kugeuka, kutamka na kuacha kwako bado ni kule kwa kibinadamu? Wokovu ni wa Mungu.

*Basi, ndugu zangu nawaamuru ile injili niliyohubiri; ambayo ndiyo mliyoipokea na katika hiyo mnasimama na kwa hiyo mnaokolewa; ikiwa mnashika maneno niliyohubiri isipokuwa mliamini bure. Kwa maana niliwatolea ninyi hapo mwanzo yale niliyoyapokea mimi mwenyewe ya kuwa kristo alikufa kwa dhambi zetu, kama yanenavyo maandko; ya kuwa alizikwa na kufufuka siku ya tatu na kumtokea Kefa na wale Thenashara. (1 Wakorintho 15:1-5)*

Kwangu inaonekana kuwa wewe unang'ang'ana sana ili "kushika kabisa"kuliko jinsi ulivyo kwa kile ambacho umekishika. Hili ni Neno ambalo unalishika, chakula chake, kufa kwake kwa dhambi zetu, kuzikwa kwake, na ufufuo.

Tafadhali yatafakari haya;

1) Utakatifu wa Mungu.
2) Uovu wako katika nuru yutakatifu wake
3) Neema Yake ni kuu kwako liko dhambi zako (warumi 5:20)

Tafadhali usiweke imani yako kwa kujiamini .Hapa nina ushauri,usadiki kwamba umeongeza juhudi yako,na ikiwa utayasema haya kwa Mungu bila kufanya ombi la kujidai.

"Ee Mungu,uniwue radhi mimi mwenye dhambi"(Luka 18:13) na "Asante sana kwa wokovu na msamaha wa dhambi katika jina la Yesu".

Utayaona yafuatayo kama dhibitisho maishani mwako;

1 Yohana 3:14— upendo wa kristo
1 Yohana 2:3 —Utii.
1 Wakorintho 2:14— Ufahamu.
Wagalatia 5:19-23— Tunda la roho.
Yohana 13:34-35— Upendo wa kristo.
Yohana 5:24 ——Mpokee kwa neno lake.
Waebrania 12:5-11 —Utakaso.

Mambo haya ni hakika kwa wale tu walio wakristo wa kweli. Ikiwa hautayaona haya katika maisha yako, basi wewe ungali nje ya wokovu. Hatahivyo, nawazia haitakuwa hivi.

Katika Bwana Yesu Kristo
Jim..

---

**O K T O B A 12**

Muhebi Vickie,

Alasiri hii nimekuwa nikisoma- Marko 10. Ningependa usome na kulinganisha hadithi hizi mbili za yule Mtawala chipukizi na Tajiri, ukianzia- Marko 10:17 na yule kipofu Batimayo, ukianzia aya ya 46. Baada ya kuzisoma uyatafakari haya:

| **Barubaru tajiri** | **Bartimayo kipofu** |
|---|---|
| 1. Tajiri | 1. Mwombaji |
| 2. Kukimbia | 2. Ameketi |
| 3. Afya nzuri | 3. Kipofu– akatupa vazi lake |
| 4. Nifanye nini ili niuridhi uzima wa milele. | 4."Mwana wa Daudi nirehemu" |
| 5. Amri 6 (Yesu) | 5. "Wataka nikufanyie nini?" |
| 6. "Yote nimeyashika" ( Tajiri) | 6. "Mwalimu wangu nataka |
| 7. "Umepungukiwa na neon moja" Ukauze, ukawape, na njoo Unitafuate.(Yesu) | 7. " Enenda zako imani yako mekuponya" |
| 8. Akaenda kwa uzuni. | 8. Mara akapata kuona akamfata Yesu. |

Mtu wa kwanza alidhani anaweza kuyashika, naye hakuweza, akeanda zake kwa huzuni. Na wa pili alijua hawezi na kwa hivyo akamwamini Yesu -asili 100%.

Mpenzi Vickie, naamini umekuwa kama Batimayo, kwani mwenendo ni huo huo.

Katika Bwana wetu Yesu kristo,
Jim.

## O K T O B A 19

Muhebi Jim,

Ahsante sana kwa barua yako ya mwisho. Ni ya busara; inaonyesha kuwa mepesi, rahisi na ni karimu.

Umebashiri sawa yale yote nimekuwa nikijaribu kuyafanya. Nimelichukua pendekezo lako. Niliomba ulipokuwa ukiandika. Kila siku ninamsihi Mungu anijalie maishani mwangu na kuniongoza katika chaguo la mapito yake. Ningali ninachukua muda mwingi kujizuia, lakini namsihi Mungu anisaidiye zaidi.

Sielewi mambo mengi. "Kwa nini" – ni nyingi mno. Ni vigumu sana kwangu kueleza ni aina gain ya upendo Mungu hupeana. Nimechukua muda wangu mwingi nikiwazia jambo hili – nimeona niachane nalo. Kila wakati imekuwa vigumu kwangu kuwazia; kuna mtu ambaye ananipenda kweli! Nina uhakika huu ni utoto – lakini umeniandama aitima ya utu uzima. Mungu annipenda na kwa msahada wake, nitajifunza kuyakubali.

Nilisoma hadthi hizi mbili katika Marko kuhusu yule mtu tajiri na kipofu. Sisemi nii tajiri bali kulinganishwa na wengine, mimi nimebahatika. Ninahitaji kuwa na shirika na Mungu. Kunusurika kwangu kimaisha, kumenisaidia sana kuishi hata nyakati za ugumu. Hivi majuzi nimetembua ni nini chanzo cha kunusirika kwangu; na kila wakati imekuwa – Mungu. Mara nyingi watu wamestaajabia juhudi niliyo nayo ya kustahimili mambo wao hudhania hawawezi kuwa nayo. Ingawaje sikuwauliza, nimefahamu kwamba sikuyapitia pekee yangu. Mimi nimelindwa na Mungu. Ninaweza kutazama nyuma na kuyaona vyema sasa. Uchungu niliouona maishani mwangu, ungeniondoa uhai wangu - lakini haukuweza. Kila wakati nimekuwa nikiona kuna kisababu cha mimi kusonga mbele, kuuweka mguu wangu mbele ya mwingine – nikitumainia kesho iliong'aa – kila wakati nikifahamu ya kwamba watu wengine waling'ang'ana na hali mbaya sana hata kuniliko

1)Ijapokua nilijaribu kutabasamu, haidhuru kwa lolote lililo kuwa ligumu, bali kwangu yaliwezekana— kwa sababu Mungu alinioa ulinzi.

Nitamshukuru Mungu kila siku kwa kunipenda mimi – akitosheka kumtazama mwanawe jinsi alivyo vumilia uchungu mkuu kwa ajili yangu. Siwezi fikiria ni uchungu ulioje ukiutazama – najua haungependa kuona ikwa ungetaka. Ninahitaji kumkaribisha Mungu moyoni mwangu mara mia moja kila wakati kwa sababu huwa ninajitahidi sana. Nitajifunza kwa uwezo wake na anaweza kunibadilisha.

Nimependa barua yako – siku moja tutakutana – Asante kwa kuchukua mudfa wako na kujali kuniandikia na kunipigia simu.

Wakati mwingine huwa ninajazwa sana – inastajabisha! Nina shangazwa jinsi inavyonionekania vizuri. Ni vigumu sana niwazie mambo mengine.

Jim, ninajua wee unatembea na Mungu. Nitakuombea wewe na kazi yako pia. Ninatumai unaelewa jinsi umekuwa chombo cha dhamana kunisaidia mimi. Nina uhakika kuwa umesaisia wengi kwa msaada wa Mungu. Mungu akipenda, wakati mmoja nitamsaidia na mwengine pia.

Pendo langu kila wakati,
Vickie.

## O K T O B A 24

Muhebi Vickie,

Barua yako ya tarehe 19 imeasili hivi leo. Jibu lake litakuwa fupi sana. Kwanza nitakunakili wewe mwenyewe:

"Kila siku ninamsihi Mungu anijalie maishani mwangu na kuniongoza katika chaguo la mapito yake".

"Kila siku ninahitaji kumkaribisha Mungu maishani mwangu mara 100 na ndio maana huwa na jitahidi sana".

Wewe huwa unamsihi Mungu kila siku ukidhani inakupasa kumwomba mara 100 kila siku.

La, haistahili kumwomba Mungu mara 100 au mara moja kwa siku. Sababu ufanye hivyo, ni ikiwa alikutembelea na akaondoka kwenda zake. Ikiwa alijibu mahitaji yako, haustahili kuomba zaidi ya mara moja, siku zote za maisha yako. (Hakika haustahili kumsihi hata kidogo – tazama! "Krismasi yaja …. " kwa ukurasa ufuatao).Ikiwa aliingia ndani Alisema "sitakupungukia kabisa wala sitakuacha kabisa". Waebrania 13:5. Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapoteza kamwe; wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu. Baba yangu aliye nipa hao ni mkuu kuliko wote wala hakuna mtu awezaye kuwapokonya katika mkono wa baba yangu. Mimi na baba tu umoja" Yohana 10:28-30; na sehemu ya mwisho ya warumi 8:31-39.

Epuka kumsihi! Mpe shukrani na umulize kufanya hivi mara 100 kwa siku.

Tena nikikunakili wewe…………

" Ni ya busara, inaonyesha kuwa mepesi, rahisi na ni karimu".

Krismasi yaja. Marafiki na jamaa watakuletea zawadi. Zimelipiwa tayari, kufungwa na jina lako kuandikwa juu yake. Je, utamwendea kila mpaji na "kumwitisha" zawadi yako? Je, utaziitisha mara mia moja?

Hautahitaji kuziuliza kamwe. Unaweza kuenda zako, ukose kuzipokea, ukose kuzifungua na kuziache papo hapo. Unaweza kuzikataa, lakini hauhitaji kuziitisha. Wokovu wako ndivyo ulivyonunuliwa, ukalipiwa na jina lako likiwa juu yake.

> *Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya kristo amekuwa kiumbe kipya;ya kale yamepita tazama; Yamekuwa mapya. Lakini vyote pia vyatokana na Mungu aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwa kristo. Naye alitupa huduma ya upatanisho; yaani; Mungu alikuwa ndani ya kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, asiwahesabie makosa yao, naye ametia ndani yetu neno la upatanisho. Basi tu wajumbe kwa ajili ya kristo. Kana kwamba Mungu anasihi kwa vinywa vyetu; twawaomba ninyi kwa ajili ya kristo mpatanishwe na Mungu. Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate haki ya mungu katika yeye. (2 Wakorintho 5:17-21).*

Kwa niaba ya Kristo ninakusihi,"Upatanishwe kwa Mungu" Usiombe wewe; Yeye amekwisha kuomba. Wewe ni kupokea na kumshukuru.

Haujaniambia lolote kuhusu maisha yako. Usione ni lazima kwa kusikia hivyo. Umenisimulia mengi kuonyesha wewe ni "nusura" asiye – tishika. Na sababu hii imekufanya uone ugumu wa kumwamini Mungu. Mungu hawezi kuonekana kuwa mwaminifu ili hali umejiamini wewe mwenyewe.

Hatahivyo, umeelewa vyema sasa.

Zisahahau hizo "Kwa nini" zako. Je, kama ungelipewa wewe, ungeliweza kuonyesha umeyatoshelesha kuyajibu? Ikiwa chumba kina giza hauwezi kuuliza "Jinsi"au "kwa nini" stima haiwaki kabla haujabonyeza kiwashio.

Haukukataa kuzaliwa kwa sababu haukujua "jinsi"au "kwa nini" ubongo wako, moyo na figo zako zinavyofanya kazi. Haukumsisitiza daktari maalum (PhD) kuchungua maumbo yako kabla ya kuzaliwa.

"Kwa nini" zako zitajibiwa baadaye, au labda haitakuwa na maana yeyote kwako.

Katika Bwana wetu Yesu Kristo,
Jim.

---

## N O V E M B A 1

Muhebi Jim,

Nimebahatika sana wewe kuwa sehemu ya maisha yangu. Nyaraka zako zimekuwa zenya ubusara kwangu. Imekaribia sana [nikama] umegundua kile ninacho wazia. Ahsante sana kwa kunipa muda wako. Asante kwa uvumilivu wako.

Ninaposoma barua zako ninajuta kwa kukosa maarifa. Umekuwa haki kwa ushawishi wako.

Wiki hii ninasoma kutoka ufunuo wa Yohana au labda kuanzia kesho mapambazuko. Ninajua nitahitaji kusoma, kuchunguza na kuomba kwa miaka mingi, ili nipate kufahamu maandiko kama wewe. Kwa matumaini Mungu atanipa fursa hiyo.

Nimemuomba Mungu aniongoze kuchagua kanisa nitakaloshiriki. Ningali ninangojea jibu. Sioni kama nina ufahamu zaidi kufanya uamuzi huo.

Ingawaje ninataka kubatizwa, nilimwambia Brat kuwa ningependa kufanya hivyo ikiwa unaweza kunibatiza. Sina uhakika na "Utaratibu" wa ubatizo. Je, utahitaji kubatizwa na kiongozi wa kanisa?" Uzoefu wangu wa kidini hauwezi kunisaidia kulijibu swali hilo kwa sasa.

Ninalihisi hitaji la kuandikia kanisa la Katoliki barua kuwajulisha kweli ninayoamini hivi sasa. Ninaelewa kuhama kwangu kutaonekana ni duni kwao. Wadhamini wangu wa ubatizo watakasirishwa sana na jambo hili.

Inashangaza yale nimekuwa nikiyaskia kwa watu, sijayasikia kwa miaka sasa tangu nimtambue Kristo. Siwezi kukawia kuyashiriki nao!

Ninajua sijakufunulia mengi kuhusu maisha yangu. Nina miaka 35, nimeoleka na nimejaliwa wana wawili. Hii ni ndoa ya pili kwa mume wangu na kwangu mimi. Mume wangu alijaliwa watoto wawili kwa ndoa yake ya kwanza – lakini wakafa (Ungonjwa wa ajabu). Tulimzika yule mdogo miaka mbili iliopita na yule mkubwa miaka tano iliyopita. Imekuwa pigo kubwa na la uchungu jumla kwa jamii yote, haswa mume

wangu. Ana uchungu mwingi sana. Anasema haamini Mungu na yeye ni kafiri. Tena kwa kinywa chake hicho atakwambia; angemchukia Mungu anayeruhusu binti zake kuteseka kwa muda mrefu na kwa hali ngumu sana. Nimekuwa nikimwomba kila siku.

Nimewalea watoto wawili kafiri – Kuna mmoja chuoni na mwingine shule ya kati. Hawatofautiani kabisa na mama yao. Lakini wananipenda na kuniheshimu. Ni watoto wakubwa lakini hawamjui Bwana. Pia ninawaombea kila siku.

Maisha yangu ya hapo awali yalikuwa mchanganyiko wa dhulumu na dhuluma. Mamaangu alikuwa ni (angali) mlevi kupindukia. Nilipofika umri mkubwa "kujizuia" nilitoroka nyumbani. Nilijifungua mtoto wa kwanza nikiwa na umri wa miaka 16. Tangu wakati huo, maisha yangu yaliadhirika kwa sababu nilifanya uamuzi mbaya (nilitumia madawa, pombe na wanaume). Nilipotimia miaka 21 (sasa hivi ni mama mzee) niliacha kutumia madawa. Nikawa mja mzito tena, nikaoleka (sio kwa baba mtotoangu). Tukahamia kule Carlifinia. Hakuwa mwaminifu. Tuliamia urudi Utah na baada ya muda mfupi tulitalikiana.

Nilirudia tena kuwa na uhusiano wa kirafiki tu na baba bintiangu (baba ya kijanaangu aliyefariki) kama urafiki tu. Akawa na uhusiano angalau na bintiangu; akawa mmoja katika "jamii yetu" (pia na mume niliyenaye sasa). Naye (babaake bintiangu) alikufa miaka mbili iliyopita; muda mfupi tu baada ya binti - akambo wangu.

Katika yote haya; magonjwa, uchungu, kung'ang'ana na vifo maishani mwangu, nimegundua jinsi nilivyokuwa na bahati kwa miaka michache iliyopita. Ninao watu wa karibu katika jamii yangu ambao hawajawahi kubahatika.

Nimefaulu katika biashara. Nampenda mume wangu na watoto wangu. Vitu vyote vya asili nilivyokosa utotoni mwangu, watoto wangu sasa wamevifurahia. Nimejielemisha mwenyewe, watoto wangu na kujishirikisha katika raha ya kila aina, ipatikanayo kwa fedha- NA NIMEJIHISI KUWA NA UPWEKE SAWA NA VILE NILIVYOKUWA UTOTONI.

Ninatabasamu kwa mara ya kwanza maishani kwa sababu nina jihisi tu ni mwenye furaha.(Hapo awali kutabasamu na sarakasi vimekuwa hila). Sina shaka na nia yangu, kwa vile Mungu amenisaidia sana kunusirika, ingawaje sikumjua. Na kwamba ninamjua sasa na kila siku ninajifunza mengi kumhusu; na ni vigumu sana kueleza jinsi nilivyo na furaha.

Ameanza kutenda kazi maishani mwangu. Na hii ndio mara yangu ya kwanza kujisikia napendwa kwa kutofanya lolote. Upendo nimekuwa nao katika maisha ya hapo awali umekuwa wenye vikwazo, angalau nimesikia hivyo.

Simtambui babaangu mzazi, ingawaje nina kumbuka akinitembelea wakati mmoja. Nampenda hata bila ya kumfahamu yeye. Miezi sita iliyopita nilimtafuta nikapata alifariki. Allikufa miaka minne iliyopita. Ningelianza msako wangu mapema, ningelimjua. Katika maisha yangu sikuliona umbo la babaangu na sitamwona tena. Kama singelikuandikia singelianza kumtafuta Mungu. Na kwa vile nimempata sitaki kumwacha! Asante tena kwa kunisaidia.

Pendo.
Dadaako katika Kristo!
Vickie

---

**D I S E M B A 11**

Muhebi Jim,

Sijakuandikia kwa muda mrefu – na sijapata majibu kwa barua zako. Ninatumaini yanakuendea vyema pamoja na jamii yako.

Nimekuwa nikishugulika na kazi nyingi sana. Wiki mbili zilizopita nimekuwa mnyonge. Nimekaa tu hapa nikitafakari ni kwa nini, na sasa nimeelewa. Sijakuwa nikisoma kila siku na kuchunguza nilivyokuwa nikifanya. Pia sijakuwa nikiomba kila mara kama hapo awali.

Usiku kucha nilisoma na kuomba, na nikasikia vizuri sana. Na leo sijafanya lolote bado na pole pole unyonge umeanza kuniingia tena. Na kwa hivyo nikaamua kukuandikia barua (ambapo nimerudia kuiandika kwa muda sasa), na kwa hivyo nitarudia kusoma kama kawaida.
Kila mara wakati kama huu wa mwaka huwa mgumu sana kwangu kufurahia. Nikuwa nikitarajia mwaka huu uwe tofauti, lakini ninaona kuiofanya tofauti, ninahitaji kumtazama yesu na kumfanya makutano ya maisha yangu. Ninajua nikifanya hivyo, na mambo mengine yatakuwa salama. Sijui ni kwa nini sijafanya hivyo, na kwa nini nifanye kuwa ngumu

Mojawapo ya hii masika, nitakutembelea hapo kwa gari ili tuonane nawe. Na ikiwa itakuwa bahati utembee huku kabla sijakuja hapo, tafadhali nijulishe.

Swali kwako: usiku kucha tumekuwa tukisoma Yohana 11. Mtu anapokufa huwa anaenda mbinguni moja kwa moja? Basi ikiwa ni hivyo ufufuo ni wa nini? Ikiwa hapana, ni mahali gain walipo hadi kufufuliwa? Je, ufufuo ni zaidi ya mmoja ? Yesu alipofufuliwa kutoka kwa wafu alikuwa na mwili wa asili- je, pia nasi? Nimeshangazwa sana.

Uwe na Krismasi kuu, na pia bukheri wa mwaka mpya!!!

Pendo,
Vickie Meacham

**D I S E M B A 16**

Muhebi Vikie,

Barua yako ilifika alfajiri hii ikiwa na zawadi kwa jamaa kutoka kwako. Asante sana!. Mwanzo wako ni sawa (au ni sawa kiasi). Jambo la muhimu ni kuwa na wakati na Mungu katika Bibilia na kwa maombi ndipo uzidi kukaa katika furaha ya Bwana. Sehemu hiyo nyingine si kinga, bali ni dawa. Sehemu hiyo inaitwa kukiri dhambi. Leo nitakutumia kanda ya kaseti kuhusu somo hili pamoja na mwongozo kwa kijikaratasi ili upate kuelewa.

Kidogo tu, tafadhali, soma 1 john 1:5-10, usome mara kadhaa. Baada ya kusoma hiyo aya, uutazame uzuri wa hakika na kweli ulipo katika aya zenye nambari zisizo na ugao na ubaya ukanushao kweli katika aya zenye nabari zenye ugao. Jizoeshe kutenda aya ya 7 na 9 ukianza na aya ya 5, jiepushe kutenda aya ya 6, 8, na 10. Zisome aya zingine zote 1 Yohana, ukitizama na kushika neno unalolifahamu.

Na sasa ni swali lako kuhusu ufufuo wa mwili.
Nafsi inaenda mbinguni mara tu tunapokufa pasipo na mwili. Mwili tunauacha hapa hapa.

*Kwa maana kwangu mimi kuishi ni kristo, na kufa ni faida. Ila ikiwakuishi katika mwili kwangu mimi ni matunda ya kazi; basi nitakalolichagua silitambui. Ninasongwa katitkati ya mambo mawili; ninatamani kwenda zangu nikae na kristu maana ni vuzuri zaidi san; bali kidumu katika mwili kwahitajiwa zaidi kwa ajili yenu.*
(Wafilipi 1:21-24) pia tazama II Wakorintho 5:6-9.
2.Ufufuo unafanyika wakati Yesu Kristo anarudi pale mawinguni

*Lakini wandugu hatutaki msijue mkahuzunika kama na wengine wasio na matumaini. Maana ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa, akafufuka, vivyo hivyo na hao walio lala katika Yesu, mungu atawaletea pamoja naye. Kwa kuwa twaambieni haya kwa neno la bwana, kwamba sisi tulio hai, tutakao salia hata wakati wa kuja kwake Bwana, hakika hatutawatangulia wale waliokwisha lala mauti kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika, na sauti ya Malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo, watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani;na hivyo tutakua pamola naye Bwana milele. Bas, farijianeni kwa maneno haya (1Wathesalonike 4:13-18). Maandiko mengine kuhusu kipindi hiki ni 1 Wakorintho 15:47-54).*
3.Tutakuwa na mwili wa utukufu kama yesu, lakini ni baada ya yeye kurudi.

Lakini, wenyeji wetu sisi, uko mbinguni. Na kwa bidii twamtazama mwokozi kutoka huko, ndiye Bwana yesu kristo; atakayeubadilisha wetu wa unyonge, upate kufanana na mwili wake wa utukufu, kwa, uweza, ule ambao kwa hilo aweza hata kuviitisha vitu vyote viwe chini yake. (Wafilipi 3:20-21)

Pia 1 Yohana 3:1-3,Tito 2:11-14,Warumi 8:22-25.

Ni wako katika Bwana wetu Yesu Kristo,
Jim.

*Lakini wandugu hatutaki msijue mkahuzunika kama na wengine wasio na matumaini. Maana ikiwa twaamini ya kwamba yesu alikufa, akafufuka, vivyo hivyo na hao walio lala katika yesu, mungu atawaletea pamoja naye. Kwa kuwa twaambieni haya kwa neno la bwana, kwamba sisi tulio hai, tutakao salia hata wakati wa kuja kwake Bwana, hakika hatutawatangulia wale waliokwisha lala mauti kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika, na sauti ya Malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo, watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani;na hivyo tutakua pamola naye Bwana milele. Bas, farijianeni kwa maneno haya (1Wathesalonike 4:13-18). Maandiko mengine kuhusu kipindi hiki ni 1 Wakorintho 15:47-54).*

Tutakuwa na mwili wa utukufu kama yesu, lakini ni baada ya yeye kurudi. Lakini, wenyeji wetu sisi, uko mbinguni.

# I N J I L I

Baada ya kusoma jinsi ya kuwa huru kutoka kwa uchungu, unaweza kutambua ya kwamba wewe si Mkristo. Kama wewe ni Mkristo, waweza kuokolewa kutoka katika dhambi hii ya chukizo. Ikiwa wewe si mkristo, basi dhambi yako inaunganika na dhambi zingine na kuwa na tabia iliyo ya mazoea ya dhambi. Ili kuuondoa uchungu huu, unahitaji tabia ya zamani. Wewe mwenyewe hauwezi kuuondoa. Ni Mungu tu anaweza kukuondolea.

**Hapa Kuna sehemu yako.**

1. Inastahili kwanza uwe na hitaji la kuwahuru kutokana na hatia na hukumu ya maovu yako na nguvu ya dhambi.
2. Inakupasa kujua huwezi lolote katika hitaji hili.
3. Inakupasa kujua ya kwamba hautafanyika kuwa huru na kuwa mwema au kutokuwa mwema wala kwa njia nyingine itokanayo kwa nguvu zako mwenyewe.
4. Unastahili ujue Mungu amekwisha kukuokoa na akamtuma Bwana Yesu duniani hapa ili afe kwa ajili ya waovu. “kwa maana hapo tulipokuwa hatuna nguvu, wakati ulipotimia, kristo alikufa kwa ajili ya waovu.” Warumi 5:6 (NIV=TMK).
5. Siku tatu baada ya kifo hiki cha dhambi, Bwana yesu alifufuka toka mauti ili kutufanya sisi haki “Alitolewa kwa ajili ya makosa yetu na kufufuliwa ili mpate kehesabiwa haki. “ (Warumi 4:25).
6. Na sasa roho mtakatifu anakuelekeza wewe kuongoka dhambini mwako, ili kumwiitia Bwana Yesu, kumwaminia Yeye, kifo Chake na ufufuo.

*“Kwa sababu ulimkiri yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kutamani moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Warumi 10:9( NIV=TMK)”*

*“Na sasa wandugu ningependa kuwaarifu ile injili niliyowahubiria; ambayo ndiyo mliyoipokea na katika hiyo mnasimama, na kwa hiyo mnaokolewa; ikiwa mnayashika sana maneno niliyowahubiria isipokuwa mliamini bure. Kwa maana naliwatolea ninyi hapo mwanzo yale niliyoyapokea mimi mwenyewe, ya kuwa yesu kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko, nay a kuwa alizikwa, nay a kuwa alifufuka siku ya tatu, kama yanenavyo maandiko, naya kuwa alimtokea kefa; tena na wale thanashara” 1 Wakorintho 15:1-5 (NIV=TMK)*

Na ukishamwiitia Bwana Yesu, mshukuru kwa upatanisho wake kwa Baba, kwa kukusamehe dhambi zako na kukupa wewe uzima wa milele.

Basi kwa furaha ya kusamehewa kwako, mshuhudiye mtu yeyote jinsi Mungu amekutendea.

Ikiwa utatuandikia, tutakupa msaada wa vitabu na majarida ili vikusaidie kusimama katika maisha ya ukristo

<u>MANENO YALIYOTUMIKA</u>

NIV = New International Version
TMK = Tafsiri Mpya ya Kimataifa
Kipepesi =Fax
Mtarjumi = Translator
Barua pepe= E-mail
Mtandao = Website
Zana = Store
Karakana = Workshop
Sitashara = Mid sixteen
Barubaru = Teenager

**Mtarajimu:Evans Ipicha**

**Box 3461 COD 30200,**

**Kitale.**

**Barua pepe:evans_ipicha@yahoo.com**

# MASHIRIKA YA JAMII YA KIKRISTO

Labda umejipata una uchungu au umemkosa mwenzio,au wewe ni mdaku,mwenye kuuzunika au una uhusiano mbaya na wazazi wako. Ni uwezekano unajijua una mambo haya ndani mwako hata baada na kabla ya kukisoma kijitabu hiki ili kupata suluhu. Ikiwa hauyaelewi mashauri haya,au unayaelewa bali hauwezi kuyatenda,au, hautaki kuwa na badiliko,basi kuna uwezekano mkubwa una shida nyingine kuzidi,yani,wewe sio mkristo.Tafadhali uzisome *nyaraka kuhusu kuwa mkristo* pale ukurasa 45,pia Injili pale ukurasa 52.Tafadhali omba Bibilia ya Agano Jipya,kiswahili cha kisasa,vitabu—*Upendo Uzingira* na Festo Kivengere pia *Kuwa Mkristo* na Jim Wilson.Vitabu na Agano Jipya ni bure.Tafadhali niandikie au nipigie.Kwa njia hii nitaweza kuasiliana nawe kwa ufasaha,kwa wepesi na kwa undani, kweli hii ya habari njema ya Yesu Kristo.

***Attn:Jim Wilson***
***Community Christian Ministries***
***P.o. Box 9754***
***Moscow,ID 83843— 0180***
***Simu na kipepesi:(208) 883— 0997***
***Barua pepe: ccm@moscow.com***
***Mtandao:ccmbooks.org***
***Mtarjumi:evans_ipicha@yahoo.com***

Unaweza kuasiliana na yeyote kati ya waandishi wa vitabu hivi kupitia kwa anuani hii.

